

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 5 Mei, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

#### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

#### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

**NAIBU SPIKA:** Hati za kuwasilisha Mezani, Waziri wa Maji. Kwa niaba yake, Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Eng. Maryprisca Mahundi.

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Katibu!

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## **MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali. Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Mbagala sasa aulize swalii lake.

Na. 190

### **Hitaji la Shule Mpya Mbagala**

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuipa fedha Halmashauri ya Temeke ili iweze kujenga Shule mpya za kutosha kutokana na Jimbo la Mbagala kuongoza kuwa na wanafunzi wengi wa Shule za Msingi na Sekondari?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Jafari Abdallah Chaurembo, Mbunge wa Mbagala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha miundombinu ya elimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Temeke, katika mwaka wa fedha 2017/2018 hadi 2019/2020 Serikali iliipatia Halmashauri ya Wilaya ya Temeke Shilingi milioni 724 kwa ajili ya ujenzi wa Shule mpya ya Msingi ya Marten Lumbanga na Shule ya Msingi Dovya. Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri ya Wilaya ya Temeke kupitia mapato yake ya ndani imejenga jengo la ghorofa moja kwa ajili ya Kidato cha Tano na Sita katika Shule ya Sekondari Mbagala kwa gharama ya shilingi bilioni 1.056.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imiteitengea Halmashauri ya Wilaya ya Temeke shilingi bilioni 1.74 ambapo shilingi bilioni 1.53 zitaelekezwa katika Jimbo la Mbagala kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya katika Kata ya Chamazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali ilikamilisha maboma 10 ya madarasa ya Shule za Msingi katika Halmashauri ya Wilaya ya Temeke kwa gharama ya Shilingi milioni 137.5. Aidha, kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018 hadi 2019/2020 Serikali imejenga madarasa mapya 25 ya Shule za Msingi katika Halmashauri ya Wilaya ya Temeke kwa gharama ya shilingi milioni 500.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri ya Wilaya ya Temeke kuitia mapato yake ya ndani imejenga vyumba 76 vya madarasa ya Shule za Sekondari kwa gharama ya shilingi bilioni 1.72. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga Shilingi milioni 220 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 11 vya madarasa ya Shule za Sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Temeke. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Shilingi milioni 209 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya Shule za Sekondari.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo yanatia moyo, sasa nataka kujua; kwa kuwa Sera ya Serikali ni kuwa na Sekondari katika kila Kata: Je, ni lini sasa Serikali itajenga Shule za Sekondari katika Kata ya Mbagala, Kilungule na Kibonde Maji ambapo Kata hizo hazina Sekondari kabisa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili: Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kuongozana nami kwenda katika Jimbo la Mbagala kujionea hali ya msongamano wa wanafunzi darasani katika Shule ya Mbande, Chamazi,

Mianzini, Kilamba, Nzasa, Mbagala, Rangi Satu, Mbagala Kuu, Mzinga, Kilungule na Kijichi? (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameainisha baadhi ya Kata hususan Kata ya Mbagala, Kilungule pamoja na Kibonde Maji ambazo mpaka sasa hivi hazina Sekondari; na Sera ya Serikali ni kwamba kila Kata lazima iwe na Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Jimbo la Mbagala ambako anawapigania kwamba hizo Kata zote zitapata Sekondari za Kata ambazo zipo katika mpango wetu. Kwa sababu sasa hivi Serikali tuna mpango wa kujenga sekondari 1,000 nchi nzima katika zile Kata zote ambazo hazina sekondari. Kwa hiyo, mionganoni mwa Kata tutapeleka Shule za Sekondari ni pamoja na Kata alizozia inisha; Kata ya Mbagala, Kilungule pamoja na Kiponde Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Mheshimiwa Mbunge alikuwa anaomba tuongozane tukaone msongamano katika shule ambazo amezia inisha hapa ikiwemo Mbande, Chamazi, Rangi Satu, Mbagala Kuu, Mzinga, Kijichi na Kilungule; nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, nipo tayari, hata akisema baada ya maswali na majibu twende, mimi nitakwenda kwa ajili ya hiyo kazi ya wananchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante sana. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami siko mbali sana. Madhara yaliyopo katika Jimbo la Mbagala ni sawa sawa na Jimbo langu la Temeke.

Nimeona hapa Shule nyingi za Sekondari zimeenda kujengwa Mbagala, lakini Temeke bado tuna kiu; kama nilivyo sema siku zote, Temeke tunazaliana sana na sasa tuna watoto wengi wa Darasa la Kwanza. Tutakapofika mbali, naamini kabisa sekondari hizi zilizopo haziwezi kutosha hasa kule Vituka, Tandika, Kurasini, Mtoni, Temeke 14, kote tunatamani sekondari hizi ziwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kwamba kama atakwenda naye Mbagala, basi twende pamoja na Temeke tufike. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuahidi Mheshimiwa Mbunge naye kwamba tutakavyopanga safari ya Pamoja, Mbunge wa Mbagala pamoja na Mbunge wa Temeke tutakwenda. Nilainisha Kata za Mbunge wa Mbagala na wewe tutakwenda wote katika maeneo ya Vituka, Tandika, Kurasini, Temeke 14, kuhakikisha tunafanya kazi ya wananchi. Nanyi wote mnafahamu, Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kuondoa tatizo la Madarasa nchi nzima, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Alaudin Hasham Salim, Mbunge wa Ulanga sasa aulize swali lake.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Salim, naomba swali lake Na. 191 lipatiwe majibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga, inabidi nikuite kwanza ndiyo uzungumze. Mheshimiwa Asenga kwa niaba ya Mheshimiwa Hasham Salim.

Na. 191

**Tatizo la Barabara katika Wilaya ya Ulanga**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA - K.n.y. MHE. SALIM A. HASHAM** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani kutengeneza barabara za Ulanga na kutenga bajeti ya dharura ili *TARURA* iweze kukarabati barabara mara tu zinapoharibika?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuipatia *TARURA* ya Halmashauri Ulanga usafiri ili kuongeza ufanisi katika kazi zao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alaudin Hasham Salim, Mbunge wa Jimbo la Ulanga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha miundombinu ya barabara katika Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga, Serikali imeongeza fedha za matengenezo ya barabara kutoka shilingi milioni 471.49 katika mwaka wa fedha 2020/2021 hadi shilingi 671.49 katika mwaka wa fedha 2021/2022 ikiwa ni ongezeko la asilimia 42.4.

Aidha, Serikali imekuwa ikitenga 5% ya bajeti ya fedha za matengenezo ya barabara kwa ajili ya kazi za dharura. Kupitia fedha za dharura, *TARURA* katika Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga imejenga madaraja ya Epango na Ikangao kwa gharama ya Shilingi milioni 64.5 katika mwaka wa fedha 2018/2019.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua mahitaji ya magari kwa ajili ya usimamizi wa miradi ya barabara na uendeshaji wa ofisi za Mameneja wa *TARURA* katika Halmashauri zote nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga. Wakala una magari 192 yaliyopo katika hali nzuri kwenye Mikoa na Halmashauri, magari 107 mabovu na magari 15 katika Ofisi za Makao Makuu.

Katika mwaka wa fedha 2020/2021 *TARURA* imetenga shilingi bilioni 2.8 kwa ajili ya ununuzi wa magari 26 na pikipiki tisa. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022 *TARURA* imeidhinishiwa shilingi bilioni 2.8 kwa ajili ya ununuzi wa magari 30. Magari hayo yataapelekwa kwenye Halmashauri mbalimbali ambazo hazina magari na Halmashauri ambazo hazina Magari kama Ulanga, zitapewa kipaumbele. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa majibu mazuri, na kwa niaba ya Mbunge wa Ulanga Mheshimiwa Salim, naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa lazima ukitaka kwenda Ulanga upite Jimbo la Kilombero na kwa kuwa Wilaya ya Malinyi, Ulanga, Jimbo la Mlimba na Jimbo la Kilombero ni ukanda mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ni muhimu kuwa na timu ya dharura ya *TARURA* ikaenda kwenye eneo hilo kwa sababu Wilaya ya Kilombero, Jimbo la Mlimba, Ulanga na Malinyi hakuendeki?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili: Je, Mheshimiwa Waziri pia haoni kwa udharura huo akatafuta haraka iwezekanavyo gari la kuwapelekea wananchi wa Wilaya ya Ulanga kwa maana ya timu ya *TARURA* ikapata gari la dharura wakati huu wa mvua ambapo njia hazipitiki? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Jambo la kwanza ameionomba Serikali kupeleka timu ya dharura kwa ajili ya kwenda kupitia zile barabara ambazo zimebadilika na kufanya tathmini. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, hivi ninavyozungumza sasa hivi kuna timu zipo huko kwa ajili ya kuangalia zile barabara zote mbovu ambazo zilipitiwa na hili janga la mvua yakiwemo maeneo ya kule Malinyi. Kwa hiyo, watu wapo kazini na hiyo timu inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu katika Bunge hili wengi huwa wanatusikiliza sasa hivi, ninaagiza wapitie tena upya waangalle hiyo tathmini ya barabara ya Kilombero kupitia Ulanga inafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ameionomba kwamba tuwe na gari la dharura kwa ajili ya Ulanga. Kama nilivyoeleza katika jibu la msingi kwamba, tumeshatengewa fedha na katika hizo fedha tutanunua magari 30 na miongoni mwa maeneo ambayo tumeyapa kipaumbele, tutapeleka gari kwa ajili ya *TARURA* ni katika Jimbo la Ulanga. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Ulanga watapata hilo gari.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Barabara za Ulanga ni sawa sawa na barabara za Mlimba:-

Je, ni lini barabara ya kutoka Mlimba Mjini mpaka Tanganyika Masagati ambayo inatengenezwa na *TARURA* itawenza kukarabatiwa na kutengenezwa kwa sababu kutokana na mvua ni mbaya sana kiasi cha kuleta taabu ya kupitika? Ahsante sana. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Mbunge anauliza ni lini barabara ya kutoka Mlimba kwenda Tanganyika Msagati itajengwa kwa sababu ipo katika hali mbaya?

Mheshimiwa Naibu spika, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tumelipokea ombi lake na Ofisi ya TARURA watafanya tathmini na watatafuta fedha kwa ajili ya matengenezo ya eneo hilo. Ahsante sana. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na swalii la Mheshimiwa Jesca Jonathani, Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini.

Na. 192

#### **Huduma katika Hospitali ya Frelimo**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itarekebisha tatizo la Hospitali ya Frelimo ambayo inapata mgao kama Kituo cha Afya wakati ni Hospitali ya Wilaya ya Iringa tangu mwaka 2013?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, Mbunge wa Jimbo la Iringa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vya kutolea huduma za afya nchini ikiwemo Hospitali za Halmasahuri hupatiwa mgao wa fedha za ruzuku kwa ajili ya uendeshaji na ununuzi wa dawa na vitendanishi na vifaa tiba kwa kuzingatia vigezo maalum vilivyowekwa. Vigezo hivyo ni pamoja na idadi ya watu wanaopata huduma katika eneo husika, umbali kilipo kituo, pamoja na idadi ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, utofauti wa mgao baina ya vituo vya kutolea huduma za afya ikiwemo Hospitali ya Frelimo na Hospitali nyingine za Halmashauri hutokana na vigezo hivyo. Hospitali ya Manispaa ya Iringa Frelimo ilisajiliwa tarehe 25 Julai, 2013 kama Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa na ilianza kupokea mgao wa ruzuku ya fedha za uendeshaji kama Hospitali kuanzia Agosti, 2013 ambapo kwa mwaka huu wa fedha mpaka Machi imepokea kiasi cha shilingi 53,32.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu iliyopo katika Hospitali ya Frelimo ni pamoja na jengo la Utawala, jengo la Huduma za Wagonjwa wa Nje, jengo la huduma za Maabara, jengo la huduma za Mionzi, jengo la Ufuaji na jengo la Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto. Miundombinu inayokosekana katika Hospitali hii ni pamoja na jengo la upasuaji, Wodi za kulaza wagonjwa, jengo la kuhifadhi maiti, na jengo la kutunzia dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuongeza majengo kwenye Hospitali hii ili kuboresha huduma zinazotolewa. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa ajili ya majibu mazuri ya Serikali, lakini naamini Naibu Waziri yeye mwenyewe ameona namna ambavyo changamoto ni kubwa. Hii ni Hospitali ya Wilaya

yenye takriban wakazi 200,000 na kwa mwaka mzima wa fedha tumepewa shilingi milioni 53. Kwa hiyo, anaweza akaona ukubwa wa tatizo ulivyo na kwamba haiwezi kututosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, swali langu la nyongeza sasa: Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kutujengea vituo vingine vya Afya katika Jimbo la Iringa Mjini, hasa katika Kata za Kitwili, Igumbilo, Nduli, Isakalilo na Mkwawa ili angalau kupunguza mzigzo katika Hospitali ya Frelimo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, je, ni lini Serikali itaufanyia kazi mpango au ombi letu tulilolileta kama mkoa la kuomba sasa hospitali hizi zibadilishane maeneo; pale ilipo hospitali ya wilaya ijengwe ya mkoa na ile ya mkoa tuachiwe wilaya kutokana na eneo finyu lilitopo katika hospitali yetu ya wilaya ili kufanya utanuzi zaidi kwenye eneo la hospitali ya mkoa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Hospitali hii ya Frelimo ni hospitali ya Manispaa ya Iringa na kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu langu la msingi, hospitali hii bado ina upungufu mkubwa wa miundombinu kwa maana ya wodi kwa ajili ya kulaza wagonjwa; wodi ya wanaume, wodi ya watoto lakini pia wodi ya akinamama. Hii imepelekea pamoja na umuhimu wa hospitali hii kuhudumia wagonjwa wachache zaidi ikilinganishwa na hadhi ya hospitali yenye. Nndio maana kwa vigezo vile vya mgao wa fedha za ruzuku, inapata fedha kiasi hicho ambacho kimsingi lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba tunatenga

fedha kwa ajili ya kuongeza wodi katika hospitali ile ili ihudumie wananchi wengi zaidi na mgao wa fedha uweze kuongezeka Zaidi. Katika mwaka ujao wa fedha tumetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunajenga wodi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusiana na ombi la kujenga vituo vya afya katika kata hizi za Kitwiru, Igumbiru, Mkwawa na nyingine nilizozitaja, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi ni kujenga vituo vya afya katika kila kata na nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge amekuwa mstari wa mbele sana kuhamasisha wananchi kujitolea nguvu zao kuanza ujenzi wa vituo hivi na sisi kama Serikali tutaendelea kumuunga mkono kuhakikisha tunatenga fedha katika bajeti zijazo kuunga mkono nguvu za wananchi katika kujenga vituo vya afya katika kata hizi kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni kweli kwamba Mkoa wa Iringa umewasilisha mapendekezo kwa kufuata taratibu zote kuomba Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa iweze kubadilishana na hospitali ya rufaa ya mkoa. Sisi kama Serikali tumepokea mapendekezo hayo kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutayafanyia kazi na tathmini maombi hayo. Baada ya hapo tutatoa maamuzi ya Serikali ili kuhakikisha kwamba tunaboresha miundombinu ya huduma za afya katika Mkoa wa Iringa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa *Engineer Stella Martin Manyanya*, Mbunge wa Nyasa, sasa aulize swali lake.

Na. 193

### **Mkopo wa Injini za Boti**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

Je, kwa nini mikopo ya injini za boti isitolewe kwa mtu mmoja mmoja aliye tayari kuliko kutoa kupitia vikundi jambo ambalo linachelewesha ukuaji wa Sekta ya Uvuvu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvu, Mheshimiwa Abdallah Ulega, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa *Engineer Stella Martin Manyanya*, Mbunge wa Nyasa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 43(h) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025 inaelekeza Serikali kuhamasisha uanzishaji na uimarishaji wa Vikundi na Vyama vya Ushirika vya Msingi vya Wavuvi Wadogo kwa lengo la kuwapatia mtaji, ujuzi na vifaa pamoja na zana za uvuvi katika maeneo ya mwambao wa bahari ya Hindi, Maziwa, Mabwawa na mito ili kuongeza uzalishaji, ajira na kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza ilani hiyo, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali iliazimia kuhamasisha wavuvi na wakuzaji viumbe maji kujunga kwenye vyama vya ushirika ili kuwa na sauti ya pamoja, kufikiwa kirahisi, kutatua changamoto zinazowakabili pamoja na kuwa na usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi. Aidha, Serikali imekuwa ikiviwezesha vyama vya ushirika kwa kuvipatia elimu, zana na vifaa bora vya uvuvi kama vile injini za boti pamoja na kuvunganisha na taasisi za kifedha ili kupata mikopo yenye riba na masharti nafuu kwa lengo la kufanya shughuli zao kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Serikali itaendelea kuhamasisha na kuwezesha vyama vya ushirika. Aidha, mtu mmoja mmoja anayo fursa ya kuomba kukopeshwa injini za boti kupitia taasisi za kifedha nchini. Hivyo, natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote kuhimiza wavuvi na wakuzaji

viumbe maji wa maeneo yenu kujiunga kwenye vyama vyama ushirika vya wavuvi kama chachu ya kuwaletea maendeleo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Enginer* Stella Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, jitihada ambayo inatumika na Wizara hii katika kukamata wale wanaotumia nyavyo ambazo hazifai au katika masuala mengine yanayohusu kukusanya mapato ni kubwa sana kuliko zinazotumika katika kuwawezesha hawa wavuvi na ndiyo maana kuna wakati nilisema kwa nini wavuvi wameendelea kuwa maskini kuliko sekta nyagine. Nauliza swali hili kwa sababu Wizara yenyewe iliamua kutoa ruzuku ya injini za boti, lakini kwa kuwafanya hawa wananchi lazima wakae kwenye kikundi ni sawa na kuwafunga miguu yule mwenye ari ya kufanya kazi akimbie anamsubiri mwenzake ambaye anatakiwa mpaka achangie. Je, ni lini Serikali itaangalia upya suala hili ili kuwawezesha wavuvi hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Ziwa Nyasa lina mawimbi makubwa sana kiasi kwamba kuvulia ile mitumbwi midogo midogo ambayo haina injini inakuwa ni changamoto kubwa kwa hawa wavuvi, kiasi kwamba sasa inafikia mtu mwenye injini moja ya boti inabidi avute mitumbwi mitatu mpaka minne kwenda kilindini na kurudi, jambo ambalo ni hatari na wale wanaoenda kuvua wanazama kila wakati hata juzi kuna mvuvi amepotea. Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha, kuwezesha na kutoa mafunzo kamilifu kwa wavuvi hawa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu wa Waziri ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza uniruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Stella Manyanya kwa namna ambavyo amekuwa mstari wa mbele kuwapigania jamii ya wavuvi wa Ziwa Nyasa. Naomba nimhakikishie kwamba Serikali imejipanga vyema katika kuhakikisha wavuvi wote nchi wanapata sulhu ya changamoto zinazowakabili wakiwemo wavuvi wa Ziwa Nyasa na ndiyo maana katika wakati huu tulionao Serikali imejipanga kwenda kuhakikisha tunajenga soko la kisasa katika eneo la Mwambao wa Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni lini Serikali itaangalia upya suala la kuwezesha wavuvi mmoja mmoja. Sera yetu ya Vyama vya Ushirika ukiitazama vyema na lengo letu ni katika kuhakikisha kwamba wavuvi hawa wanakuwa na sauti ya pamoja. Ni kweli tunaweza tukawasaidia na tuko katika kuwasaidia kuhakikisha kila mmoja mwenye nia njema aweze kufikia lengo la kuwa na mashine na ikiwezekana awaajiri na wenziwe. Hata hivyo, wanapokuwa pamoja ni kwa ajili ya kuwawezesha kuwa na sauti ya pamoja kulifikia soko, ili kuwarahisishia kutokubanwa na kulaliwa na wateja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Waheshimiwa Wabunge tuliunge mkono jambo hili na sisi Serikali tumekubaliana kuhakikisha tunaongeza jitihada kwenye kupeleka mikopo kama vile ya *VICOBA*, mikopo kupitia Benki ya Kilimo na madirisha mbalimbali ya benki za kibashara ili yaweze kuwasaidia hata mvuvi mmoja mmoja ambaye atakwenda kuajiri wavuvi walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya suala la kutoa elimu; utoaji wa elimu ni jambo endelevu. Nimpe pole sana Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya* kwa ajali zinazowapata wavuvi katika eneo la Ziwa Nyasa na maeneo mengine ya wavuvi wote na sisi tumejipanga sana kupitia Chuo chetu cha *FETA* cha Utaalam wa Uvuvi kuhakikisha tunapeleka elimu ya kutosha katika maeneo yote ya wavuvi ili waweze kushindana na kuhakikisha kwamba wanakuwa tayari kuendana na hali halisi hasa za kimazingira na ili

kuondoa uwezekano kupatikana kwa hizi ajali ambazo zinawapata wavuvi wa kule Nyasa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwantumu Zodo, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na vyama vya ushirika walivonavyo wavuvi lakini bado wavuvi wetu wana hali duni sana kiuchumi katika ukanda wetu wa Pwani. Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuwakwamua wavuvi wa pembezoni mwa Bahari ya Hindi kwa Mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Lindi na Mtwara katika kushiriki kwenye uchumi wa *blue*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ya Mifugo na Uvuvi majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwantumu Zodo; kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan inao mkakati madhubuti au inayo mikakati madhubuti ya kuhakikisha inawasaidia wavuvi wa ukanda wa Pwani hasa kuendana na uchumi wa *blue* kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti tunayoitarajia ya mwaka 2021/2022, yako mambo ya msingi yatakayofanywa. La kwanza ni kuhakikisha tunaongeza uzalishaji katika miamba ya kuvutia Samaki, tutatengeneza katika Ukanda wote wa Pwani. Vile vile kama haitoshi tutahakikisha kwamba tunatengeneza vichanja vya kukaushia samaki, sababu moja kubwa inayowasumbua wavuvi ni upotevu wa mazao ambao wanayazalisha kwa kuoza na kwa kuharibika. Tunataka tuhakikishe kwamba samaki wote wanaozalishwa na wavuvi wa ukanda wa pwani hawaharibiki kwa sababu tutawaongezea thamani kwa kuwakausha, lakini vile vile tutakwenda kuongeza uzalishaji wa barafu na kuwa na *cold rooms* za kutosha katika ukanda

mzima wa pwani, ili kuweza kuitumia vyema uchumi wa *blue* na kuongeza kipato cha mvuvi mmoja mmoja na hatimaye kuongeza kipato cha Serikali yetu. Naomba wavuvi watuunge mkono ili kuweza kufikia lengo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nawaona mmesimama, lakini sasa nadhani majibu yametolewa kwa kirefu kabisa, kila mtu atakuwa amepata majibu ya eneo lake.

Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 194

**Eneo Lilitengwa na Bandari kwa Mwekezaji-Mtwara**

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza:-

Je, ni kwa kiasi gani eneo la EPZ lilitengwa na Mamlaka ya Bandari Mkoani Mtwara kwa ajili ya uwekezaji limetumika kwa shughuli iliyokusudiwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ujenzi wa Bandari Huru ya Mtwara (Mtwara *Free Port Zone*) unahusu ujenzi wa sehemu maalum ya Bandari yenye gati na sehemu ya ugavi kwa ajili ya kuhudumia Sekta za Mafuta na Gesi. Madhumuni ya kuanzishwa kwa Eneo la Uwekezaji katika eneo la Bandari Huru ya Mtwara ilitokana na hitaji la makampuni yanayotoa huduma kwa Makampuni yanayofanya shughuli za utafutaji wa Gesi na Mafuta katika mwambao mwa Pwani ya Nchi za

Tanzania, Kenya na Msumbiji ambayo yalikuwa yanahitaji kuwa na kituo cha ugavi (*supply base*) karibu na Bandari ya Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Eneo la Mradi wa Uwekezaji lenye ukubwa wa jumla ya hekta 110 katika Bandari Huru ya Mtwara (Mtwara Free Port Zone) linaendelezwa kwa awamu. Katika awamu ya kwanza, eneo la ukubwa wa hekta 10 limeendelezwa kwa asilimia mia moja kama ilivyopangwa. Shughuli za utekelezaji wa mradi huo zimehusisha ujenzi wa miundombinu wezeshi ya ndani na nje (*offsite and onsite infrastructure*) ikiwemo barabara kwa kiwango cha lami, umeme na mfumo wa usambazaji wa majisafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uendelezaji wa miundombinu katika eneo hilo kukamilika kwa asilimia mia moja (100%), kwa sasa shughuli za uwekezaji katika eneo hilo zinaendelea vema na makampuni matatu (3) yanafanya shughuli hizo za uwekezaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anastazia Wambura, swali la nyongeza.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; kama tulivyosikia majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba ni hekta 10 tu ndizo zimeendelezwa kwa asilimia 100 na wakati hekta zilizotengwa zaidi ya miaka 10 ni hekta 110. Kwa hiyo inashangaza sana kuona kwamba uendelezaji unasuasua sana. Napenda kujua, ni lini sasa hekta zote 110 zitaendelezwa ili kusudi wapatikane wawekezaji wengi Zaidi kwa sababu mpaka sasa ni wawekezaji watatu tu ndiyo wamepatikana? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; nataka kujua kama Serikali sasa itakuwa tayari kutoa sehemu ya eneo kwa ajili ya wajasiriamali wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili waweze kufuga kuku katika *large scale* kwa ajili ya *ku-export* nchi Jirani? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Wambura.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza dhamira ya Serikali bado haijabadilika kwa hiyo ku-*offload* hilo eneo kwa ajili ya matumizi mengine, mahitaji ya namna hiyo yakinke na ikionekana malengo ya awali yaliyokuwa yametengwa eneo hilo lote kwa ajili ya uwekezaji wa *Oil and gas* yamekuwa *absolute* kwamba haliwezi kufanyika *then* Serikali inaweza kutazama. Mpaka sasa Serikali bado inaamini kwamba kuna umuhimu wa kulihifadhi eneo hilo, kwaajili ya kuendelea kufanya *expansion* kwa awamu kutokana na mahitaji kama ilivyo sasa hivi. Kwa hiyo suala la kuligawa hilo eneo kwa matumizi mengine hilo bado halina nafasi kwa kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu lini litaendelezwa lote; kama sote tunavyofahamu kwamba kuna wakati wa biashara ya *gas* na *oil* duniani ina-*boom* na kuna wakati imeshuka. Sasa hivi kama mtaona kwamba malengo yalikuwa ni kufanya uwekezaji kwa ajili ya kuhudumia uwekezaji wa *oil and gas* katika nchi yetu ya Tanzania, lakini kwa ajili ya nchi ya Msumbiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu kwenye ulimwengu namna gani ambavyo *explorations* ya *gas* ilivyoshuka na namna ambavyo uwekezaji uliokua ufanyike Msumbiji na wenyewe ume-*delays* sasa hivi. Kwa hiyo naamini kwamba Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Mtwara, mahitaji ya eneo hilo kwa ajili ya uwekezaji mkubwa kwa ajili ya *gas* na mafuta bado unahitajika duniani. Kwa hiyo tuta-*expand* matumizi ya eneo hilo kutokana na *demand* na kama kuna wawekezaji wako tayari maeneo ya Mtwara na wameshawa-*approach* Wabunge ama wananchi wa Mkoa wa Mtwara wanakaribishwa Wizara ya Viwanda na Biashara ili tuweze kujadili pamoja namna ya kulitanua hilo eneo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa twende Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlagila, Mbunge wa Kyela, sasa aulize swali lake.

Na. 195

### **Kuanzisha Kilimo cha Umwagiliaji Kyela**

**MHE. ALLY A. MLAGHILA** aliuliza:

Je, ni lini Serikali itaanzisha kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia Mto Songwe, Kiwira, Mbaka na Lufilyo ili kuongeza uzalishaji wa mpunga na kukuza uchumi wa nchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, majibu.

### **NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Anyigulile Mlaghila, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji pamoja na fursa zilizopo katika Bonde la Mto Songwe pamoja na mabonde ya Mito Kiwira, Mbaka na Lufilyo, Serikali ilitekeleza miradi mbalimbali katika mabonde hayo. Katika Wilaya ya Kyela, kupitia Mpango wa Kilimo awamu ya kwanza (*ASDP I*), Serikali ilijenga Maghala mawili ya kuhifadhiya mpunga katika skimu za Makwale na Ngana. Aidha, wakulima walipata mafunzo ya uendeshaji wa skimu, kilimo chenye tija na masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imekamilisha ujenzi wa Skimu ya Mbaka iliyogharimu Sh.358,877,336.48. Kazi zilizotekelizwa ni pamoja na Uchimbaji wa mfereji mkuu mita 1,900; Ujenzi wa tuta la bwawa (*formation of embankment*) urefu wa mita 450 na usakafiaji wa mfereji mkuu kwa zenge mita 1,355.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina Mpango wa kuendeleza hekta 3,005 za umwagiliaji katika Bonde la Mto Songwe kwa ubia baina ya Serikali ya Tanzania na Malawi chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bonde la Mto Songwe. Aidha, Serikali itaendelea na juhudzi za kutafuta fedha ili kuendelea na uendelezaji wa mabonde hayo pamoja na mabonde mengine nchini kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila swalii la nyongeza.

**MHE. ALLY A. JUMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijauliza naomba unipe nafasi pia nikushukuru wewe na Bunge hili tukufu kwa niaba ya Wananchi wa Kyela, pia Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuhakikisha kwamba baadhi ya wananchi wanapata msaada hasa wale walioathirika na mafuriko. Naomba niseme ahsante sana kwa Mama yetu Rais wetu ambaye ndiyo anayeongoza nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza ni kama ifuatavyo; nikweli kuna *Scheme* ambazo zimetajwa za Ngana na Makwale, hizi skimu zimechukuwa tumito tudogo na tuchache sana ambayo tuna maji machache.

Sasa naomba niulize Serikali je, wanampango gani wa kutumia Mito ya Mbaka, Rufirio na Kiwila, mbali na Songwe ambayo ina maji mengi na ya msimu wote ili kujenga mabwawa makubwa kama ilivyofanyika utafiti na JICA miaka 1969 mpaka 1970 ili pia tupunguze mafuriko?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, Kyela tunaelekeea kupata mwekezaji mzuri ambaye yuko tayari kuendeleza zaidi ya hekari elfu 10 akishirikiana na wananchi, lakini pia yuko tayari kujenga kiwanda kikubwa ambacho *kita-process* mpunga. Je, Serikali itakuwa tayari kushirikiana na mwekezaji huyo na sisi kwa Pamoja? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hili la mwekezaji, wala halihitaji majadiliano mafuru, kama mwekezaji yupo na *serious investors* karibu Wizara ya Kilimo tukaenaye, tujadiliane naye tuone anahitaji msaada gani ili tuweze kusaidiana kuweza kufikia adhima ya kuwekeza na haya ni maelekezo ya Serikali wala hatutomsumbuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mito miwili aliyoitaja nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge; mfano maeneo yete yaliyokubwa na mafuriko sasa hivi kwa maana kuanzia Mkoa wa Kilimanjaro na maeneo ya Kyela kwa maana ya Mkoa wa Mbeya na maeneo mengine, wataalamu wetu wa Wizara ya Kilimo wapo sasa hivi wameshakwenda kwa ajili ya kufanya tathimini na ingawa kuna *stand* ya JICA na zipo *stand* zingine ambazo zilifanywa katika baadhi ya maeneo kwenye nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi wataalamu wa Wizara ya Kilimo wa Tume ya Umwagiliaji wana *review stand* zote zilizofanywa zamani ili kuangalia namna gani tunaweza kuziboresha na kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wengine wote kwamba maeneo yote *potation* yatafanyiwa kazi katika kipindi cha miaka hii mitano Inshallah!

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Nishati Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, Mbunge wa Jang'ombe sasa aulize swali lake.

Na. 196

### **Bei ya Umeme Zanzibar**

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro wa bei ya umeme unaotumika na Watanzania waishio Zanzibar ili kuweka usawa kwa Watanzania wote?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa wa Nishati naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, Mbunge wa Jang'ombe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeendelea kushughulikia suala la bei ya kuuza na kununua umeme baina ya Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*) na Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO*) ili kuupatia ufumbuzi mgogoro huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Timu ya Wataalamu wa Taasisi husika zilikutana katika vikao mbalimbali na kufanya uchambuzi wa kina wa vigezo vilivyoohusika katika kupanga bei hiyo ya kuuzia umeme kwa wateja wakubwa wa kununua umeme ikiwemo *ZECO*. Kutokana na uchambuzi huo, inapendekezwa kuwa vigezo hivyo vipitiwe upya ili kuleta unafuu kwa wateja wa aina hiyo ikiwemo *ZECO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo hayo yaliwasilishwa katika Kamati ya Wizara zinazoshughulikia masuala ya Muungano ili kufanya kazi mapendekezo hayo na kupata ufumbuzi wa kudumu wa suala hili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, swalii la nyongeza.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali nami niseme msemo mmoja *vafil-bidhi ilal baras*, wenye weupe ukisuguwa utatia doa, kwenye jawabu nzuri kama hili na ninaishukuru sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi katika kuliona hili na wachache katika watu wanaofanyiwa

mema wakashukuru miongoni mwao na mimi mja wake Mungu Mheshimiwa Ali King.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe tu Serikali juu ya haya mapendekezo na huko yalikopelekwa labda waseme neno.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ali Hassan King kwa sababu neno la Serikali ni hilo lilokuja kwa mahandishi hapo na tunashukuru kwa hizo pongezi kwa Serikali. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mbunge wa Sumve sasa aulize swali lake.

Na. 197

**Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba Kuunganishwa na Makao Makuu ya Mkoa wa Mwanza**

**MHE. KASALALI E. MAGENI** aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya kutoka Magu – Bukwimba hadi Ngudu itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami ili kuu nganisha Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba na Makao Makuu ya Mkoa wa Mwanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer Godfrey Kasekenya Msongwe* majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ninapenda kujibu Swali la Mheshimiwa Emmanuel Mageni Kasalali, Mbunge wa Sumve ,kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya kutoka Magu – Bukwimba hadi Ngudu ni sehemu ya barabara ya Mkoa

yenye urefu wa kilomita 71 inayoanzia Magu – Bukwimba – Ngudu hadi Hungumalwa. Barabara hii nikiunganisha muhimu kati ya Wilaya ya Magu na Kwigumba kupitia Isandula (Magu) – Bukwimba – Ngudu – Nyamilama hadi Hungumalwa.

Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) imekamilisha kazi ya Upembuzi yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Magu – Bukwimba – Ngudu hadi Hungumalwa kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilometra 71. Kazi hii ilifanywa na Mhandisi *Mshauri M/s Advanced Engineering Solution* kwa ghamra ya shilingi milioni 638.486 na kukamilika mwaka 2019. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha za kugharamia ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ujenzi kwa kiwango cha lami ukisubiri upatikanaji wa fedha, Wizara yangu kupitia *TANROADS* inaendelea kuihudumia barabara hiyo ili iweze kupitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya Shilingi milioni 475.551 zilitengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara hii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, swali la nyongeza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuwa barabara hii ni ya muhimu sana kwenye uchumi wa nchi yetu na uchumi wa Kanda wa Ziwa, kwasababu inapunguza umbali wa kutoa Shinyanga mpaka Mkoa wa Mara kuelekea nchi jirani ya Kenya, kwa zaidi ya kilometra 73 na Serikali imekuwa ikiahidi ujenzi wa barabara hii katika Awamu kuanzi ya Tatu mpaka Awamu ya sasa na Wananchi wa Wilaya ya Kwigumba wanahitaji kuunganishwa na Makao Makuu yao mkoa wao kwa barabara ya kiwango cha lami.

Je, ni lini sasa Serikali itaachana na maneno ya kutafuta pesa na kuanza kujengwa barabara hii kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, barabara inayoanza Fulo kuitia Nyambiti mpaka Malia yenyeye urefu wa kilometra 73 pia ni barabara muhimu sana kwenye uchumi wa Wilaya ya Ksimba na barabara hii imeahidiwa kwenye ukurasa wa 77 wa ilani ya Chama cha Mapinduzi kuanza kufanyiwa upembuzi yakinifu na hatimaye kujengwa kwa kiwango cha lami. Je, ni lini sasa Serikali itaanza kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Msongwe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Awamu ya Tano iliyopita taratibu za ujenzi kwa kiwango cha lami umeanza na ndiyo maana tumekamilisha usanifu wa kina mwaka 2019 kwa hiyo si tu zimekuwa ni ahadi lakini tayari tumeshaanza utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Sumve kwamba barabara alioitaja ya Fulo Nyambiti Malia ameisema mwenyewe kuwa imemeanishwa kwenye ilani ya Chama cha Mapinduzi na nimuhakikishie katika kipindi hiki cha Awamu ya Sita kama tulivyosema imemeanishwa kwenye ilani, lakini pia imeongelewa na Mheshimiwa Rais wakati analihutubia Bunge hapa ni kati ya barabara ambazo zitafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mbunge na Wananchi wa Sumve kwamba tutatekeleza kama tulivyopanga ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga swalii la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa swalii la nyongeza kwa kuwa barabara ya kutoka Kalenga kwenda Ruaha *National Park* ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa hili hasa unaotokana na utalii na kwa kuwa upembuzi yakinifu na usanifu ulishafanyika siku nyingi. Na kwa kuwa pia Serikali imeweka kwenye ilani tangu Awamu ya Nne mpaka sasa na

imekuwa ikitenga fedha kidogo kidogo. Je, kwa nini sasa Serikali isianze kujenga kidogo kidogo kutokana na hizo pesa wanazotenga maana imekuwa ahadi ya muda mrefu? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Kiswaga Mbunge wa Kalenga asubiri bajeti tutakayo pitisha nina hakikika ni kati ya barabara kama endapo bajeti itapita itakuwa ni kati ya barabara ambazo zitatekelezwa kuanzia bajeti tunayoiendea. Kwa hiyo, naomba awe na subira na asubiri tutakapo anza kupitia bajeti ya Ujenzi na Uchukuzi.

**NAIBU SPIKA:** tunaendelea na swali la Mheshimiwa Mohamed Lujua Monni Mbunge wa Chemba.

Na. 198

#### **Barabara ya Handeni – Kiteto – Chemba hadi Singida**

**MHE. MOHAMED L. MONNI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Handeni- Kiberashi-Kiteto – Mrijo – Chemba – Kwa mtoro hadi Singida kwa kiwango cha lami kwa kuwa ipo kwenye llani na pia Ahadi ya Mheshimiwa Rais?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Mwita Mwita Mwikwabe Waitara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa

Mohamed Lujua Monni, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Handeni – Kiberashi – Kwa mtoro – Singida ni barabara ya mkoa yenye urefu wa kilometra 461. Kati ya urefu huo, kilometra 111 zipo Mkoa wa Manyara, kilometra 171 Mkoa wa Dodoma na kilometra 47.1 Mkoa wa Singida. Barabara hii nikiunganisha muhimu cha Mikoa ya Singida, Manyara, Dodoma na Kanda ya Pwani hasa bandari ya Tanga na Dar es salaam. Kukamilika kwa barabara hii kutapunguza idadi ya magari ya nayopita katika barabara kuu ya kati *Central Corridor* kuelekea Kanda ya Kati na Kanda ya ziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*), imekamilisha Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara hii. Kwa sasa Serikali ipo katika maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii. Katika Mwaka wa Fedha 2021 jumla ya Shilingi bilioni 6 zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Aidha, katika mapendeleko ya bajeti ya mwaka 2021/22 barabara hii itazingatiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Lujua Monni swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali hili limeulizwa mara mbili kwa mujibu wa Taarifa mbalimbali kutoka Bunge lako majibu yamekua ya kitolewa hayo hayo, sasa naomba kujua hata hizo bilioni 6 ambazo zimetengwa kwa ajili ya mwaka unaoishia mwenzi mmoja ujao hazijawahi kutumika mpaka leo. Naomba kujua lini sasa hizi bilioni 6 sasa zinaanza kufanya ujenzi kwenye barabara ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni nini *commitment* ya Serikali kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwasababu Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye ziara ya kuomba kura aliahidi itajengwa kwa kiwango cha lami, naomba kujua...

**NAIBU SPIKA:** umeshauliza Mheshimiwa, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumshukuru Mbunge kwa jinsi ambavyo ifuatilia barabara hii barabara ndefu na kweli ni kiunganishi cha mikoa tangu Singida hadi Tanga na imepangiwa katika bajeti bilioni 6.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumuahidi Mbunge huyu kwamba kabla ya bajeti hii kwisha barabara hii itatangazwa katika kipande ambacho kimepangiwa kilomita 20. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Miraji Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana barabara hii tuna maslahi nayo kama alivyojibu swali Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa sababu barabara hii inaunganisha mikoa minne na barabara hii inahistoria katika nchi yetu imefika wakati sasa Serikali iamuwe kujenga barabara hii kilometra 461 iishe kuliko kuanza kuwa na vipande vidogo vidogo.

Ni lini Serikali itajenga barabara yote? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi wa Uchukuzi majibu.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ina Wabunge wengi ambaao wanaifuatilia sana na ninawashukuru sana kwa kuweza kuwa wanatukumbusha kila mara umuhimu wa barabara hii. Lakini kama alivyojema Mbunge barabara hii inaurefu wa kilometra 460 na tunaendelea kujenga kwa vipande kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu unaoendelea kama nilivyosema katika swali lilipita tutajenga kipande kimoja na katika bajeti hii ambayo tuna ijadili mwaka huu barabara hiyo vilevile imezingatiwa kwa hiyo napenda kuwaahidi wananchi tangu mikoa ya Singida hadi Tanga ambayo barabara hiyo inapita kwamba vipande vinaendelea kujengwa na barabara hiyo tutaizingatia kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tumalizie Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Ally Yahya Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, sasa aulize swali lake.

Na. 199

**Mkakati wa Kumaliza Changamoto za Mawasiliano  
ya Simu – Nanyumbu**

**MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza:-

Je, ni lini changamoto ya mawasiliano ya simu Wilayani Nanyumbu itamalizika katika Kata za Likokona, Mkonona, Nangomba, Nandete, Napacho, Lumesure, Michiga na Chipuputa?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Eng. Andrea Mathew Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA  
HABARI** aliibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Ally Mhata, Mbunge wa Nanyumbu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ina jukumu la kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo yote ya vijijini na mijini yasiyo na mvuto wa kibashara. Mpaka sasa kuitia tumeshafikisha

miradi 1,057 ambapo miradi 686 imeshakamilika na miradi 371 inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizo za Serikali bado kuna maeneo mengi yakiwemo maeneo ya Jimbo la Nanyumbu ambayo hayana huduma ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuititia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, umevifanya tathmini vijiji vya Kata ya Likokona, Mkonona, Nangomba, Nandete, Napacho, Lumesure, Michiga na Chipuputa katika Jimbo la Nanyumbu. Vijiji vya Kata hizi vimeingizwa katika Mradi wa Mpakanini Kanda Maalum awamu ya sita ambapo zabuni tarajiwa kutangazwa kabla ya kwisha kwa mwaka wa fedha 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vya Jimbo la Nanyumbu vilivyoingizwa katika zabuni hiyo inayotarajiwa kutangazwa ni kama ifuatavyo:-

1. Kata ya Likokona Vijiji vya Misawaji, Namaka, Msinyasi, na Likokona;
2. Kata ya Mkonona Vijiji vya Nambundu, Waniku and Namaromba;
3. Kata ya Nandete Vijiji vya Chivikikiti na Nakole;
4. Kata ya Lumesure Kijiji cha Lumesure;
5. Kata ya Michiga Kijiji cha Makong'ondera; na
6. Kata ya Chipuputa Vijiji vya Mpwachia, Nakatete na Ngalinje.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Vijiji vya Kata za Nangomba na Napacho vitaingizwa kwenye awamu nyingine ya miradi ya kufikishiwa huduma za mawasiliano kadri bajeti itakavyokuwa inaruhusu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba tufanye masahisho katika majina ya vijiji. Kata ya Mkonona ni Nambunda siyo Nambundu na siyo Waniku.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya masahisho hayo, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa dhumuni la uanzishaji Mfuko huu pamoja na madhumuni mengine ni kuziwezesha vile vijiji vya mpakani kuweza kupata mawasiliano ya simu hasa kuhakikisha ulinzi na usalama wa nchi yetu unakuwepo. Mfuko huu ulianzishwa mwaka 2007, vijiji vile bado vina matatizo makubwa ya mawasiliano. Hivi ninavyoongea hatuna mawasiliano ya simu ya *Airtel* wala mitandao mingine. Je, wakati mchakato huu wa kutangaza tenda unaandaliwa ni hatua gani za dharura zinachukuliwa hili kuhakikisha vijiji vile vinapata mawasiliano hasa kwa kipindi hiki kigumu ambacho usalama wetu na nchi ya Msumbiji ni mbaya? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, tatizo hili la mawasiliano linakwenda sambamba na usikuvi wa redio yetu ya *TBC*. Katika Wilaya yangu hatuna kabisa mawasiliano ya *TBC*. Je, ni hatua gani za dharura Mfuko huu unaweza kuisadia *TBC* ikasikika ndani ya Jimbo langu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Eng. Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la

nyongeza la Mheshimiwa Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuonyesha ukaribu na Wizara yetu kwa kuhakikisha kwamba anatupatia taarifa sahihi ili na sisi tuweze kuzifanyia kazi kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ameongelea vijiji ambavyo viko mipakani, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote tayari imeshafanya utafiti na tathmini ya vijiji vyote Tanzania nzima siyo Nanyumbu peke yake ambapo maeneo yote ya mipakani tunatarajia kuutangaza tenda kwa ajili ya ujenzi na kuhakikisha kwamba tunalinda mipaka yetu yote. Mipaka ya Mtwara, Namanga, Sirari pamoja na maeneo mengine Serikali tunafahamu kabisa kwamba mawasiliano ni jukumu letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nilisema katika jibu la msingi maeneo haya ni yale ambayo mara nyingine hayana mvuto wa kibishara. Ndio maana kupitia Mfuko huu kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema ulianzishwa mwaka 2007 kazi yake mahsus ni kuhakikisha tunafikisha mawasiliano katika maeneo ambayo watoa huduma wengine hawawezi kufikisha mawasiliano, hilo ni jukumu la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Sasa hivi *Ku-migrate* kutoka *4G* kwenda *5G service providers* wengi duniani wamegundulika wanatumia *multivendor* badala ya kutumia *system* ambayo imewekwa. *Multivendor* inaongeza *risk* ya *complicity* ya *5G*. Wanafanya hivyo kupunguza ghamama zao na mteja anapoingia kwenye *5G* anataka apate *speed* anayolipia. *5G* inaweza ika-

*download* kitabu cha kurasa 1,000 for 3 to 5 seconds. Serikali imejiandaa vipi ili *risk* hii ya *complicityya* 5Gisitokee Tanzania kama ilivyoanza kutoa kwenye nchi nyingine?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, teknolojia ya 5G na 4G vyote hivi vinaendana na uwekezaji. Tunaposema uwekezaji wa 3G, 4G na 5G kwanza lazima Serikali ijiridhishe watoa huduma waliopo wanapotumia hizi *spectrum* ambazo tumewapitia kwa ajili ya 3G na 4G wameweza ku-deploy vizuri kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoondoka kutoka teknolojia moja kwenda teknolojia nyingine pia inaathari ya moja kwa moja kwa watumiaji wa huduma hii. Kwa hiyo, ni lazima sasa tutengeneze mazingira ili pindi tutakoporuhusu sasa *spectrum* ya 5G kutumika basi watoa huduma pamoja na watumiaji wa huduma hii wawe tayari kwa ajili ya mabadiliko hayo. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali na majibu, sasa nilete matangazo tuliyonayo asubuhi hii kabla hatujaendelea na ratiba yetu. Kwanza ni matangazo ya wageni walioko hapa Bungeni na tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge.

Tutaanza na wageni wawili wa Mheshimiwa Mwanaidi Khamis ambaye ni Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambao ni mama yake mzazi Ndugu Rukia Suleiman na mdogo wake Ndugu Mwantum Khamis kutoka Zanzibar, karibuni sana. (*Makof!*)

Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi amba ni Watendaji wa Halmashauri ya Msalala, Mkoani Shinyanga wakiongozwa na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo Ndugu Saimon Berege, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana amba ni ndugu zake Maria Kijazi na Consolata Hilary kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo kutoka Jijini Arusha, amba ni Katibu Mwenezi wa CCM, Wilaya ya Arumeru Ndugu Joshua Hungura na Mtendaji Kata ya Bwawani Ndugu Saimon Kaaya, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Jeremiah Amsabi amba ni Madiwani wastaa fu kutoka Jimbo la Serengeti, Mkoani Mara na hawa ni Ndugu Pasto Maiso na Ndugu John Mahemba, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni saba wa Mheshimiwa Masache Kasaka amba ni Viongozi wa Vyama vya Ushirika yaani *AMCOS* wanaolima tumbaku kutoka Wilayani Chunya, Mkoani Mbeya wakiongozwa na Ndugu Yohana Chawene, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava amba ni wanamaombi kutoka Turiani, Mkoani Morogoro na Mkoani Geita wakiongozwa na Ndugu Elizabeth Uri, karibuni sana. (*Makofi*)

Wahesimiwa Wabunge, lipo pia tangazo la kikao kutoka kwa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, anawatangazia wajumbe wote wa Kamati hii kwamba siku ya leo tarehe 5 Mei, 2021 kutakuwa na kikao cha Kamati kitakachofanyika katika ukumbi Na.231, ghorofa ya pili, jengo la Utawala kuanzia saa saba mchana. Kwa hiyo, baada ya kuahirisha shughuli za Bunge hapa

wajumbe wa Kamati hii mnaombwa mkahudhurie kikao hicho.

Lipo pia tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba siku ya kesho Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anakusudia kutayarisha futari kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge. Kwa sababu hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnaombwa siku ya kesho mtakapokuja asubuhi msiegeshe magari lile eneo la maegesho ya magari kwa sababu futari itaandaliwa hapo. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika anawakaribisha sana Wabunge na watumishi wote wa Bunge kwa ajili ya *Iftar* hiyo ambayo ni ya muhimu kuhudhuria maana Mheshimiwa Spika ye ye mwenyewe atakuwepo. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu.

#### **NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:**

#### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 - WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea, kwa muda wetu tulionao leo kwa ajili ya uchangiaji na majina niliyoletewa hapa mbele ni dhahiri hatutaweza kuchangia dakika kumi kila mmoja. Kwa hivyo, tutakuwa tukichangia kila mmoja dakika saba.

Tutaanza na Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini atafuatiwa na Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota ajiandae.

**MHE. JUMANNE A. SAGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia kwenye sekta ya elimu. Nami niungane na Wabunge waliozungumza tangu jana kupongeza juhudzi za Wizara ya Elimu katika kuimarisha na kuboresha elimu kwa ajili ya vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwapongeze ushirikiano unaoimariswa kati yao na TAMISEMI maana Wizara ya Elimu imebaki na sera, TAMISEMI imebaki na utekelezaji lakini tunaona jinsi wanavyoendelea kushirikiana. Wizara inatafuta resources inazipeleka TAMISEMI na TAMISEMI wanatekeleza miradi. Wizara inabuni maandiko yanakwenda kutelezwa na TAMISEMI kwa maslahi ya maendeleo ya nchi yetu. Hata huu Mpango wa Elimu bila Malipo najua uliandaliwa na Wizara ya Elimu na ikatoa miongozo na TAMISEMI ikaingia kwenye utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda nitajikita kwenye maeneo machache. Bahati nzuri mimi ni mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii lakini ukiisikiliza jamii yote imekuwa ikizungumza juu ya kutoridhishwa na mwenendo wa elimu kwa ajili ya maendeleo ya vijana wetu. Wakati mwingine tusipokuwa waangalifu tunaweza tukajikuta lawama hizi zinaelekezwa kwa Waziri na Waziri na wataalam wake wakaona kama ni watuhumiwa wa kushusha elimu yetu. Mimi naomba niwashauri kwamba viongozi wa Wizara na wataalam walioko Wizarani ni wawakilishi wetu tu katika kusimamia sekta ya elimu. Hivyo, ni vema watusikilize sisi wawakilishi wa wananchi na wadau wengine wanapozungumza mambo haya *then* wapange mikakati ya utekelezaji na uboreshaji kwa kuwahusisha wadau hawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo, naungana na wasemaje wote waliopita wanaosema elimu yetu ina changamoto. Sote tuna watoto na tunaona wakitoka vyuoni au shulenii hali zao huwaje. Wakati fulani nikiwa mmoja wa watendaji wa Serikali wataalam wanapoandika hata ile ku-*draft* barua Mtendaji Mkuu unakuwa na kazi ya ziada kurekebisha barua ile. Hii zote ni

*indicators* kwamba uwezo wa vijana wetu ni changamoto kubwa. Kwa hiyo, ni vizuri tukishauriwa kwamba pana changamoto tuisikie na tuone namna ya kui-*address*. Kama mtu anamaliza chuo kikuu hawezি kuandika barua nzuri ya kuomba kazi inayoshawishi lazima tujue kwamba kwenye elimu yetu lipo tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo, naomba nijikite kwenye Jimbo la Butiama, nimkumbushe Waziri, najua nililisema hili kwenye Kamati na nikajibwa lakini nina maoni kwamba ni vizuri tukasikiliza na tuone namna ya kutanzua. Katika dhamira ya kumuenzi Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Baba wa Taifa Ietu, Serikali ilikubali kuanzisha Chuo cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu (*Mwalimu Julius Nyerere University of Agriculture and Technology*) ni zaidi ya miaka kumi sasa hakijaanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, chuo hiki kipo kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi yam waka 2010-2015 lakini kiko kwenye *Five Years Development Plan I* ya mwaka 2010/2011 - 2015/2016 lakini pia kiko kwenye *Five Years Development Plan II* ya mwaka 2016/2017 - 2021/2022. Kwa kuanzia Mkoa wa Mara na Wilaya ya Butiama walifanya mambo mengi; moja ni kukubali *ku-sacrifices* iliyokuwa Shule ya Sekondari *O-Level*/na *A-Level* iitwayo Oswald Mang'ombe *High School* yenye ekari 86 yawe majengo ya kuanzia chuo kikuu hiki, lakini Butiama ilitoa ekari 573 kama eneo la kujenga *campus* kuu na eneo la Baiki.

Pia tulikubaliana kwamba viwepo vitivo kwenye Wilaya zote za Mkoa wa Mara na kule Rarya Kinesi walioa jumla ya ekari 75; Serengeti eneo la Kisangula walitoa ekari 136 na maeneo yote yalipewa hati miliki kwa jina la chuo hiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa upande wake ilitekeleza wajibu wake ambapo ni pamoja na kukubali kuanzisha mitaala 35; 26 ya shahada na 9 stashahada, miongozo na sera mbalimbali zaidi ya 25 ilitayarishwa na kuidhinishwa na mamlaka husika kwa maana Ofisi ya Rais,

Utumishi na Msajili wa Hazina. Wizara pia ilitoa wataalam 79; *academic staff* 42 lakini watumishi mwega ambao ni *administrative staff* 37.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachohuzunisha tangu watumishi hawa wapelekwe zaidi ya miaka saba iliyopita chuo hakijaanza lakini wanalipwa mishahara. Kinachotuma zaidi ni kwamba shule ile ilijengwa ili itumike lakini sasa haitumiki kwa ajili ya wanafunzi wa sekondari pia haitumiki kama chuo.

Sasa watu wa Butiama na Mkoa wa Mara wanauliza chuo hiki kitaanza lini? Anayetakiwa kusajili chuo hiki ni *TCU* ambayo iko chini ya Wizara. Wizara chini ya Mheshimiwa Prof. Ndalichako ilikubali chuo kianze na wakapeleka wataalam *including Deputy Vice Chancellors* lakini hadi leo hakuna kinachoendelea. Wananchi wanauliza hivi lengo la Serikali lilikuwa nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi wananchi wa Butiama wanataka chuo kianze kama ilivyodhamiriwa awali. Wamechoka kusubiri, wanaomba majibu ya Serikali. Kwa kweli katika mazingira haya majibu yasipokuwa ya kuridhisha najuliza hivi nitaachaje kuing'ang'ania shilingi ya Mheshimiwa Waziri wangu.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, kengele ya pili imegonga.

**MHE. JUMANNE A. SAGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja lakini naomba swalı langu hili lijibewe vizuri. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mheshimiwa Charles John Mwijage ajiandae.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru sana kwa kupata nafasi ili niweze kuchangia Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajielekeza kwenye maeneo mawili; kwenye Bodi ya Mkopo pamoja na Shule yetu pedwa ya *St. Jude* ambayo ipo pale Mkoani Arusha. Hii ni shule ambayo inasomesha watoto 1,800 bure. Wanatoa chakula bure, usafiri bure, wanalala kwenye mabweni bure na masuala mengine yote. Watoto hawachangii hata shilingi moja. Pia wanasomesha watoto 350 Chuo Kikuu kwa gharama zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, pia wameajiri watu 295. Kati yao, Watanzania ni 286 na wageni wako saba. Cha kushangaza mwaka 2020, mwezi Oktoba, *TRA* walikwenda kuifunga akaunti ya shule hiyo ambayo ipo kwenye Benki ya *NCBA* na tarehe 03, Novemba, 2020, walikwenda kuchukua fedha kiasi cha shilingi milioni 500 kutoka kwenye akaunti ya shule hiyo huku wakiwa wamewapa *assessment* ya shilingi bilioni 5.43.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unajiuliza, hii shule haifanyi biashara, wanaunga mkono juhudhi za Serikali za kusomesha bure watoto wa Kitanzania. Mazingira ya shule ni mazuri, lakini bado *TRA* wanakwenda wanawagawia *assessment* ya *5.4 billion* na wanafunga akaunti yao na wanachukua fedha kiasi cha milioni 500, fedha ambayo ingetumika kwa ajili ya chakula cha watoto, kwa ajili ya *uniform* za watoto na masuala mazima ya uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, nadhani Wizara ya Elimu, mama yangu, Mheshimiwa Prof. Ndlichako, ana kazi kubwa ya kuliangalia suala hili kwa kushirikiana na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba. Katika hili nitumie fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Elimu kwa sababu yeye alimtuma Katibu Mkuu wake akaenda kutembelea shule hii akaona changamoto hizo na wakaahidi kwamba wataongea na Wizara ya Fedha ili changamoto iondoke kwenye shule hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ushauri wangu kwenye eneo hili, kwa sababu shule hii haifanyi biashara, nina mapendekezo mawili. Pendekezo la kwanza shule hii ipate msamaha wa kodi. Pendekezo la pili, kwa sababu tumepata taarifa maana kuna wadau wanasaidia kwenye shule hii na tunaambiwa zaidi ya asilimia 92 ambaao wanasaidia shule hii wanatoka Australia na wako wageni ambaao wanafanya kazi ya kusaidia kwenye *fundraising* na wanasaidia kwenye masuala ya *marketing*, wameomba vibali vyakazi kupitia Idara ya Kazi, wamekosa. Sasa hivi wamekata rufaa kwa Waziri mwenye dhamana, mama yangu, Mheshimiwa Mhagama, mtu ambaye ni mchapakazi, ni mtu ambaye anaendana na falsafa ya Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu kwamba Mheshimiwa Mhagama atakwenda kulipa kipaumbele jambo hilli, tuwasaidie watu hawa wawilli wapate vibali vyakazi na vibali vyaukaazi ili mwisho wa siku wasaidie kutafuta fedha kwa ajili ya shule ile na watoto wa Kitanzania waweze kunufaika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la pili ni kuhusu Bodii ya Mikopo. Katika hili kwa kweli...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gambo, hebu tusaidie jambo moja; katika hiyo shule, umetaja hiyo idadi kubwa ya wanafunzi.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Ndiyo.

**NAIBU SPIKA:** Hiyo shule ina wanafunzi wanaosomeshwa bure tu au inao na wengine ambaao wanafunzi kwa kulipa fedha?

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wote pale wanafunzi wa kike 600 na pia wameanzisha na shule ya sayansi, wana masomo ya *PCB* na *PCM* ili kuunga mkono juhudii za Serikali za kupambana na changamoto ya sayansi na teknolojia. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Haya, endelea na hoja yako.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kuhusiana na Bodi ya Mkopo. Kwanza kabisa nitumie fursa hii kuipongeza sana Serikali Sikivu ya Awamu ya Sita chini ya mama yetu, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. Nampongeza pia Waziri wa Elimu kwa sababu nina imani ameshauriana na Mheshimiwa Rais na mwisho wa siku akaweza kufanya maamuzi haya yenye tija kwa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata taarifa kwanza siku ya Mei Mosi, Mheshimiwa Rais alitutangazia kwamba asilimia sita ya kulinda thamani ya fedha imeondolewa. Jana pia tumepata taarifa kuwa asilimia 10 ambayo ilikuwa imewekwa kwa wale ambao wanachelewa kulipwa kama *penalty* na yenyewe pia imeondolewa. Hayo ni mambo makubwa na kama Wabunge tumekuwa tunayapigia kelele kwa muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna changamoto moja kubwa. Tunafahamu kwamba mwaka 2016 Bunge hili lilitunga sheria, lilifanya marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo kutoka asilimia nane kwenda asilimia 15. Changamoto ambayo naiona kwenye hiyo sheria ni kwamba badala ya sheria kuanza kutumika mwaka 2016, imerudi toka watoto walivyaonza kukopeshwa hizo fedha. Matokeo yake, ukiangalia ripoti ya CAG ya mwaka 2016/2017, kwa sababu wao wanafanya *sampling*, hawakwenda kwa wahusika wote ambao wanatakiwa kulipa. Wanafunzi au wafanyakazi 4,830 wanalipwa mshahara chini ya moja ya tatu, kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria Na. 7 ya mwaka 1970 inasema ni lazima mtumishi yeoyote ambaye anafanya kazi, lazima makato yake yasizidi mbili ya tatu ya malipo au pato ghafi ambalo analipwa. Kitendo cha Wizara ya Elimu kushirikiana na Serikali yote kwa ujumla kurudi nyuma zaidi mwaka 2016 imekwenda kuwaathiri wafanyakazi wengi sana. Wapo ambao walikopa kwa sababu wanajua wao

wanakatwa asilimia nane, unavyomkata asilimia 15 maana yake ni kwamba unakwenda kuathiri kipato chake na mpango wake mzima wa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia waraka wa Serikali wa Novemba, 28, 2012, wenyewe Kumbukumbu Na. CE26/46/01/66 unaelekeza makato ya watumishi yasizidi mbili ya tatu ya mishahara yao ghafi. Kitendo cha Serikali kwenda kuwakata watumishi zaidi ya mwaka ambao sheria imetungwa, kwanza ni kukiuka sheria na kutumia mabavu, kitu ambacho tunadhani siyo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Rais wetu ni mtu msikivu, ni imani yangu jambo hili litakwenda kupewa kipaumbele na pendekezo langu kwenye jambo hili ni kwamba asilimia 15 ianze kukatwa kuanzia mwaka 2016 na isirudi nyuma illi kuwapa ahueni wafanyakazi wetu. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles John Mwijage na Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, ajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyopo Mezani. Niungane na wenzangu waliopita kuchangia kuwapongeza viongozi wa Wizara hii tukianza na Waziri wa Elimu, mwalimu wangu, Mheshimiwa Profesa Ndalichako; Naibu wake, Mheshimiwa QSOmari Kipanga; na Katibu Mkuu, kaka yangu, Dkt. Akwilapo; na wasaidizi wake kwa jinsi wanavyochapa kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia hotuba hii unajua kabisa imeandaliwa na walimu, ina maelezo machache na takwimu nyingi na inajieleza wazi nini kimefanywa ndani ya mwaka mmoja na miaka mitano iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile hotuba hii imekuja na majibu ya kilio cha Watanzania kuhusu sekta ya elimu.

Ukisoma ukurasa wa 69 utakuta dhamira ya Wizara kwamba sasa inakusudia kufanya mapitio makubwa, siyo mtaala tu, wataanza kupitia Sera ya Elimu ya Mwaka 2014. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu, tusianze kudai mtaala, tuanze na mabadiliko ya sera. Tukibadilisha sera na vitu vingine vitabadiili. Kwa hiyo, hongereni sana Wizara ya Elimu, mmesema mtabadilisha sera, mnapitia Sera ya Elimu ya 2014 lakini siyo hivyo tu, mtapitia na Sheria yetu ya Elimu, ile Sheria Na. 25 ya Mwaka 1978 pamoja na mabadiliko ambayo yamefanywa. Hapo kwa kweli mnakuja vizuri, kwa sababu lazima tufanye mabadiliko ya jumla na siyo vipande vipande.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda wa miaka mitano tumeona Wizara hii ikifanya kazi kubwa ya ukarabati katika miundombinu ya shule. Mkoani Mtware tumeshuhudia, siyo ukarabati wa Chuo cha Elimu Kitangali, ni ujenzi mpya kwa sababu majengo yote yamewekwa chini na tukaanza na ujenzi mpya, hongereni sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia maeneo matatu. Sehemu ya kwanza, pamoja na mambo mazuri ambayo yamefanywa, nami nitilie mkazo kwenye mabadiliko haya ya mtaala. Ni kweli kwamba sasa hivi kilio kikubwa cha wanajamii ni kwamba wahitimu katika mfumo wetu wa elimu wanashindwa kukidhi haja ya mahitaji ya kule wanakokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sasa hii dhamira ya mabadiliko ya mtaala yafanye kiukweli kwa sababu hayo ndiyo mahitaji ya sasa. Ukiangalia sababu za kubadilika kwa mitaala, mojawapo ni mahitaji ya kwenye jamii, ambayo ni haya yanayojitokeza sasa hivi. Kwa hiyo, tufanye mabadiliko ya kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wakati shughuli hii itakapofanyika basi tuwe na ushirikishaji mkubwa wa makundi yote. Tuanze kuwashirikisha wanajamii, tushirikishe walimu kama watekelezaji wa mtaala, wanafunzi wenyewe

washirikishwe, siyo hivyo tu, na taasisi mbalimbali ambazo zinahusika na masuala ya elimu, nao washirikishwe. Hili suala la mabadiliko ya mtaala lisiwe suala la watu wa Wizara ya Elimu tu, iwe ni jamii kwa upana wake na taasisi mbalimbali. Siyo hivyo tu, na wadau mbalimbali ambao wanahusika kwenye sekta ya elimu nao washirikishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukishabadilisha mtaala, siyo kwamba tumefanikiwa, kuna kazi kubwa sana inhabidi ifanyike. Tuna kawaida ya kubadiilisha mtaala bila kuangalia tunakwendaje katika kuutekeleza huo mtaala. Kwa hiyo, tukishabadilisha ule mtaala mpya tuandae mazingira ya vyuo vyetu na shule zetu kutekeleza mtaala mpya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanafunzi au mwanachuo akishaenda kwenye hivyo vyuo vyetu, akute kuna *facilities* za kutosha kujifunza maarifa mapya ambayo yapo kwenye mtaala mpya. Tukiacha hata shule au taasisi zetu kama ilivyo, tutakuwa na mtaala mpya ambao utashindwa kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tunahitaji maandalizi makubwa ya walimu na wakufunzi wetu ili waweze kutekeleza mtaala mpya, kwa sababu hawa ndio watakaokwenda kuutekeleza mtaala. Wasipoandaliwa, kuna kawaida ya kufanya mabadiliko ya mtaala tukaishia kwenye watu wa Wizara au kazi ya kanda tu, tufike mpaka kwa mwalimu wa darasa naye ashirikishwe aweze kutekeleza mtaala mpya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie mchango wangu wa pili kuhusu muundo mpya wa Wizara ya Elimu, hususan nafasi ya Kamishna wa Elimu. Ukitosha Sera ya Elimu na Sheria ya Elimu, Kamishna wa Elimu ana majukumu mazito sana, lakini kwa muundo wa Wizara ya Elimu uliopo, kamishna unampa kusimamia maeneo mawili tu; Elimu ya Msingi kwa maana ya *primary* na *secondary* na elimu maalum. Kamishna wa Elimu hagusi elimu ya juu na elimu ya ufundi. Hapa kuna changamoto. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamishna wa Ardhi anasimamia ardhi yote, hasimamii ardhi ya mjini tu na kuacha vijijini; na Kamishna wa Kodi anasimamia kodi zote. Kwa nini Kamishna wa Elimu, asimamie elimu ya msingi tu na elimu maalum; elimu ya vyuo vikuu hashughulikii na elimu ya ufundi hashughulikii? Tumpe mamlaka Kamishna wetu wa Elimu. Kama hoja ni sifa, kitu ambacho sioni kama ni sifa, kwa sababu Kamishna wa sasa wa Elimu ni *Doctor*, ana sifa na ninamfahamu, ni mcha Mungu, ni mwadilifu na mchapa kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ili kamishna wetu awe na majukumu kama yanavyotajwa kwenye Sera ya Elimu na Sheria ya Elimu, asimamie sekta zote; ahusike kwenye elimu ya msingi, elimu ya sekondari, elimu ya juu na elimu ya ufundi. Haiwezekani kama mtaaluma mkuu akajifunga katika maeneo machache tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Wizara ya Elimu na Wizara ya Utumishi mlisughulikie hili, turudishe muundo wa zamani ambapo Kamishna wa Elimu, kwa tafsiri nyingine *Chief Education Officer* basi awe Msimamizi Mkuu wa Sekta ya Elimu na siyo ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Charles Mwijage atafuatiwa na Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu na Mheshimiwa *Eng.* Stella Martin Manyanya ajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia sekta ya elimu, ambayo ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nitumie fursa hii kuipongeza Serikali kwa kufanya uamuzi ulioondoa kero katika sekta ya elimu, kero zilizokuwa zinazuia wananchi au

baadhi ya wananchi kupeleka watoto shule, hasa hili suala la karo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hizo pongozi, nizungumzie visiwa vya kwetu. Wilaya yangu ya Muleba inazo kilometra za mraba 7,000 ambazo ni maji na ndani yake ziko kata tano ambazo zina watu wanaishi na visiwa karibu 39.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo na pendekezo langu kwa Serikali, Kata za Ikuza na Mazinga wananchi wenyewe wanahangaika kujenga sekondari. Naiomba Serikali kuitia TAMISEMI, Mheshimiwa Ummy na Mheshimiwa Prof. Ndalichako, hawa wananchi wa Ikuza na Mazinga uwasaide kwa jitihada zao wamalizie sekondari zao. Itatusaidia sisi kuona vifo vya watoto wanaoanguka na mitumbwi wakati wa hali mbaya ya ziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapoondoaa Ikuza na Mazinga unabaki na Goziba, Kerebe na Bumbile. Ninalo ombi, na niliwahi kulipeleka kwa Mheshimiwa Rais, Mungu amlazi mahali pema Peponi, najua Mheshimiwa mama Samia atachukua wazo hili alifanyie kazi. Wananchi wa Kerebe, Goziba na Bumbile wana sekondari yao moja iko Bumbile. Tunachoomba, pesa za sekondari ya Kata, mnazotaka kupeleka kwenye kila Kata msizipeleke Goziba, wala Kerebe, zote mzipeleke Bumbile. Mwende Bumbile mtujengee mabweni na madarasa ya ku-*accommodate* watoto karibu 1,000 ili watoto wa visiwa vyetu 39 wawe wanakaa bwenini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mhamasishaji mkubwa wa elimu, lakini huwa nashindwa kuhudhuria misiba watoto wanapozama kwenye mitumbwi. Ukienda pale, watu wanakuangalia wewe, wanakuona ndio mchawi, kwa sababu ndio ulishawishi mtoto aende shule. Sasa mimi siyo mchawi, mnisaidie kwa kujenga mabweni Bumbile na kujenga madarasa watoto wakae shulenii wasome. Watoto wanataka kwenda kusoma, lakini wanatoka kwenye visiwa vidogo vidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikwambie, Ziwa Victoria kitaalam hubadili hali ya hewa baada ya dakika 25. Unaingia kwenye ziwa liko vizuri, baada ya dakika 25 limebadilika. Mwezi Februari, mimi mwenyewe na wataalam tisa wa Halmashauri tulisalimika kufa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, umeniskia rafiki yangu, Mheshimiwa Mama Joyce Ndalichako umenisikia. Naomba Bumbile Sekondari sasa iitwe Prof. Joyce uweke shule ya bweni ya Serikali watoto waache kufa, nami nikaonekana mchawi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye uboreshaji wa sekta ya elimu. Naunga mkono Serikali kuboresha suala la sheria za elimu, ule Muswada wa Sheria ya Elimu uletwe na kuboresha sera. Ninachotofautiana na ninyi, mnasema mlenge mahitaji ya sasa, ushauri wangu ni kwamba; na Waziri wa Fedha ananisikia; Dira ya Taifa inakwisha mwaka 2025, Dira ya Taifa inapaswa ihuishwe sasa. Dira ya Taifa ya 2025 ni *outdated*, tunapaswa kuangalia miaka 50 mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, leteni Dira ya Taifa ya mbele na sheria za elimu, Sera ya Elimu itakayoundwa iwaandae Watanzania kupambana miaka 50 hadi 60 mbele. Mengine yote yako vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie maboresho yanayoweza kufanyika sasa, nakubaliana na Wizara kwamba wataboresha Shule za Ufundı, wakianzia na Ifunda na lyunga. Wamezitaja shule tisa, hizo shule zilitakuwa maarufu miaka ya sabini nikiwa sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimweleze Mheshimiwa Waziri ajaribu kukumbuka, Ifunda ilipokuwa maarufu tulikuwa na sekondari hazizidi 200 Tanzania. Hizo tisa zilipokuwa maarufu sekondari Tanzania nzima hazikuzidi 200, leo tuna sekondari zaidi ya 4500, kwa hiyo Shule za Ufundı zitengenezwe *proportionally* kwa uwiano, kuwe na shule za Ufundı *proportionally* uwiano wa 9:200 sasa 4,500 itakuwa ngapi? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri, wamelenga kuleta masomo ya ujuzi, wasiwachanganye watoto, wawafundishe mazingira, kilimo, biashara, ufundi, hapana. Tuige mfano wa zamani, ziwepo shule za mchepuo wa kilimo, mchepuo wa biashara, mchepuo wa ufundi, waliosoma *SHYCOM* wanajua. Mwanafunzi aliyesoma *SHYCOM* alikwenda kusoma Chuo Kikuu akirudi *CPA* anaipiga *perseat*. Mwanafunzi wa *SHYCOM* alikuwa na makali yake hata na Waziri wa Ujenzi wa sasa alisoma Chuo cha Ufundii, ndiyo ma-engineer ambao wanatisha sasa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuige mfano wa zamani, chenga ya zamani si mbaya ilimradi goli linafungwa. Kwa hiyo naishauri Serikali iende kwa mfano huo. Kwa mfano, shule za michezo, wachukue shule ya michezo, mtoto anayejua kucheza mpira na kukimbia wafundishe Hesabu, Kiingereza na Kiswahili basi, kinachobaki asubuhi na jioni anacheza mpira, Kiingereza na Hesabu. Kwa hiyo aende, aende, hiyo ndiyo *specialization*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo haisuburi sera, haisuburi sheria ni kunisikiliza na Mheshimiwa Waziri akiniita, anapaswa kuwa na soda, nitamshauri na mambo yanakwenda. Hakuna haja ya kusubiri kubadilisha dira, ndiyo mkakati huo, watoto wanawachosha, wengine wanasema wasome mazingira, wasome na vitu vingi, watasoma mpaka wapi. Mheshimiwa Waziri apunguze ili watu wawe na umahiri (*specialization*) ili waweze kuelewa zaidi tuweze kwenda. Maisha ya binadamu ni miaka sabini, msiwafundishe kana kwamba wataishi miaka 900. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie *VETA*, mtaala wa *VETA*, *VETA* yetu inapaswa kureke...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa  
Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele imeshalia.

**MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie. Tubadilishe mtaala wa *VETA* ulenge sekta za kiuzalishaji, *the productive sectors*. *VETA* si ya kufundisha udereva, udereva wa magari madogo si kazi waende kwenye *productive sectors*; kutengeneza chakula, watengeneze maziwa, watu wanakula hawawezi kuacha kula, kwa hiyo *VETA* ibadilike. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Elimu naamini ukinunua hiyo soda, atakuja aeleze hayo anayosema kwa kirefu zaidi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer Stella Martin Manyanya* na Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, ajiandae.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa uzima kuwepo katika Bunge lako hili Tukufu. Pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii ya Elimu. Elimu imekuwa na falsafa nyingi wakati wa miaka nenda rudi. Kulikuwa na suala la Elimu ni Ufunguo wa Maisha, Elimu ni Bahari, Elimu haina Mwisho. Hayo yote ilikuwa ni kuhakikisha tunahamasisha elimu katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara ya Elimu pamoja na TAMISEMI kwa jinsi ambavyo wanajitahidi kuhakikisha kwamba elimu katika nchi yetu inasonga mbele. Kama tunavyofahamu elimu ndiyo imefanya Taifa hili likafika mahali hapa. Kuna mwanafalsafa mmoja aliwahi kusema anaitwa J.K. Chesterton alisema: "*Education is simply the soul of a society as it passes from one generation to another.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo yote ni mwelekeo wa kuhakikisha kwamba Taifa letu linakwenda kuwa salama kwa sababu wananchi wetu wanapata elimu. Nitakuwa mwizi wa

fadhila nisipoishukuru TAMISEMI kwa jinsi ambavyo wametuletea fedha za mabweni, madarasa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo nitajikita katika maeneo manne kuhusu vikwazo vya elimu. Vikwazo vya elimu viro vingi lakini leo nitajikita katika vinne. Kwanza, suala la lugha, lugha ya kufundishia katika shule za msingi kuanzia chekechea mpaka darasa la saba ni Kiswahili, lakini mtoto huyo anapofundishwa Kiswahili masomo kumi na moja, mara moja anatoka kuingia *form one*, anafundishwa masomo yote Kiingereza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto hawa wanateseka kwa sababu hawajui lugha ya Kiingereza wanapoingia *form one*. Hii inatuleta utata mkubwa, watoto wanachukia shule, hawapendi shule kwa sababu hawaelewi wanapofundishwa darasani *form one* mpaka *form four* na wakati huo huo wanapewa mtihani huo kwa Kiingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niiombe Wizara ya Elimu hebu suala hili liangaliwe kwa sababu ukiangalia shule za *private* kuanzia chekechea mpaka darasa la saba ni Kiingereza, lakini mtoto wa shule ya Serikali anakwenda *form one* akiwa anajua Kiswahili tu, ushindani huu hauko sawa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Waziri wa Elimu atakapokuja hapa atuambie utafiti huu unasema nini kuhusu mtoto wa darasa la kwanza wa Serikali mpaka darasa la saba, akaja akaingia *form one* kwenda *four* inakuwaje? Hapo kuna usawa au tunawatesa watoto kisaikolojia. Naomba tupate maelezo kwamba Serikali inafikiria nini kuhusu hili jambo, kwa sababu hata ukiangalia ufaulu katika za Serikali watoto wanapata *zero* nyingi. Tunasema tupunguze *zero*, tutapunguza *zero* wakati tunawatesa watoto kwa lugha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia shule za *private* wanafaulu sana kwa kiwango cha juu, kwa sababu wao wametoka Kiingereza shule za msingi, wameingia shule za

sekondari lugha ni ile ile ya Kiingereza. Suala hili naomba baadaye Waziri atakapokuja aweze kutueleza vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikwazo kingine ni chakula shuleni. Watoto wanateseka, kule shuleni wanasemwa, Serikali imetoa elimu bure au elimu bila malipo, wazazi wanasemwa hatuwezi kuchangia maana Serikali imetoa fedha. Sasa ni vizuri Wizara ya Elimu na TAMISEMI itoe tamko kwamba kila mzazi ana wajibu wa kuhakikisha kwamba mtoto wake anapata chakula au Serikali itoe chakula mashuleni, kwa sababu tunatengeneza Taifa ambalo tunadhani tuna usawa lakini hatuna usawa. Tutatenga watu walionacho na wasionacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wanaosoma *private* wanakula chakula kizuri mpaka wanamaliza shule, lakini watoto wanaosoma shule zetu za Serikali wanateseka, wanakataa shule, wanaingia makorongoni, wengine wanapata mimba na kadhalika. Ni kwa nini sehemu hiyo Wizara isitoe tamko, imekaa kimya, naomba atakapokuja pia aweze kutujibu kuhusiana na hiyo suala la chakula shuleni watoto wanateseka na kadhalika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la upungufu wa walimu. Hili ni tatizo, mtoto anakwenda shuleni lakini katika masomo ya *physics, chemistry, biology* hakuna Mwalimu, lakini mwisho wa siku anapewa mtihani, kuna usawa gani hapo? Naomba Serikali iijitahidi kwa kadri iwezavyo kuwaajiri Walimu hasa wa sayansi ili kuleta usawa katika shule za Serikali na *private*, vinginevyo tutatengeneza Taifa la wenye nacho na wasio nacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba suala la Walimu liangaliwe, waajiriwe walimu wa kutosha. Nilikuwa nasoma taarifa ya Umoja wa Mataifa inasema hadi kufikia 2030 inahitajika Walimu milioni 69 kukidhi. Je, Tanzania sisi tumejiandaaje na suala hilo la kuhakikisha kwamba tumekuwa na Walimu wa kutosha. Pia, naomba Waziri atakapokuja atuambie pamoja na kwamba kuna ajira 6,000 za Mheshimiwa Rais wetu, mama Samia Suluhu Hassan

amesema waajiriwe, lakini bado kuna haja ya kuongeza jitihada za kuhakikisha kwamba Walimu wanatosheleza ili kuleta usawa katika shule zetu za *private* na shule za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, naomba suala la elimu ujuzi, wenzangu wamezungumza sana. Tuhakikishe kwamba katika Taifa letu mtu akimaliza, sio anazunguka na vyeti kutafuta kazi, anazunguka na vyeti huku na huku, kazi, kazi, lazima Wizara ya Elimu itengeneze Elimu Ujuzi. langalie namna gani itatengeza hiyo sera ili iweze kuhakikisha kwamba watu wetu wanakwenda kusoma lakini wawe na ujuzi wa kutosha kujajiri na hata kuajiriwa ndani na nje ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Noah.

Mheshimiwa Waziri nataka kuamini yale uliyosema utasikiliza mawazo ya wadau mbalimbali, hii hoja ya lugha huwa inajitokeza sana, nadhani ni kwa sababu hakuna maelezo mahsusiyaliyowahi kutolewa ili watu tupate tofauti ya lugha na maarifa. Je, kuna mchango wowote wa lugha kwenye kutoa maarifa kwa mtu mmoja kupeleka kwingine. Kwa sababu mambo mengi tunayozungumza ni mapya. Baadhi yetu tulisoma kwenye mifumo ile unatoka nyumbani unaongea lugha mama, kwa maana ya zile lugha zetu za kiasili, unaenda kuanza Kiswahili darasa la kwanza, unaenda *form one* unaanza Kiingereza, unaenda *A level* kingereza ama chochote utakachosoma, unaenda Chuo Kikuu, lakini huko kwote ulikuwa unakutana na hii aina ya hawa tunaofikiri wapo vizuri zaidi.

Ukienda darasa la kwanza utakutana na watoto wa mjini mjini hivi, wao wanazungumza Kiswahili, lakini si kwamba wao wanakuzidi maarifa darasani. Wewe pia unaweza ukafanya vizuri tu, pamoja na kwamba lugha umeanzia ngazi hiyo. Kiingereza pia ni hivyo hivyo, ukienda kidato cha kwanza

utakutana na waliosoma shule hizi tunazofikiri wameanzia shule ya awali Kingereza, lakini hawakuzidi darasani.

Waheshimiwa Wabunge, najaribu kueleza namna ambavyo lazima tupate huo uelewa, tusipoupata tutazungumza kila siku kwamba pengine tukitumia Kiswahili maarifa yataenda vizuri, lakini humu ndani tu tukisikiliza Wabunge ambao wengine hawakupata hiyo fursa, Kiswahili chenyewe ni shida, yaani mtu kuinyoosha sentesi moja ya Kiswahili fasaha hawezi. Kwa hiyo, je, hayo ni maarifa au ni tatizo tu la lugha kwamba tuna tatizo la kujua lugha. Kwa sababu tusije tukakimbilia tu, kwenye Kiswahili halafu tukajikuta hata hicho Kiswahili chenyewe hatuna uwezo wa kupeleka maarifa kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Ni vizuri sana tupate uelewa huo itasusaidia Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa *Engineer Stella Martin Manyanya* nilikuwa nimeshamtaja, atafuata Mheshimiwa Tunza Issa Malapo na atafuatiwa na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa kupata muda huu wa kuweza kuchangia. Nianze kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, lakini pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi ambavyo anavyotuongozoa. Pia niwashukuru ndugu zetu wa Kenya kwa jinsi ambavyo wamempokea vizuri Mheshimiwa Rais wetu, basi nasi tunafarijika kwa faida ya pande zote mbili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianzie kwanza na Jimbo langu, niishukuru sana Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kutuwezesha kupata Chuo cha *VETA* ambacho ningembo sasa kiweze kuanza na kuondoa kero ya ajira hasa kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, naomba kuna shule ya Mbambabei *High School* ambayo Wizara iliisaidia lakini sasa hivi kuna jengo pale Jengo la Utawala na Maktaba ambalo ni jengo moja kwa muda mrefu halijaweza kukamilika. Niwaombe kupeleka fedha ili jengo hili sasa liweze

kutumika na kuwasaidia hawa wanafunzi ikizingatiwa kwamba shule hii toka imeanza imefanya wanafunzi wake wafaulu vizuri na kweli inashika katika nafasi nzuri za kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna maboma ambayo yalikuwa yamepewa fedha ya mabwalo na michoro maalum, lakini imeonekana kwamba zile fedha huwa hazitoshelezi kujenga hayo mabwalo. Kwa hiyo niombe tumalizie hayo mabwalo kwa sababu fedha nyngi za Serikali zimeshatumika na nguvu za wananchi, hivyo ni vema tuyamalizie. Kuna pale Nyasa, kuna shule ya *Engineer Stella Manyanya* na Liuli ambayo inaendelea sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba nimefurahishwa pia na michango mbalimbali ambayo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wametangulia kuzungumza. Michango ambayo imekuwa, imetazama kwa kina kiasi kwamba pengine kama itafanyiwa kazi inaweza ikarekebisha sekta hii ya elimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, nipende kuwakumbusha ndugu zangu hawa na wananchi kwa ujumla, si kwamba nchi yetu imekuwa haina mikakati maalum ya elimu, tatizo ninaloliona ni uendelevu na wakati mwingine kufanya maamuzi ambayo yanakuwa, yaani kama vile mmoja hana taarifa za kutosha, kwa hiyo ikifikia kufanya maamuzi akimsikia wa kwanza, wa pili wamezungumza, basi maamuzi yanafanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano katika hili suala la ujuzi linalo zungumzwa siku zote, hili suala si jipya, suala la ufundu si jipya tumekuwa na shule maalum za sekondari za ufundu, lakini shule hizi kwa sababu moja au nyininge, naweza nikasema zilifanyiwa uharamia, vifaa vikauzwa, wanafunzi pale wakawa hawafundishwi tena ufundu. Vile vile unakuta sasa hivi hizo shule zilikuwa kuwachukua sasa wanafunzi wa elimu ya sayansi ya kawaida. Ukifuatilia ni kwa nini? Ndiyo maana nasema pengine kwenye Wizara hii ipo haja sana hata mambo ya usalama yaimarishwe, kwa sababu unaweza ukapewa ushauri mwingine ambao unajua baada ya miaka

mitano utaua kabisa ile dhamira ya nchi kuipeleka mahali fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano mimi binafsi niseme kwamba nilikuwa kwenye Wizara hii na ninapozungumza sijaribu kusema kwamba hakuna kinachofanyika, Mawaziri wanafanya kazi kubwa na wataalam wanafanya kazi kubwa, lakini hayo ndiyo niliyoyaona kipindi hicho, vyuo havina Walimu wa ufundi. Leo hata ukianzisha vyuo vya ufundi, hawa Walimu wapo kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna ile hali ya mihemko, kwa mfano kuna wakati ilisemwa kwamba huyu amemaliza *Advanced Diploma*, ya nini? Labda umeme au ufundi, huyu mshahara wake utakuwa mdogo kuliko yule wa *degree*. Nani atakuwa mjinga akasome *Advanced Diploma* ambayo ni *competence base* aache kwenda kwenye *degree* na uwezo anao? Kwa hiyo hayo ni mambo ambayo yanasaababisha watu kufanya maamuzi yasiyo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunazungumza kwamba Watoto wengi wakimaliza vyuo hawawezi kujajiri, ni kweli hata wakikaa chuoni hawataweza kupata ujuzi wote, lakini hayo mazingira ya kujajiri huko kwenye maeneo yetu yakoje? Nani anafurahia sasa hivi aende kujajiri kwenye uvuvi ambapo uvuvi bado anatumia kale kamtumbwi ambako hajui kama atapona. Kwa hiyo lazima tujenge mazingira mazuri ambayo yanamfanya huyu mtoto akimaliza chuo aweze kwenda kujajiri. Bila kufanya hivyo tutakuwa tunazungumza lakini hatutafika. Kwa hiyo ninachoomba, wakati utakapofikia wa kufanya marekebisho au maboresho mbalimbali, ni vema kuangalia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulianzisha chuo kwa mfano Chuo Mahiri kile cha Nelson Mandela, lakini unapokuja kugawa rasilimali unakuta chuo kile ambacho unakitaka kifanye mambo makubwa ya umahiri kinawekewa bajeti sawa sawa na chuo kingine ambacho kinafanya mambo ya kawaida. Kwa hiyo kama hatutakuwa tunawekeza kulingana

na mahitaji halisi ya kumwezesha huyu mwanachuo aliyepo kwenye eneo fulani, tutakuwa tunapoteza muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya kiufundi, kisayansi au utafiti mara nyingi tunaona uchungu sana kuyapatia fedha, unaona kama vile unapoteza, ukimpa fedha akanunue sijui ka-resister, ka-transistor unasema mbona hela nyingi hii naenda kununua ka-resister, lakini hatujui kwamba katika mafunzo ya aina hiyo lazima mtu ajue kuharibu, ajue kufanya kitu kikawa sawa. Atajua kitu kimekuwa sawa baada ya kujifunza kwa njia zote. Amekosea, ameharibu lakini baadaye anakuja kupata jambo ambalo ni jambo zuri. Kwa hiyo tuseme tutakavyosema hatutakwenda kufanikiwa. Pia tuhakikishe kwamba tunawekeza kwenye wabobezi wa maeneo hayo ya kazi za vitendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisiposema kwamba nchi yetu imeweza, imefanya mambo mengi. Siku za nyuma ulikuwa hata nyuma tunazojenga ukiziangalia zipo ovyo ovyo tu, lakini siku hizi baada ya kuwa na hao vijana ambao wengine wametoka VETA, wanajifunza maeneo mbalimbali hali yetu ya kiuchumi na kijenzi au uwekezaji imekuwa ni tofauti na ilivyokuwa. Kwa hiyo lazima tujipongeze kwa yale ambayo tumeyafanya vizuri, lakini tuendelee kuboresha katika maeneo yale ambayo bado hayajawa vizuri. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niseme tu kwamba...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana! Mheshimiwa Tunza Issa Malapo atafuatiwa na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mheshimiwa Kabula Enock Shitobelo ajiandae.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi asubuhi ya leo niweze kuchangia.

Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema. Nianze kuchangia kwenye *issue* ya kubadilisha mtaala. Kwangu nafikiri Serikali inatakiwa ifanye hili jambo kwa utulivu kwa kusikiliza wadau, ninachoona elimu yetu ya Tanzania wakati mwagine inaathiriwa sana na matamko ya kisiasa. Mwanasiasa mwenye madaraka akiamka asubuhi analolifirkiria yeye bila kufuata ushauri wa kitaalam kwasababu, kwenye elimu kuna mambo mengi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia kubadili mtaala sio jambo la siku moja. Tunatakiwa tufanye *need analysis* kwa nini huu uliopo haufai na kama haufai tunaongeza nini au tunapunguza kitu gani? Sio suala la kuamka siku moja ukasema watoto wasijifunze hiki wajifunze hiki na kunatakiwa kuwe na taratibu lakini kuwe na maandalizi. Kwa sababu, unapobadilisha mtaala ukumbuke unatakiwa walimu nao uwafundishe waweze kwenda kuutekeleza ule mtaala ambao wewe unautaka. Lakini unakwenda kubadilisha mtaala elimu za msingi, walimu ngazi ya cheti wanafundishwa yale yale ya zamani, hiko ndio kilichopo sasa hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, fuatilia mtaala wa ngazi ya cheti unaofundishwa, halafu fuatilia mambo tunayoyataka watoto wetu wa shule za msingi wayasome. Kwa hiyo, ninachoomba tufanye mambo kwa utulivu tuangalie, tumetoka wapi? Tuko wapi? Na tunataka kwenda wapi? Tuache mihemko tuna wataalam wazuri kweli kweli tuepuke mambo ya kisiasa.. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda kuzungumzia Idara ya Udhibiti Ubora, kwangu natambua sana umuhimu wa Idara ya Udhibiti Ubora, lakini kila tukisimama humu ndani hata ukisoma hotuba ya kamati imeeleza wana changamoto kubwa ya fedha. Tunaweza leo tukaona udhibiti ubora hawafanyi kazi zao sawasawa pamoja na mambo mengine, lakini wanakosa bajeti ya kutosha. Ili mtu aweze kukagua ni lazima afike, anafikaje kama hana gari, hana mafuta, hana vitendea kazi ama watumishi wachache? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anajua namna Idara hii ilivyo na changamoto ingawa kuna baadhi ameanza kuzitata. Nikiri kwasababu, nafuatilia najua kuna baadhi zimeanza kutatuliwa lakini nguvu zaidi inahitajika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kitu kingine ninachotaka kusema, kila mtu anahitaji watoto wasome, yaani mimi Tunza ukiniliza ninahitaji wamakonde wenzangu kule kwetu wasome. Lakini, *Issue* inakuja mdhibiti ubora yeye ana *checklist* ili asajili shule kuna vigezo ambavyo vimewekwa. Shule iwe na choo, iwe na madarasa mangapi, iwe na ofisi, iwe na madawati, kuwe na vitabu, kuwe na walimu kuwe na nini, anaweza kuisajili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sio kwamba akikuta tu wanafunzi wamekaa wanasoma anaweza kusajili. Sasa pendekezo langu kwa Wizara, tunataka wasome lakini pia tunataka wasome katika mazingira bora. Kwasababu, tendo la kujifunza linahitaji mazingira bora tusichukulie tu kwamba, watu tunataka wasome *no!* Tunataka wasome katika mazingira bora. Labda, kwasababu, *population* inaongezeka mahitaji ya watoto kusoma ni makubwa. Labda tuangalie mrudi kwenye zile *checklist* ikiwezekana basi hizi shule zipangwe kwa madaraja. Kwamba, hii imesajiliwa imekidhi vigezo vyote, hii tumaisajili tunaipa uangalizi miaka mitatu, hii tunaisajili tunaipa uangalizi mwaka mmoja urekebishe hiki na hiki na hiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda twende kwa mtindo huo tunaweza tukafanikiwa, lakini tukiacha tu kwamba kila shule mtu akitaka isajiliwe basi isajiliwe, hata kama haijatimiza vigezo maana yake ni nini? Tunaweza kwenda kusajili shule lakini zikatoa elimu ambayo sisi hatukuitarajia. Matokeo yake tukija humu ndani tena tutakuja kulalamika kwamba, watoto wetu wanajifunza lakini hawaelewi hawawezi kuajirika kumbe tumeharibu msingi tangu kule wakati tunasajili zile shule zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hilo suala kwasababu, tunataka watoto wetu wasome ni suala la kukaa wakaguzi waangalie namna gani wanakwenda kuweka vigezo mbalimbali na shule zingine ziwe kwenye uangalizi ili kusudi watoto wasikose kusoma lakini pia wasome katika mazingira ambayo yataweza kuwfafanya wao wajifunze vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda kumalizia kwenye hoja ya vyuo vya ualimu. Natambua kwamba, Serikali kuna baadhi ya jitihada imefanya ikiwemo kuboresha majengo ya vyuo vya ualimu. Kwa mfano, Chuo cha Ualimu Mtwara kawaida kweli majengo yameboreshwa, lakini uboreshaji ule wa majengo yale uende sambamba na uboreshaji wa maslahi ya wafanyakazi. Unaweza ukawa na majengo mazuri lakini wafanyakazi waliopo pale kama huwatekelezei matakwa yao kwa mujibu wa sheria, wafanyakazi wa vyuo vya ualimu hata *annual increment* ya mishahara yao ni shida. Hata kupata pesa za likizo, kupata nauli, kupandishwa madaraja, kulipwa kwa wakati kwao ni shida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wale wafanyakazi wa vyuo vya ualimu wakufunzi ni watu wa kuwaangalia kwa jicho la pekee. Kwasababu, elimu yote tunayozungumza shule za msingi ndio wao wanakwenda kutengeneza walimu. Lakini pia, Mheshimiwa Waziri namuomba akaangalie namna mtaala wa *grade A* ule wa cheti, unavyoendana na mabadiliko yanayofundishwa shule za msingi. Kama kuna *gap* tunaomba hilo *gap* walitoe kwasababu, nimekuwa nikifutilia sana wakufunzi wanalamika kwamba, kile kitu ambacho kiko huku kwenye ngazi ya cheti, ni cha zamanii ukilinganisha na kitu ambacho kinafundishwa shule za msingi sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zile *TRCs, Teachers Resource Centers* naomba zitumike kwasababu, niliongea hapa hata kisu kinatakiwa ukikinunua unakitumia baadaye unakinoa kuongeza makali yake. Kwa hiyo, zile *TRCs* zilikuwa zinasaidia walimu kufanya mafunzo kazini, wanakwenda pale

wanaongezewa maarifa kwa hiyo, mambo yanakwenda vizuri. Naomba uangalie sana Idara ya Ukaguzi kwa jicho la pekee kwasababu, Idara ya Ukaguzi ndio CAG wa elimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo machache nakushukuru sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, atafuatiwa na Mheshimiwa Kabula Enock Shitobela. Mheshimiwa Fred Atupele Mwakibete ajiandae.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote niitumie fursa hii kuipongeza Wizara ya Elimu na Serikali kwa ujumla, kwa maamuzi yaliyofanyika kuititia sera ya elimu ya kuanzisha shule za kata, ambazo zinasaidia wanafunzi wengi hasa wale wanaotoka kwenye familia za masikini. Uamuzi huu ulikuwa uamuzi mzuri sana kwa Taifa letu hili linaloendelea kwasababu, imetoa fursa ya watoto wengi wanaoishi kwenye mazingira ya chini kupata fursa hiyo ya kupata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kuititia takwimu takribani kwa sasa tuna shule za kata 3,900, shule hizi zimejengwa kwa nguvu za wananchi na kumaliziwa na Serikali kuititia Wizara yetu ya Elimu na Wizara ya *TAMISEMI*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hoja yangu leo katika shule hizi ninajaribu kutizama ni namna gani tunaweza tukafanya maboresho na kuzalisha watoto wenye elimu inayostahili, kwa maana ya elimu bora kutoka kwenye shule zetu hizi. Ni mwalimu *by professional*, shule ili iitwe shule lazima iwe na walimu na wanafunzi lakini lazima iwe na madarasa, maktaba na maabara. Kwa sababu, tunaamini katika elimu, elimu anayopata mwanafunzi darasani ya kufundishwa na mwalimu ni asilimia 25 peke yake zaidi ya asilimia 75 ya ujuzi anaoupata mwanafunzi, inatokana na mazingira yanayomzunguka. Kwa maana anajifunza kutoka kwenye maabara, lakini anajifunza kutoka kwenye maktaba ili kuweza kupata ubunifu na stadi ambazo anastahili kuzipata. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye shule zetu hizi zaidi ya 3,900 tunakosa hayo mazingira ya kumuwezesha mwanafunzi kujifunza, kwa maana shule zetu hazina maabara na shule zetu hazina maktaba. Mazingira ya kujifunzia ni magumu sasa nini kifanyike? (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe sana Serikali kupitia Wizara ya Elimu na pengine kushirikiana na TAMISEM/ambayo ndio wasimamizi wa hizi shule za kata. Kuangalia sasa namna gani Serikali inaweza kuweka malengo ya makusudi, kukamilisha maabara katika maeneo mengine ambayo zimeshaanza kujengwa. Lakini kuweka maktaba kwa ajili ya kuwasaidia watoto hawa wa wakulima na wanyonge wa Tanzania, waweze kupata elimu sawasawa na watoto wa matajiri na wale wanaoishi kwenye miji mikubwa ambayo ina shule nydingi ambazo zina hali nzuri ya kutolea elimu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipenda kulizungumza hili kabla sijakuja kwenye hoja yangu ambayo nilitamani kuizungumza zaidi leo kuhusiana na *specialization*. Namna ya kupanga michepuo kwenye shule zetu na hii sio tu kwa zile shule maalum zinazosimamiwa moja kwa moja na Wizara ya Elimu, lakini vile vile, kwenye hizi shule zetu za kata. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi ambacho sisi tulikuwa shulenii tunasoma tulikuwa tunaona, ukienda kwenye shule fulani utakuta kuna michepuo wa kilimo, ukienda shule nydingine utakuta kuna michepuo wa ufundi, unaenda shule nydingine ni michepuo wa sanaa. Haikuwekwa bahati mbaya ilikuwa inawafundisha wanafunzi kujidendeza kutengeneza ujuzi na maarifa tangu wakiwa katika ngazi za chini kabisa za kupata elimu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, na ukiwa mwalimu ukifundisha kidato cha kwanza mtoto anasoma pale kwa takribani mwaka mmoja, akienda kidato cha pili tayari umeshamfahamu kwamba, huyo mtoto anaweza kwenda kwenye michepuo gani? Na unamshauri kwenda *ku-specialize* kupunguza mzigo wa masomo ambao mwisho wa

siku hauwezi kumsaidia. Mtoto anapangiwa anakwenda kwenye *combination* za sayansi, mwingine anakwenda kwenye *combination* za sanaa, mwingine za biashara. Na mwisho wa siku ndio tunakuja tunapata *ma-accountants*, tunapata hawa madaktari, tunapata na watu wa namna hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niiombe na niishauri sana Serikali hoja hii pia ameizungumzia vizuri Mheshimiwa Charles Mwijage, hatuna sababu ya kuwafundisha watoto wetu *general education*, tutengeneze *specifically* tunataka mtoto ahitimu akiwa ameiva kwenye eneo gani mahsusii katika elimu anayopata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *specialization* kwenye elimu ni suala muhimu sana. Hivi tunalalamika leo tunataka kubadilisha mfumo wa elimu, tunataka kubadilisha mtaala wa elimu, kwa mashaka tu kwamba pengine huu mtaala haumsaidii mtoto kuweza kukabiliana na mazingira anayoyaishi. Lakini kiukweli mtaala hauwezi kutusaidia, kama hatujaamua kumuandaa huyu mtoto kwenye mazingira yake tangu mwanzo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tulikuwa tunasema jana, Mheshimiwa mmoja alizungumza humu ndani, kuna dhambi gani mmasai kuingia darasani na kumfundisha mtoto namna ya kufuga ng'ombe? Kuna dhambi gani kumuita mvuvi, baharia akaingia darasani akafundisha mtoto namna nzuri ya kuvua samaki? Hata wakati tunasoma walimu walikuwa wanakaa pembeni anamuita *traffic* anafundisha watoto namna ya kuvuka barabara, ni elimu. Elimu tusiwekee mipaka kiasi cha kuwafanya wanafunzi wetu kukariri, tutengeneze mazingira ambayo mtoto anaweza kujifunza kadri mazingira yake yanavyomruhusu na kutengeneza ujuzi wa kuweza kuendeleza maisha yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya jambo hilo nizungumze kidogo kuhusiana na soko la elimu. Tumeingia kwenye mazingira ambayo elimu sasa inakwenda kuwa ni biashara. Tuna shule za *private* na tuna shule za Serikali. Shule

za *private* Mheshimiwa Waziri pia uje ultizame vizuri, inawezekana kuna namna fulani inatengenezwa siasa ya kuwaaminisha umma kwamba, shule za *private* ndio zinatoa elimu nzuri kuliko shule za Serikali. Lakini ukweli ni kwamba, shule za Serikali zina mazingira mazuri, zina walimu wa kutosha, zina maeneo mazuri ya watoto kujifunzia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ukitaka kumfundisha mtoto masuala ya kilimo shule ya kata ya msingi labda, Kwemakame ina eneo zuri la kuweza *ku-practice* kilimo kuliko shule ambayo inapatikana pale Dar es Salaam. Kwa hiyo, tuna haja pia ya kuuza na kutoa namna gani shule zetu zina mazingira mazuri ukilinganisha na hizi za *private*, mwisho wa siku tutakuwa... (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa kengele ya pili Imegonga.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Haya. Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe huwa inabidi ukichangia utazame huku mbele ukishaona nimewasha *mic* ili nisikukatishe sentensi yako, ukimaliza unaunga mkono hoja. Kwasababu, nikikuzungumzisha maana yake inaingia hiyo kwenye taarifa rasmi za Bunge. Kwa hiyo, muwe mnaangalia hapa nikiwasha ujue muda umefika malizia sentensi ili uwe unamatiliza vizuri mchango wako. Mheshimiwa Kabula Enock Shitobeloo atafuatiwa na Mheshimiwa Fred Atupele Mwakibete, Mheshimiwa Almas Athuman Maige ajiandae.

**MHE. KABULA E. SHITOBELO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia katika Wizara ya Elimu. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema hata uhai pia. Napenda kumpongeza Rais wetu mpendwa Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anazoendelea kuzifanya. Niende moja kwa moja kuchangia hoja hii ya Wizara ya Elimu. Tatizo la ajira katika nchi yetu limekuwa tatizo kubwa sana,

kusababisha matatizo mengi kwenye familia hasa kwa kina mama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, wakinamama wengi wanalea watoto kupitia biashara ndogo ndogo kama mama lishe na kutembeza hata vitu vidogo vidogo, kwa ajili ya kujipatia pesa kwa ajili ya kutunza watoto wao na vile vile kuwapeleka shule. Mama huyu wakati anampeleka mtoto shule anakuwa na imani kwamba, baada ya kuhitimu masomo mtoto yule ataweza kuwa mkombozi wake. Lakini, badala yake mtoto yule anapohitimu masomo anajikuta anaongeza mzigo tena kwa mama yule, anaanza tena kutembea kila siku na vyeti kwenda kutafuta kazi akitumia nauli ya mama yake, anaomba kila siku kwa mama nauli. Kwa hiyo, inazidi kumuongezea shida mama huyu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na ukizingatia mama huyu anakuwa amekopa mikopo kwenye *SACCOS* na sehemu mbalimbali kama *VICOBA*, ili aongezee ule mtaji wake na kuweza kupata *school fees* ya mtoto wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa naiomba Wizara ya Elimu ijaribu kuangalia mitaala yake lakini pia, iwajengee watoto *confidence* kuanzia utotoni kwamba, haendi kusoma kwa ajili ya kufanya kazi au kuajiriwa. Wawajenge kisaikolojia kwamba, anaenda shule kutoa ujinga au kuongeza elimu ya vitu mbalimbali. Lakini nia yake ni kupata biashara, akifanya biashara anauwezo wa kutengeneza maisha yake au kutengeneza faida kubwa kuliko hata huo mshahara ambao angeenda kulipwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niiombe sana Wizara ya Elimu ijaribu kuliangalia hilo, ili kuwajengea uwezo watoto wetu wa kujitegemea kuliko kutegemea ajira. Mfano, tukiangalia matajiri wengi duniani ni wale ambao hawakusoma sana je, tumejaribu kujuliza ni kwa nini wale ambao hawakusoma sana wameweza kufanikiwa sana katika biashara au katika kujitegemea? Jibu ni kwamba,

waliona hawana *option* nyingine hawakusoma hawana vyeti vizuri nya kuweza kuajiriwa katika nyadhifa nzuri. Kwa hiyo, ndio maana wakasimamia zile biashara zao au kazi yao, kama walikuwa wakilima walilima vizuri na kuhakikisha mazao yale yametoka kwa wingi na kuweza kuuza kupata pesa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizidi kuiomba Wizara ya Elimu isimame vizuri kuangalia hiyo mitaala hata kama ni mtoto anakwenda kusoma kama anasomea kilimo, akitoka pale akaweze kulima na kuangalia ni nini kitakachowea kumpatia manufaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndio mchango wangu, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilishamtaja Mheshimiwa Atupele Mwakibete atafuatiwa na Mheshimiwa Athuman Maige, Mheshimiwa Salma Kikwete ajiandae.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma ambaye ametufanya tuwepo katika Bunge lako hili Tukufu. Pili, nimpongeze sana Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Prof. Joyce Ndalichako kwa kuiongoza vizuri Wizara hii ya Elimu pamoja na Naibu wake na watendaji wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa, nimshukuru Mheshimiwa Waziri na Serikali yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo wameweza kulitendea haki Jimbo la Busokelo. Busokelo mengi yamefanyika kupitia Wizara ya Mheshimiwa Prof. Ndalichako hususan ujenzi wa shule mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza katika Mkoa wa Mbeya mojawapo ya halmashauri

zinazofanya vizuri sana kwenye mitihani ya kidato cha nne Busokelo tumekuwa tukiongoza kwa miaka miwili mfululizo. Hii ni kutokana na msaada mliotupatia kama wa ujenzi wa shule za wasichana na za watoto wa kiume. Kwa mfano, *Busokelo Girls* imejengwa na inafanya vizuri na ndiyo inayoongoza, *Busokelo Boys* imejengwa inafanya vizuri na inaongoza. Kuna shule nyingine zimekarabatiwa kama Ntaba Sekondari, Mwakaleli Sekondari, Ruangwa, Lufilyo, kwa kweli mnastahiki pongezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zaidi ya yote mmejenga na Chuo cha VETA ambapo leo hii *VETA* Busokelo inachukua wanafunzi kutoka mikoa mbalimbali. Niipongeze sana Wizara hii kwa sababu hivi karibuni walitoa agizo kwamba vyuo vyote vya *VETA* vichukue wanafunzi na ambao siyo wanafunzi waende kusoma katika vyuo vyote nchini. Busokelo tumelitekeleza hilo na hadi sasa wameshajilidhisha zaidi ya wanafunzi 300. Kwa hiyo, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu na kwenye Vitabu vya Imani mfano Biblia imesema: "Mkamate sana elimu, usimwache aende zake; Mshike, maana yeye ni uzima wako". Maneno haya ni kutoka Mithali 4:13 ndiyo maana tunang'ang'ana na suala zima la elimu. Mataifa mengi yaliyoendelea yamewekeza sana kwenye sekta ya elimu. *Nicompliment* michango ya Waheshimiwa Wabunge kwamba Taifa kama China waliwekeza sana katika ufundi ama vyuo vya kati ndiyo maana leo hii ipo vile ambavyo tunaiona. Hawakuwekeza sana katika vyuo vikuu kwa sababu waliona wafanyakazi wazuri ni wale ambaao wamepata elimu ya kati ama vyuo vya kati. Kwa hiyo, naamini pia tunaweza tukajifunza kuititia kwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi inayoongoza kwa kutoa elimu bora dunia nzima ni Finland. Pia tunaweza tukapeleka wataalam wetu huko wakajifunza kwa nini Finland inaongoza kwa kutoa elimu bora. Ukitisoma ripoti mbalimbali za *World Economic Forum* pamoja na ripoti zingine utaona hiki nachozungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri yafuatayo katika sekta ya elimu. Tumezungumza suala la mitaala, ni kweli ni changamoto na Mheshimiwa Waziri ametoa *commitment* hapa kwamba wanakwenda kuibadilisha ama kuihusisha mitaala hii ya elimu. Ikipendeza Mheshimiwa Waziri anaweza kutuma wataalam wake ama wao wakaja huku wenzenetu wa South Africa, wana mfumo ambao nimewahiusema huku Bungeni ambao unawasadia sana vijana wengi ambao wanamaliza vyuo na wengine wakiwa vyuoni kupata kazi baada ya kumaliza masomo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wao wanatumia mfumo unaitwa *Youth Education System (YES)*. Tafsiri yake hawataishia tu kwamba wakisoma imetoka lakini Serikali inafanya utaratibu mara baada ya kumaliza masomo yao ya vyuo kuwaunganisha na taasisi, mashirika na makampuni mbalimbali yaliyopo katika nchi yao. Sisi pia tukifanya hivyo maana yake wanapotoka kule wanakuwa na ujuzi kamili kwa sababu kwa miaka hii mitatu mwanafunzi akiwa chuoni siyo rahisi sana kupata uzoefu wa kusema anaweza kufanya kazi bali akiunganishwa na taasisi na mashirika ambayo yanafanya kazi tayari itakuwa rahisi sana huyo mwanafunzi kupata ujuzi lakini baadaye kuajiriwa na taasisi hizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nataka nizungumzie suala la Bodi ya Mikopo. Nimezungumza hapa mara nyingi na tarehe 31 Machi, 2021 niliuliza swali, je, ni sifa zippi za mwanafunzi ambaye anastahili kupata mikopo? Mheshimiwa Naibu Waziri alieleza lakini ukweli Bodi ya Mikopo kuna haja ya msingi ya kufanya *either transformation* ama kubadilisha kanuni zinginezo ili wanafunzi wote wenye sifa wapate mikopo siyo kama ilivyo sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mionganoni mwa Wabunge ambao nimewapeleka wanafunzi wangu zaidi ya 20, zaidi ya mara mbili au mara tatu kwenda Dar es Salaam kuwatafutia mikopo maana wana sifa lakini hawapewi mikopo. Ukitutana na Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Mikopo atakwambia vizuri kabisa lakini utekelezaji wake unakuwa haupo. Nashauri Mheshimiwa Waziri aiangalie vyema hii Bodi

ya Mikopo kwamba kuna haja ya msingi ya kubadilisha mifumo inayotumika pale ama kuiboresha zaidi ili wanafunzi wote wenye sifa wapate mikopo hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Mheshimiwa Mbunge aliyechangia jana mikopo hii isiwe tu kwa vyuo vikuu. Tumezungumza hapa kwamba nguvu kazi kubwa ipo katika vyuo vya kati, kama tutaweza kutoa mikopo hata kwa vyuo vya kati ndiyo tutapata nguvu kazi ya kuzalisha lakini uchumi utaboreka zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni suala zima la upungufu wa walimu katika shule na halmshauri zetu. Busokelo peke yake walimu wa sekondari kuna upungufu wa zaidi ya walimu 93, walimu wa shule za msingi 439 pamoja na matundu ya vyoo zaidi ya 500. Kwa hiyo, tunawaomba Mheshimiwa Waziri utakapokuja ku-*wind up* hapa aone namna gani anaweza kutusaidia katika jimbo hili la Busokelo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunajenga shule nydingine kwa kushirikiana na wananchi wa Busokelo, kuna shule inaitwa Kifunda Sekondari, Ntaba Sekondari na Ndembro Sekondari. Pia nitumie fursa hii kuwapongeza sana *Diaspora* wa Busokelo ambao wameendelea kuiwezesha na kuichangia shule yetu ya sekondari inayoitwa Busokelo *Girls*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na hayo nataka nimalizie kwa kusema, tukiboresha vyuo vya VETA kwa maana ya vyuo vya ufundi, nina hakika elimu yetu ya Tanzania na ajira hakutakuwa na changamoto kwa kuwa watakuwa wamepata ujuzi hakika na sahihi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkongo hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Athuman Maige atafuatiwa na Mheshimiwa Salma Kikwete, Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya ajiandae.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kuniruhusu nichangie Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa kweli lazima nikiri kwamba Wizara hii imefanya kazi kubwa sana jimboni kwangu na nchi nzima. Mimi kwangu nawapongeza sana kwa kunijengea shule za upili wa juu. Tulipoingia madarakani hatukuwa na hata shule moja ya upili wa juu yaani high school tunazo mbili sasa. Pia wananijengea *VETA* na hii itasaidia sana kupeleka fedha vijijiini kwani mafunzo yatakayopatikana watafanya kazi vijijiini. Vilevile tumepata fedha za maboma na tumejenga nyumba za walimu na madarasa na tumepata madawati. Hapa pia nilishurukuru Bunge letu, Bunge lilitupa madawati ambayo yamekwenda kuwekwa kwenye shule zangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo siongelei ufundi kwa sababu Mheshimiwa Manyanya amenigusa sana kwamba ilikuwa hujuma kuua shule za ufundi. Hili lichukuliwe kama ni sababu kubwa sana ya kulegalega kwa elimu ya ufundi hapa nchini, hujuma hii ilitupata sisi Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitaongelea suala la lugha ya kufundishia na *VETA* kuwa chini ya Wizara ya Elimu na Sayansi. Kiswahili mmekigusa kidogo mimi safari hii naomba Serikali ianzishe shule ya mfano itakayoanza kufundisha kwa Kiswahili kuanzia darasa la kwanza mpaka chuo kikuu. Wazo hili lilikuwepo sijui kwa nini Serikali haikuanzisha shule ya mfano. Ichukue shule yoyote ambayo watoto wapo darasa saba waendelee *form one* Kiswahili, shule moja tu tuone matokeo yake. Maana tunabishana wataalam hawataki kusoma tafiti ambazo zipo pale *TATAC* na *BAKITA*. Watu wote waliofanya utafiti kwa miaka 40 wamesema Kiswahili ni lugha mama Tanzania ifundishwe, bado watu hawataki kutofautisha kati ya elimu, maarifa na lugha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naionba Serikali na Mheshimiwa Waziri akija hapa na nitazuia shilingi atuambie

tatizo gani lilizuia Serikali kuanzisha shule ya itakayotumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia. Tunaandikia mate na who upo, si tuanzishe tu shule leo iende mpaka *form four, form five* Kiswahili. Vitabu vyote *TATAC*vipo, wameshaandaa kitabu cha kwanza mpaka cha pili, wakianzisha shule hii wale watamalizia kidato cha nne na cha tano na watakuwa mbele hivyo wale wataalam wa *TATAC* na *BAKITA* kutafsiri kwa lugha la Kiswahili vitabu vyote vya kufundishia. Nawaombe sana tujaribu mfano huo kama itashindikana ndipo wazo la lugha litakufa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri watu wana mawazo ya nyuma kwamba Kiingereza au Kifaransa ndio elimu. Mimi nashauri tuanzishe shule itakayotumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia darasa la kwanza mpaka chuo kikuu. Sasa hivi Chuma chetu Marehemu Magufuli, Rais wetu, alisema tu historia la kwanza mpaka chuo kikuu Kiswahili, asubuhi tumefanya hivyo mbona hawakukataa? Leo tunafundisha historia darasa la kwanza mpaka chuo kikuu kwa kutumia Kiswahili mbona imewezezana, kwa nini masomo mengine ishindikane, tena masomo sasa yamepungua yamebakia machache imebakia historia na kiswahili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako linaongea Kiswahili, Serikali inatumia Kiswahili, Mahakama inatumia Kiswahili, mnawachanganya watu, hao waliosoma Kiingereza wanatumiae Kiswahili huku Mahamani au Serikalini, kumekuwa na mambo ambayo hayaeleweki. Naomba sana Kiswahili kipewe umuhimu na mimi hili kama Mheshimiwa Rais anasikia aliingilie kati, kabisa kabisa. Nashauri hili liamuliwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la *VETA*. Waajiri wanachangia Mfuko wa Elimu ya Ujuzi kuititia tozo ya *SDL* kwa asilimia 4 lakini fedha zile haziendi *VETA* zote. Sababu kubwa ilijulikana siku za nyuma kwamba fedha zilikuwa hazitoshi ndipo Mheshimiwa Kikwete akahamishia *VETA* Wizara ya Elimu ili ipatikane fedha ya kwenda Bodi ya Mikopo na ndivyo ilivyo sasa. Sasa hivi mantiki hiyo haipo

kwa sababu fedha zote zinakwenda Akaunti ya Pamoja ya Hazina. Kwa hiyo, ile mantiki kwamba fedha za *SDL* ziende Wizara ya Elimu haipo tena. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *VETA* maana yake ni kazi ndiyo maana sisi waajiri tunachangia. Tunachangia fedha zinapatikana lakini sasa *VETA* badala ya kusimamiwa na Wizara ya Kazi na Ajira ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu, chini ya Mheshimiwa Mama Jenista Mhagama sasa anasimamia Waziri wa Elimu, ni vitu tofauti. Sisi huku tunashangaa sana hii Serikali vipi? Mbona sasa ajira inasimamiwa na Wizara ya Elimu na wakati Wizara ya Ajira ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaombeni sana, waajiri huku wanashangaa. Hatukatai kuchangia na tunawashukuru sana Serikali tulikuwa tunachangia asilimia 6 mpaka imefika asilimia nne tunaomba sasa hii *VETA* irudi kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye ndiye anayesimamia ajira na kazi na ndiyo kuna mikataba ya kazi, tunataka wafanyakazi wapate ujuzi. Sasa tunasimamiwa na Wizara ya Elimu siyo shule ile; kile ni Chuo cha Ufundji Stadi ya wafanyakazi na ndiyo maana sehemu kubwa ya fedha yake inatoka kwa sisi waajiri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu na mchango huo naomba safari hii ufanyiwe kazi. Naunga mkono hoja. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, humu ndani kuna mawazo mazuri sana ila napata picha Serikali kama italazimika kufanya kazi kila wazo la Mbunge mmoja, mtihani!

Tunaendelea na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, Mheshimiwa Martha Gwau ajiandae.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru, sambamba na hilo nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema na Utukufu kwa kutujaalia uzima na uhai. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mwezi Mtukufu wa Ramadhan niwapongeze Watanzania na Waislam wote ulimwenguni kwa kukaribia kumaliza mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan. Tunawataktakia kila la kheri na mafanikio makubwa kuelekea kwenye Eid El-fitri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeza wizara kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya katika kuboresha suala zima la elimu yetu ya Tanzania. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kila bajeti lazima watenge mafungu kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu pamoja na kutoa nafasi za ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba miundombinu imeboreshwa lakini kuna changamoto nyingi katika miundombinu hii ikiwepo suala zima la maabara, madarasa, vyoo vya walimu, vyoo vya wanafunzi na miundombinu mingine mbalimbali na hasa nyumba za walimu. Changamoto hizi haina maana kwamba hakuna kilichofanyika kuna mambo mengi na makubwa yamefanyika lakini hakuna mambo utakayoweza kuyamaliza kwa wakati mmoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ni msingi wa kila kitu katika maisha ya mwanadamu. Mwanadamu asipokuwa na elimu kwa kweli anakuwa yupo nyuma. Nikirejea kwa Nabii wetu Muhammad (S.A.W) alipopewa Utume, alisema mimi siwezi kusoma. Mwenyezi Mungu akamwambia usiwe na wasiwasi kwa sababu alipewa ule Utume ili awaongoze Waislam au wafuasi wake. Mwenyezi Mungu akamteremshia Sura inaitwa *Iqra bismi rab bikal lazee khalaq kwamba nenda kasome na alipomwambia asome hakumwambia asome kitu kimoja, alimwambia soma mpaka China. Leo China ni nchi inayoongoza kwa sayansi na teknolojia katika ulimwengu huu wa leo.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nini mantiki ya kuyasema haya. Tunaboresha elimu yetu kama Nabii Muhammad asingekuwa na walimu wa kumfundisha asingeweza kupata mafanikio makubwa. Sasa kwa mukhtadha huu nataka

nichangie kuhusu udhibiti wa elimu na upungufu wa walimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukianzia kwenye suala la walimu. Tunampongeza Mheshimiwa Waziri wetu Profesa Ndalichako pamoja na timu yake ya wataalam na wametuambia kwamba kuna mkakati madhubuti wa kuongeza walimu katika nchi yetu ya Tanzania yaani kutoa vibali kwa ajili ya ajira na vibali 6,000 vitatolewa. Sasa vibali 6,000 vikitolewa maana yake ni nini? Tuna walimu 6,000, tuna halmashauri 185, kwa uwiano ina maana kila halmashauri itapata walimu 32.43. Walimu hawa kwa kweli ni wachache sana ukilinganisha na uhaba wa walimu tuliokuwa nao. Ushauri wangu hapa ni nini? Ni lazima tuongeze walimu wengi zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada kuyasema hayo, nikubaliane na Kamati yangu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusiana na changamoto zilizopo. Niongelee Udhibiti wa Ubora. Hiki chombo ni muhimu sana tena sana ni sawasawa na Taasisi ya CAG. CAG bila kuwepo ina maana kwamba upungufu mwangi uliojitokeza katika maeneo mbalimbali usingeweza kuonekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu kazi yake ni kuandaa somo na kulifundisha. Lazima awe na *Scheme of Work* na *Lesson Plan*. Akishafundisha atajitathmini yeye mwenyewe. Sasa pamoja na kujitathmini yeye mwenyewe, hatutaweza kuboresha elimu kama hakutakuwa na wadhibiti ubora ambao watakuwa wanapita shule nydingi mbalimbali hapa nchini kuona je, alichokiandika huyu mwalimu na jioni akakitathmini ni sahihi? Maana huwezi kuandika kitabu ukakihariri wewe mwenyewe na ukahariri mara ya kwanza, ya pili na ya tatu. Kwa hiyo, mwalimu huyu anatakiwa awe na hiki chombo ili ajione kile alichokifanya ni sahihi au siyo sahihi? Kiko sawa au hakiko sawa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mdhibiti ubora ili aweze kufanya kazi yake vizuri zaidi ni lazima awe na vitendea kazi. Awe na bajeti inayojitosheleza. Akiwa na bajeti hiyo,

ina maana kwamba atafanya kazi yake kwa umakini zaidi na kuhakikisha kwamba shughuli inakwenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye uhaba wa walimu, kwa mfano, ukienda kwenye jimbo langu la Mchinga peke yake, tuna uhaba wa walimu chungu nzima. Ninachoshauri, walimu hawa wanapopangwa vile vile tuwapange walimu wa kike. Kwa mfano, shule yangu ya Nangaru haina mwalimu wa kike hata mmoja. Binti akiingia kwenye ule mfumo wake wa kwenda kule angani, au ndio imeingia sasa hivi, anaongea na nani? Kwa hiyo, tunapopanga tuhakikishe kwamba walimu wa kike wanapewa nafasi kwenye shule zetu nyingi zilizopo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenda angani, maana yake kuwa katika kipindi cha hedhi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunisikiliza. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau na Mheshimiwa Alfred James Kimea ajiandae.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nachukua nafasi hii nikushukuru sana kwa kunipa hii nafasi. Kipekee namshukuru sana Profesa pamoja na timu yake ya Wizara ya Elimu kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo naenda kujikita kwenye mfumo wa elimu. Nimefanya uchambuzi wa mfumo wa elimu na nimejikita kwenye zaidi ya nchi 15 ambazo nimefanya uchambuzi. Nimepitia mfumo wa elimu wa Tanzania, Japan, America, UK, Kenya, China na vile vile nimepitia mfumo wa elimu wa Zanzibar. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hoja takriban nne ambazo ningependa kuziwasilisha. Baada ya kupitia mifumo

yote hii ya elimu, hoja ya kwanza niliyogundua inaleta utofauti kati ya elimu yetu na elimu nyingine duniani ni suala la muda wa kuanza Darasa la Kwanza na pili suala la umri wa kuanza darasa la kwanza. Vile vile ni aina ya elimu ambayo tunaitoa katika ngazi ya vyuo vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ambayo nimeigundua baada ya kupitia mifumo mbalimbali ya elimu duniani ikiwepo ya Zanzibar na ya Tanzania, kuona ni *stage gani ambayo elimu yetu inatakiwa iwe academic*, lakini ni *stage gani ambayo elimu yetu inatakiwa iwe technical* na ni *stage gani ambayo tunahitaji kuwa na mixture ya technical na academic?* (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tatu ambayo nimepitia nikagundua ni suala la miundo ya mitaala. Katika miundo ya mitaala nimegundua vitu viwili; ya kwanza, ukipitia mitaala yetu kuna tatizo kubwa sana la masaa ya kukaa darasani na vile vile masaa ya kufanya *practical, (field work)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nimeangalia mfumo wa *assessment*. Katika mfumo huu nilichojifunza, hususan mfumo wetu wa Tanzania, unawaandaa vijana kuwa na *exam fearambayo* ni mbaya sana. Katika hili wasiwasi wangu uliopo ni kwamba tumeweka uzito mkubwa sana kwenye mitihani. Unakuta mitihani ya mwisho ina takriban asilimia 70 lakini yale mazoezi ambayo yanaenda kumjengea uwezo yana asilimia 30. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya mwisho ni hoja ambayo Waziri wa Elimu alisema kwamba wanakuja na mfumo wa *ku-review* sera yetu ya elimu ya Taifa, lakini vile vile kupitia mitaala yetu ya Elimu ya Taifa. Hoja yangu ni kwamba wakati Wizara inajipanga kwenda kufanya mapitio ya hii sera, nadhani ni muda muafaka sasa wa kujikita kikamilifu kuhakikisha kwamba tunakuwa na *comprehensive review* ya sera. Tuwe na muda wa kutosha katika *ku-review and then tuje tujikite* katika *ku-review* mitaala. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yangu ni kwamba tunahitaji kuwa na sera ambayo itakuja ku-*inform* hiyo *curriculum* ambayo tunaitaka, lakini tunahitaji kuwa na sera ambayo itakuwa *customized kulingana* na *case studies* mbalimbali tulizokutana nazo katika nchi mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali baada ya kutoa hoja zangu hizo takriban tano, la kwanza, kama nilivyotangulia kusema, naomba nimshauri Waziri kuwa suala la mapitio ya Sera ya Elimu ni suala la msingi sana. Naomba tunavyopitia Sera ya Elimu ya Taifa, tufanye *harmonization* na wenzetu wa Zanzibar. Zanzibar elimu ya msingi wanaenda miaka sita, lakini tuna *labour mobility* ya kutoka Zanzibar kuja Bara, Bara kwenda Zanzibar. Ni muda muafaka sasa tufanye *harmonization* ya hii mifumo yetu ya elimu ili kuhakikisha kwamba tunapokuwa na wenzetu wa Zanzibar tunaongea lugha moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ilifanyie kazi. Tunahitaji kuwa na mfumo mmoja wa elimu kwa sababu Bara na Zanzibar ni nchi moja, nasi hatuna *restrictions* zozote kwenye masuala ya elimu. Kwa hiyo, hilo naomba tulifanyie kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni suala la kuondoa ile tunaita *exam fear*. Katika kuondoa *exam fear* mimi nina hoja ifuatayo: Nimefanya kazi vyuo vikuu. Nimefundisha Chuo Kikuu cha Dodoma muda mrefu na pia nimefundisha Chuo cha Mipango muda mrefu. Kitu nilicho jifunza na nimekisema, nadhani kuna tatizo kwenye *curriculum* zetu. Tumeweka *weight* kubwa sana kwenye mitihani ya mwisho ambayo inatengeneza *exam fear*. Mwanafunzi anahangaika ili aweze kupata A na B, badala ahangaike kupata *competency*. Nataka kushauri kwamba katika hili naomba sasa unapopitia mitaala na sera, punguza *weight* ya mitihani, peleka *weight* kwenye *practicals*, vijana tuwa-expose kwenye mazingira ya kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne, naishauri Serikali tuanzishe kitu kinaitwa *integrated education system*. Tuje na

*combination ya academic na technical.* Wabunge wengi wameelezea. Mheshimiwa Waziri wewe unafahamu, tumesoma huko nyuma kwenye shule ambapo tulikuwa tunafundishwa sayansikimu, elimu ya kilimo na vitu vingine, lakini ile elimu ilikufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapotaka kuandaa vijana waweze kujitegemea, ni muda muafaka sasa kuhakikisha kwamba tuna-*impart* hizi *competences* kuanzia huko chini shule ya msingi, sekondari na ile inawajengea *palatability* ya kupenda, kwamba baadaye niende nikasomee mambo ya kilimo, baadaye nikasomee ufundi na kadhalika. Huwezi kujenga *palatability* ya mtu akiwa *level* ya juu, unataka aende akasomee ufundi VETA. Tunahitaji ku-*instill*/kuanzia chini shule za msingi na sekondari ili wale vijana anapotoka pale anasema mimi nataka niwe fundi wa bomba.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Kuna taarifa, sijajua inatoka wapi? Mheshimiwa Mwita Getere.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, hapa. Nilitaka nimpe msemaji hapa...

**NAIBU SPIKA:** Ngoja ngoja. Kulikuwa na taarifa kutoka pale, ndiye niliyemwita. Kwa hiyo, wewe subiri kidogo.

Mheshimiwa Mwita Getere.

## TAARIFA

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nataka kumpa taarifa Mheshimiwa anayeongea kwamba rushwa siyo lazima iwe kwenye pesa peke yake. *Corruption of mind* ni jambo kubwa sana katika nchi za Kiafrika na hasa Tanzania. Kuna haja gani ya kutomwekea mtoto maarifa ya kufundishwa namna ya kufuga kuku, namna ya kufuga ng'ombe, namna ya kulima, ukamshindilia

ma-pai, ma-triangle na mambo mengi ambayo watoto wengi wanaotoka *primary* siyo kwamba wote wanaenda sekondari, wengi wanabaki vijijiini. Wanaobaki vijijiini wanabaki na nini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Getere, tafadhalii naomba ukae kidogo. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, taarifa tunazozitoa inabidi ziendane na Kanuni zetu. Mbunge anayeruhusiwa kusema kuhusu taarifa ni pale ambapo Mbunge mwenzake halafu kuna jambo anataka kumpa taarifa iliyo sahihi. Pengine kile anachokisema kimekaa namna fulani hivi. Sasa nimeona Wabunge wanasimama kusema taarifa, wakati anataka kuchangia yeye wazo lake.

Sasa hiyo ni kinyume na kanuni zetu, ndiyo maana huwa kuna nafasi ya kuchangia. Usiwe na wazo lako unataka kumpa mwenzako ili na yeye alifanye wazo lake, hapana. Unampa taarifa kwenye kile kile anachokizungumza.

Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, taarifa kutoka kwa Mheshimiwa...

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Hamna Taarifa juu ya taarifa. Kwa hiyo, uwe unashubiri kidogo, tutaenda vizuri tu, hamna shida.

Mheshimiwa Dkt. Chaya unapokea taarifa ya Mheshimiwa Getere?

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Napokea Taarifa ya Mheshimiwa Mbunge na nadhani alikuwa anaunga mkono hoja na mawazo ambayo nilikuwa nayatoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho ningependa kuishauri Serikali ni upande wa vyuo vikuu.

**NAIBU SPIKA:** Kuna taarifa nyingine. Sasa kwa utaratibu kwa sababu tunajifunza, akishazungumza mmoja akitoa taarifa, lazima mzungumzaji azungumze ndiyo mwingine anaomba tena taarifa. Kwa hiyo, kwa sasa kwa sababu hilo tulikuwa hatujalielewa vizuri, nitakupa nafasi Mheshimiwa Saashisha, lakini kwa kawaida ukikaa chini namna hiyo, akishasimama kuzungumza akaongea, unaomba upya taarifa.

Mheshimiwa Saashisha.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ahsante pia kwa mwongozo mzuri. Nataka kumpa msemaji taarifa kwamba hapo awali kabla ya mwaka 1919 Wizara ya Elimu ilikuwa na mfumo rasmi kabisa wa shule za msingi za ufundi na kwetu kule Hai tulikuwa na shule tano zenyе muundo huo. Yaani watoto wakiwa shule ya msingi walikuwa wanafundishwa pia masomo ya ufundi na kulikuwa na walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka ninavyozungumza sasa hivi, shule ya msingi ya ufundi Mshara kuna walimu ambao waliandaliwa kwa ajili ya mitaala hii kufundisha rasmi masomo ya ufundi. Tatizo ni kwamba shule hizi zimeachwa hazijaendelezwa. Kwa hiyo, nampa taarifa kwamba kulikuwa na mfumo huu, ila umelala. (*Kicheko/Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawakumbusha kwenye vishkwambi vyenu zimo Kanuni mle. Tuzipitie vizuri. Huko tunakoelekea kwenye hili Bunge ni mwisho mwisho wa kujifunza Kanuni. Baadaye itakuwa ni mtu kaa chini, soga kidogo, futa ulichosema. Sasa hivi tunaenda taratibu.

Mheshimiwa Dkt. Chaya malizia mchango wako.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali vile vile taarifa ya Mheshimiwa Mbunge na bado naendelea kuishauri Serikali kwamba tunahitaji kuhuishwa

mitaala yetu hususan katika ngazi ya shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho upande wa vyuo vikuu. Kwa uzoefu wangu ambao nimekaa kwenye vyuo vikuu, unakuta kwa mfano wale wanaosoma *certificate, diploma*, na *degree tuna wa-subject* kwenye kufanya *research*. Mwanafunzi gani wa *certificate* anaweza kufanya *research* ikatumika katika maisha yetu? Mwanafunzi gani katika *level* ya *diploma* anaweza akafanya *research* ikatumika katika maisha yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kushauri, Wizara ya Elimu, mje na mfumo unaoitwa *capstone project system*; huu mfumo unaweza ukatumika kwa ngazi za chini ambao unawajengea uwezo wale watu, tunawa-expose kwenye mazingira ya kazi, wanakuja na ubunifu, *innovations*. Unaweza ukamchukua mtu ukampeleka kwa mfano *TANESCO*, anaenda kubuni mradi fulani na ile inakuwa na *weight* kubwa kama niliviotangulia kusema huko. Badala ya kuweka *weight* kubwa kwenye mitihani tunatengeneza *fear of exams*. Tupeleke *weight* kubwa kwenye hizi *capstone projects* ambazo zitasaidia kuwajengea *competences* na *skills*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, namwomba Waziri, katika Jimbo langu la Manyoni Mashariki sina Chuo cha VETA na nina vijana wengi sana waliomaliza sekondari wanahitaji kuwa na Chuo cha VETA.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nikawa namwangalia Mheshimiwa Almas Maige kama alikuwa anayafulilia hayo maneno ya Kiingereza yaliyokuwa yanatumika na kama anayo tafsiri yake.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 168 inaeleza kuhusu lugha rasmi ya Bunge. Lugha rasmi ya Bunge.

Ukizingumza Kiswahili unazungumza Kiswahili, ukichagua kuzungumza Kiingereza unazungumza Kiingereza. Unaruhusiwa tu kuchanganya lugha pale ambapo unachukua nukuu ya lugha hiyo na unataka kutumia. Kwa hiyo, Kanuni zetu zinatutaka tuchague lugha gani tunataka kutumia ili Taarifa Rasmi za Bunge ziwe vizuri.

Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea na Mheshimiwa Ester Edwin Maleko ajiandae.

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii uliyonipa nami niweze kuchangia Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwanza naomba niipongeze sana Serikali kwa kuja na Mpango huu wa Elimu bila Malipo. Naomba nipongeze sana kwa sababu Mpango huu umesaldla vijana wetu wengi, watoto wetu wengi kuweza kumaliza Kidato cha Nne tofauti na awali ilivyokuwa elimu yenye malipo. Kwa hiyo, kwa hili kwa kweli naomba niipongeze sana Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine naomba nijikite sana kwenye mitaala yetu au mtaala wetu uliopo kwa sasa hivi, naomba tuufanyie marekebisho au maboresho ili uendane na dunia inavyotaka au mahitaji ya dunia sasa hivi yanavyotaka, wanafunzi wawe na nini au wahitimu wawe na nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tujikite sana na kuwafundisha hawa watoto ubunifu na *skills* ili wakimaliza hapo wajajiri na waweze kuajiriwa. Ni tofauti na sasa hivi ambapo wakimaliza wengi wanajikita sana kusubiri ajira na hizo ajira hazipatikani kwa urahisi na siyo nydingi za kutosheleza. Katika hilo, nina ushauri wa vitu vitatu kwenye kuboresha mitaala yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza, tunganeanzisha somo la *technical subject* katika elimu ya msingi mpaka sekondari. Kwa nini nasema hivyo? Hawa wanafunzi wanapomaliza *Form Four* kuna makundi matatu

yanapatikana baada ya kuwa wamehitimu. Kuna kundi la kwanza watakwenda *Form Five*; kuna kundi la pili watakaokuwa wazazi wao wanaweza kuwalipia shule za *VETA* na ufundi na kadhalika; na kundi la tatu ambalo hilo halitaenda *VETA*, halitaenda *Form Five*; wanafanya nini na ndio kundi kubwa kuliko haya mawili niliyoyataja mwanzoni?

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwajengea uwezo kutoka *primary* wakamaliza *Form Four* na *skills* za kutosha, wakitoka hapo wataweza kwenda kwenye Halmashauri zetu, wakapata mikopo wakaweza kujajiri, wakaunda vikundi, wakakopesheka, wakajajiri na tukasaidia kutatua tatizo la ajira. Tofauti na sasa akimaliza *Form Four* anabaki nyumbani. Sasa atafanya nini na wakati tumempa elimu bure? Kwa hiyo, akimaliza na ujuzi itamsababisha yeye kujajiri mwenyewe na kukopesheka kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *program* ya pili tungeanzisha *sports and games* katika shule zetu ambapo awali zilikuwepo na tukapata wachezaji na watu wazuri tu, lakini naona zimefifia kwa muda uliopita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, michezo inaibua vipaji shulen, inaibua wachezaji bora, wanamichezo bora kutoka utotoni na kutoka umri mdogo. Hatuwezi kusema mtu akienda kwenye *degree* ndio anaweza akawa mchezaji mzuri, hapana. Kuanzia *level* ya *primary* mpaka hapo *Form Four* atakuwa mchezaji mzuri, ndio tutakuwa na wachezaji wazuri. Kwa mfano, wachezaji wa nje kama akina Morisson, Chama, nasi tutapata wa kwetu hapa Tanzania. Nadhani wana-Simba wenzangu watakuwa wamenielewa. Kwa hiyo, tuanzishe hiso *sports* ambazo zitawasaidia watoto wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, tuanzishe *environmental subjects*. Nina maana gani hapa? Tuna bahati ya kuwa na kanda tofauti tofauti na katika kila kanda kuna kitu wanajivunia. Kuna kanda wanafanya uvuvi, kuna kanda wanafanya kilimo, kuna kanda madini, kuna kanda wanafanya uvuvi na ufugaji na kadhalika. Tutakapowapa

wanafunzi wetu mafunzo ya *environmental studies*, ataamua, mimi nataka kuwa mkulima. Atakuwa na mwalimu mkulima anamfundisha. Kuanzia *level* ya *primary* mpaka hiyo ya sekondari. Akitoka hapo anaweza akajajiri mwenyewe kwa kufuga, kulima au kuchunga. Hayo tunamfundisha kutokana na mazingira alipo. Watu wa kanda ya kati tunajua tunafanya nini, watu wa kanda ya kaskazini na kadhalika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya tukiyaongeza yatatusababishia vijana wetu wanaomaliza *form four* kwa kuwapa hii elimu bila malipo, lile kundi la tatu lililobakia, litapata kitu cha kufanya mtaani, badala ya sasa hivi wakimaliza wanakuwa wamekaa bila kazi yoyote, lakini hili lote itatusaidia sisi kama Serikali kupunguza suala la ajira kwa sababu, tutawakopesha kwenye halmashauri zetu na watajajiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la mwisho, naomba Serikali iongeze bajeti kwenye Wizara ya Elimu kwa sababu, Wizara ya Elimu inapaswa kuwapa Walimu mafunzo. Nimeongelea upande wa wanafunzi, lakini watoa huduma je, ambao ni Walimu. Naomba wapatiwe semina mbalimbali hata mara mbili kwa mwaka kwa sababu, unapompa Mwalimu semina ni kama motisha. Semina yenye hata iwe ya malipo, akipata semina yake anapata malipo yake inamsaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine motisha, kwamba, wanapopata zile semina basi kunakuwa na shule iliyofanya vizuri inapewa zawadi, kuna Mwalimu bora aliyefanya vizuri anapewa zawadi. Hii una-*motivate* Walimu wengine waliobakia au shule nyingine zilizobakia na wao kufanya vizuri zaidi, ili wapate hizo zawadi na *recognition*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na uzuri zawadi sio lazima pesa. Mtu atakapopata *certificate* kutoka kwa Mkuu wa Mkoa au kwa Mkurugenzi wa Halmashauri anajisikia yuko *well valuable*, yaani anajisikia kwamba, ameheshimika na mchango wake umechukuliwa. Hii itasaidia Walimu wetu kuwa *motivated* na wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine pia ni *reviews*. Unapokaa na Walimu wa halmashauri moja wakasema kwa nini mimi nafaulisha zaidi kuliko wewe? Wata-exchange ideas, watapeana mbinu na mikakati mbadala ambayo itasababisha na yeye akirudi afanye vizuri kwenye shule yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndio ulikuwa mchango wangu kwa siku ya leo. Nashukuru sana kwa nafasi hii na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Edwin Maleko na Mheshimiwa Kilumbe Shaban Ng'enda ajiandae.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nichangie kwenye hii bajeti ya Wizara ya Elimu. Nina mambo machache sana ya kuchangia kwenye Wizara hii na napenda nijikite hasa kwenye elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya changamoto ambazo zimetolewa imeonekana tuna upungufu wa Wakufunzi au Wahadhiri katika vyuo vyetu, lakini tuangalie ni nini kinasababisha kitu hiki? Kama tunafahamu vyuo vyetu vina *tendency* ya ku-retain wanafunzi waliofanya vizuri wabaki kufundisha wanafnzi wetu, lakini pia kufanya *research* ambazo zinasaidia kutatua changamoto zinazopatikana kwenye jamii zetu. Ili mwanafunzi awe *retained* pale chuoni ni lazima wawe ni wanafunzi wanaofanya vizuri, *First Classes* ndio zinabakizwa vyuoni. *First Class* hizi hazihitajiki chuoni tu peke yake, pia mashirika mbalimbali yanatafuta watu hawa. Kwa hiyo, maslahi ya wanaobakishwa pale chuoni ndio yanayosababisha aidha mwanafunzi huyo au wanafunzi hao wazuri wakubali kubaki chuoni au waende sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa niishauri Serikali, ione namna ya kuboresha maslahi kwa wataalam wetu hawa ambao wana kazi kubwa ya kufanya *research*, wana kazi kubwa ya kufundisha wanafunzi wetu vyuoni, ili waweze

kuwa na morali ya kubaki vyuoni kuliko kwenda kuajiriwa sehemu nyingine. Huo ndio mchango wangu wa kwanza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, naongea hili kwa kuwa nina uzoefu na nilikuwa mionganini mwa watu hao, labda kwanza naomba ku-*declare interest*. Nadhani unafahamu ugumu wa kupanda madaraja kwenye vyuo vyetu, tunaajiriwa mara nyingi kutoka vyuoni kama *Tutorial Assistant*, baada ya kupata *Masters* tunaenda kuwa *Assistant Lecturer* na baada ya hapo tunakuwa ma-*lecturer* aidha kwa ku-*publish* baada ya kukaa miaka mitatu au kupata *Ph.D.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, watu hawa wanaweza wa-*qualify*. Mtu amehangaika sana aka-*publish* au kapata *Ph.D* anapanda cheo kwa kuandikiwa tu barua umepanda, lakini wanasema tunasubiri Serikali itoe idhini ya kupandishwa vyeo ili mpewe maslahi yenu. Hii inakatisha moyo wakufunzi wetu, inasababisha watu waondoke vyuoni; tunasema Wahadhiri ni wachache, lakini Serikali ndio inasababisha. Kwa kweli, hii ni sehemu nyeti sana, tunaomba maslahi ya watu hao yaangaliwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano ni wa kwangu mimi mwenyewe, kabla ya kwenda kufanya *PhD* nili-*publish* ili niweze kupanda kuwa *Lecturer* kabla ya kwenda *PhD*. Nilipewa tu barua ya pongezi kwamba, nime-*qualify* kuwa *Lecturer*, lakini hadi leo sijawahi kupata mshahara wa mtu kama *Lecturer*. Kwa hiyo, nasema wapo wenzangu wengi huko vyuoni wana changamoto kama ya kwangu, naomba tuangaliwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, tunajua mazingira ya kusoma hapa Tanzania. Najua unaweza kuwa unafahamu watu ambao wamefanya *Ph.D* zao hapa Tanzania, kuna changamoto kubwa, lakini changamoto hii inasababishwa na maslahi mabovu ya wasimamizi wa *Ph.D* zile. *Lecturer* hana kipato kizuri, inasababisha aanze kutafuta shughuli nyingine za kumuingizia kipato. Utakuta *lecturer* na fundisha *part time*

vyuo vinne, utakuta *lecturer* anaafuga kuku ili kujiongezea kipato, anaacha kusimamia *dissertation* za wanafunzi. Kwa hiyo, kama tunataka kupandisha elimu ya vyuo vyetu, basi tuangalie maslahi ya watu hawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hilo tu, pia vyuo vyetu havina *fund*kwa ajili ya kuendesha *research*. Sio *research* tu, ili uweze kutoa watu wa *masters* na *PhD* lazima vyuo viwe *vime-subscribe* kwenye *journal* nzuri za kimataifa, viwe vina *software* kwa ajili ya *data analysis*, lakini vyuo havipatiwi fedha hizi. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ivipatie fedha vyuo vyetu ili elimu iweze kukua, hasa *research* ambazo zinahitajika kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, cha mwisho, naomba Wizara ya Elimu inisikilize kwa makini; kulikuwa kuna *institute* hapa Tanzania inaitwa *African Institute for Mathematical Science*. *Institute* hii ipo *South Afrika*, Ghana, Tanzania na Rwanda, lakini *institute* hii inafadhiliwa na wafadhili (*Donors*) kwa asilimia kubwa na nchi ambayo hii *institute* ipo nchi hiyo inatoa kiasi kidogo kwa ajili ya uendeshaji wa chuo hicho, lakini Serikali yetu imeshindwa kulipia fedha kidogo kwa ajili ya kuendesha *institute* hiyo na *institute* hiyo imekufa. Namwomba Waziri kwenye majumuisho yake aje aniambie kimetokea kitu gani kwa *institute* hii mpaka kufa?

Mheshimiwa Naibu Spika, *institute* hii inasaidia *researcher* wetu, *institute* hii inasaidia wataalam wetu kuweza kufundishwa jinsi ya *ku-apply mathematics* kwenye kutatua matatizo kwenye jamii zetu. Imefanya vizuri sana Rwanda na inaendelea kufanya vizuri, imefanya vizuri Ghana na inaendelea kufanya vizuri, Tanzania kuna nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Huo ndio ulikuwa mchango wangu. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, atafuatiwa na Mheshimiwa Kilumbe Shaban Ng'enda na Mheshimiwa Jacquiline Ngonyani Msongozi ajiandae.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa fursa hii ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Elimu. Kwanza nianze kwa kutoa pongezi nyingi sana kwa utekelezaji wa elimu bila malipo kwa sababu kwa sasa wanafunzi ambao wanahitimu wameongezeka na wataendelea kuongezeka kwa kasi kubwa. Sasa ni vyema basi Serikali ijipange ni namna gani basi itaweza kukabili mahitaji haya makubwa ya miundombinu ambayo tayari imeanza kuellemewa. Wizara imeomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi trilioni 1.384 ambazo zina ongezeko la shilingi bilioni 42.4 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2020/2021, nawapongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha hizo matumizi ya kawaida ni bilioni 480.5 ambayo ni sawasawa na asilimia 34.7 na maendeleo ni bilioni 903.9 ambayo ni sawasawa na asilimia 65.3 tunawapongeza sana kwa uwiano huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kati ya fedha hizo fedha za maendeleo ni bilioni 403, lakini bilioni 500 zinakwenda kwenye mikopo ya elimu ya juu. Sidhani kama ni sahihi fedha za mafunzo au *training* kuitwa fedha za maendeleo maana matumizi yake ni ya kawaida na matumizi ya fedha za maendeleo hayaweki kwenda kuwekwa kwenye fedha ambazo tunasema zinapelekwa kwenye mikopo ya elimu ya juu. Kwenye mafungu mengine ya fedha za kugharamia mafunzo ziko *recurrent*, ndio maana fedha zisipotolewa zote kinacho-*suffer* ni ile miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, katika mwaka huu mpaka Machi, 2021 miradi sita tu kati ya miradi 33 ya mikakati ya maendeleo ndio imepata fedha, lakini hii mingine mpaka sasa haijapata. Miradi hiyo ni *EP4R* na *Equip T* haijapata chochote mpaka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, ni vyema basi zile fedha za mikopo ya elimu ya juu zipewe fungu lake tofauti ya kujitegemea ili zile fedha za miradi zisiweze kuguswa na ziende kwenye ile miradi, ili iweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo linguine, TAMISEMI tunaomba waboreshe ushirikiano kati yao na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ili waweze kushirikiana vyema kutoa huduma hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, sina uhakika sana kama Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wanajua mahitaji makubwa ambayo yanatokana na kuanzisha utekelezaji huu wa elimu bila malipo. Kwa sababu katika kipindi hiki cha miaka minne tutakuwa tunahitaji madawati 41,333; tutakuwa tunahitaji matundu ya vyoo 75,300; vitabu 18,000,825; na walimu 41,833; na fedha za ruzuku ya wanafunzi bilioni 1,882,000,500; ambayo hiyo ni sawa na triliioni 1.476 ili kuweza kukamilisha shughuli hii ya wanafunzi watakaoongezeka katika kipindi hicho cha miaka minne. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaomba ushirikiano bora kati ya TAMISEMI, watakaowasaidia kufuatilia miradi inayotekelzeza kwenye wilaya mbalimbali mfano VETA na vyuo vikuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kufikia hapo, huo ndio mchango wangu. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kilumbe Shaban Ng'enda, atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi. Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk ajiandae. Hayupo!

Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, atafuatiwa na Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk. Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima ajiandae.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, Naibu Spika, ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana nichangie katika Wizara hii hasa kwenye maeneo ya vyuo vikuu. Nataka niambie Wizara ya Elimu kwamba, kumekuwa na vyuo vikuu ambavyo vinaendeshwa na taasisi za dini nchini Tanzania, lakini taasisi hizi tayari zimeanza kukata tamaa na kwamba, vyuo hivyo sasa hivi vinalegalega, havifanyi vizuri, lakini ninachofahamu ni kwamba, Wizara ya Elimu ndio walezi wa vyuo hivi.

Kwa hiyo, ni vizuri sasa Wizara ikasimama katika kuhakikisha kwamba, hawa wanafanya vizuri kwa kuwasaidia resources mbalimbali ikiwemo pesa pamoja na watumishi ambaao wanatakiwa wafanye kazi kwenye taasisi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hizi taasisi nazo pia zinafanya vizuri katika kuongeza elimu katika nchi yetu na zimekuwa zikifanya vizuri sana. Kwa hiyo, Wizara islimame katika eneo lake na kuhakikisha kwamba, wanawawezesha ili waweze kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa sana imeonesha kwamba, vyuo hivi na taasisi hizi zinaendelea kufa hasa ninapozungumzia chuo kimoja pale Mkoa wa Mtwara. Nacho kimekufa, chuo hakifanyi vizuri na Wizara wapo, wamekaa wanaangalia tu. Pia kuna Chuo cha AJUCO, Songea Mjini, chuo kile kimekufa hakiendelezwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikifikiria tu ni kwa nini Mheshimiwa Profesa Ndalichako anajisikiaje Nyanda za Juu Kusini kule vyuo vyetu vinakufa, yeye ni mama wa watoto yuko hapo na wala hatusaidii kuhakikisha kwamba, hawa wanaendelea kupata elimu na vyuo vile vinaendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kipo Chuo cha St. Joseph Songea Mjini nacho pia hakifanyi kazi. Jana nilimtumia memo Mheshimiwa Profesa Ndalichako, nikasema naomba unieleze hivi vyuo vitafunguliwa lini? AJUCO ya Songea na Chuo cha St. Joseph cha Songea ni lini vitafunguliwa hivi vyuo? Maelezo aliyonipa kwa kweli, hayakuniridhisha na

nasema Mheshimiwa Profesa Ndalichako leo hii wakati ana-*wind up*, naomba aje na majibu mazuri ya msingi ambayo *yatani-stimulate* niache kushika shilingi yake, vinginevyo nimpe taarifa kabisa kwamba, nakusudia kuzuia shilingi ya mshahara wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niseme kwamba, hawa *TCU* wako kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, vyuo hivi vinaendelea kufanya vizuri, lakini kazi wanayoifanya sasa ni kuzuia, kukataza vyuo visiendelee; hatuwezi kusaidia vyuo hivi viweze kufanya kazi endapo kama utaratibu utaendelea kuwa huu. Ni vizuri sasa Serikali isimame na *TCU* wafanye kazi yao ya kuwaelekeza na kuwasaidia, kuwashauri, ili vyuo hivi viweze kuendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu Ruvuma kumekuwa doro, hakuna chuo chochote kile cha Serikali ambacho kitaweza kusaidia zaidi ya *VETA*, hakuna chuo kingine ambacho kitaweza kusaidia na uhitaji ni mkubwa sana. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Profesa Ndalichako awe makini na awe *standby* kabisa kwamba, nitazuia shilingi ya mshahara wako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani sasa kijengwe chuo kikuu angalau kimoja katika Nyanda za Juu Kusini ambacho kitasaidia hasa katika Mkoa wa Ruvuma. Kijengwe chuo kimoja ambacho kitasaidia ambacho kiwe na program kama tatu hivi. Chuo kikuu hicho kwa sababu sisi katika Mkoa wa Ruvuma tunalima mazao mchanganyiko sana, kwa hiyo, nadhani kwamba, kuwe na program tatu katika chuo hicho kitakachoanzishwa ambazo ni *crop program*. *Crop program* itasaidia kuendeleza shughuli za uzalishaji kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyingine ni *Chemical Engineering*. Sisi tunalima kule korosho na kahawa, tulidhani sasa hii *chemical engineering* itasaidia hii *program* kuhakikisha kwamba, eneo lile linaendelea kustawi kupitia hizo *program*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuna Ziwa Nyasa. Ziwa hili limetulia tu halina mwendelezo wowote. Kwa hiyo, nadhani kwamba, kukiwa na program ya *fisheries* itasaidia sana kuwainua vijana wetu na watafanya uwekezaji kwenye ziwa ambalo linaonekana. Mheshimiwa Profesa Ndalichako ni mtani wangu, lakini leo mimi sina utani naye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesisitiza sana kwamba, Wizara isaidie hivi vyuo. Nakumbuka Awamu ya Tatu ya Mheshimiwa Benjamin William Mkapa ilisaidia chuo ambacho ni *University of Morogoro*, *University of Morogoro* walisaidiwa wao walikuwa na shida ya majengo, lakini Mheshimiwa Rais aliweza kutoa maelekezo wakapewa majengo ya *TANESCO* na yale majengo yaliwasaidia. Sasa ni kwa nini Mheshimiwa Profesa Ndalichako hasaidii vyuo vya Songea vile vilivyofungwa ili viweze kufunguliwa? Ana ajenda gani wakati Kusini sisi kule hatuna chuo chochote? Tunamwomba tafadhali sana, yaani kule Mkoa wetu umepooza, hakuna vijana wanaoendelea katika shughuli za kusoma kupitia vyuo vikuu.

Nakuomba sana, tafadhali sana, nilitaka kulia ila kwa sababu ni Mwezi Mtukufu, kwa hiyo nimeacha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni kwanini Mheshimiwa Ndalichako husaidii vyuo vya Songea vile vilivyofungwa ili viweze kufunguliwa? una agenda gani wakati kusini sisi kule hatuna chuo chochote tunakuomba tafadhali sana yaani kule Mkoa wetu umekuwa umepooza hakuna vijana wanaoendelea katika shughuli za kusoma kupitia vyuo vikuu. Ninakuomba sana tafadhali sana nilitaka kulia ila kwasababu Mwezi Mtukufu kwa hiyo nimeacha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Prof. Ndalichako naomba wasaidiwe hawa vyuo hivi vya taasisi za dini waweze kama kuna shinda ya majengo wapewe majengo lakini kama kuna shida ya fedha wapewe fedha, lakini pia kama kuna masuala ambayo yanahusiana na masuala la *management* nayo pia nimeambiwa kwamba ili chuo kiendelee lazima kuwe na *ma-professors* ina maana

Mheshimiwa Prof. Ndalichako wewe ulikuwa Mwalimu wa vyuo vikuu huna *ma-professors* utupelekee kule vyuo vile vifunguliwe.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja nakusudia kushika shilingi ya Mheshimiwa Prof. Ndalichako. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndalichako inabidi ye ye mwenyewe si profesa kwa hiyo inabidi aende kwenye hivi vyuo, ahsante sana. Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk atafuatiwa na Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima, Mheshimiwa Eric James Shigongo ajiandae.

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana niwapongeza sana viongozi wa Wizara hii Mama Mheshimiwa Prof. Ndalichako na mwenzake na hii ni Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia ambayo tunategemea sana kwamba mambo yake yangekwenda kwa Sayansi na Teknolojia na ninaamini wangeanza na walimu na kwasababu ni mwalimu naomba nianze na walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu ni Wizara muhimu sana katika nchi ye yote ndio tuliitegemea ilete mabadiliko yote ndani ya nchi kwasababu wao ndio wana *deal* na elimu na elimu ndio maendeleo. Lakini ninasikitika sana na walimu kwamba wamekekwa nyuma sana kwa hiyo ninaiomba hii Wizara na Serikali kwa ujumla waangalie walimu kwa jicho la huruma sana kwasababu mwalimu anafanya kazi nyingi sana akiwepo shule ana lea mwalimu, anafundisha, anatoa kazi, anazisimamia yote haya ingekuwa ni mtu mwingine mkubwa mkubwa basi yote haya angepangiwa *allowances* kwamba labda akisahihisha kuna *allowance* akitoa *homework* kuna *allowance* akitoa *home text* ana *allowance* lakini akitoa *termina test* ana *allowance* akitoa *examination* ana *allowance*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwasababu ni walimu bado halijafikiriwa jambo hili naomba sana walimu wafikiriwe sana kazi wanayoifanya ni ngumu mno. Nafikiria hata kuwaombea hawa kwamba wangkuwa na wao wanapewa afya, yaani huduma za Afya bure ingependeza sana, na ninaiomba sana Wizara ya Elimu iwatumie sana Walimu. Ninakumbuka mwaka 2009 kuna mwalimu ndio amegundua mchanga fulani pale uliokuwa unapelekwa Kenya kwamba ule ndio mchanga ambao una dhahabu, Mheshimiwa Dkt. Magufuli Hayati Mwenyezi Mungu amrehemu akhera alipo huko amekuja kuuzuia baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaamini sana kama tungewatumia walimu vizuri basi hata wanafunzi wa darasa la sita leo wangeweza kutusaidia sana katika tafiti mbalimbali hata ulinzi wa yale madini kwa mfano madini yanayoibila kule basi walimu wangeandaa wanafunzi hata wakienda kucheza mchezo fulani tu pale wakawa wamevaa nguo tofauti za wanafunzi basi wakagundua kuna madini yanaabiwa na nani anaiba, Watoto wangesema, lakini kwasababu bado walimu hatujawatumia vizuri naomba sana Wizara ya Elimu iangalie jambo hili..

Mheshimiwa Naibu Spika, ni juzi tu hapa wiki iliyopita amekuja mama mmoja alinieleza kwamba anatoka Arusha yule mama alilalamika sana kwamba wamezuiwa yale mahitaji yao yaani *increment* zao zimezuiwa sijui kupandishwa madaraja yamezuiwa kwa muda wa miaka sita. Anashukuru sasa kwamba wanakwenda kupandishwa madaraja ila wao wamestaifu wamestaifu mwaka jana mwezi Novemba sasa anahofu kwamba yale madaraja wao hayatawahu na ile *arrear* yao ya haya madaraja wanayotaka kupandishwa sijui itakuwaje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini yote haya ni kwasababu tulimchukulia mwalimu ni mfanyakazi tu peke yake. Kwa hiyo, ilivyokuja kwamba wafanyakazi wote zimezuiwa *increment* na mwalimu tukamzuia, kumbe mwalimu ni zaidi ya mfanyakazi sisi wote humu tumekuja humu kwasababu walimu wametutengeneza leo

tumekuwepo hapa kwasababu walimu wametengeneza *future* zetu lakini sisi tuliotengenezewa future hatuangali nani wametutengenezea *future* hizi. Kwa hiyo, naomba sana Wizara ya Elimu iwaangalie sana walimu sio vibaya walimu sasa kununuliwa hadi vile viatu nya kuingia shule sio tatizo hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamuomba Waziri wa Elimu aangalie pia suala la masomo haya kila unapofungua kwenye mtandao mtu anapotaka kuijunga na chuo anaambiwa awe na mfano awe na *credit* nne lakini *non-religious subject*. Nilikuwa ninamuomba Waziri afikirie kwamba sisi pamoja na uhai wetu wote duniani hapa ipo siku tutaondoka duniani, na kwasababu tutaondoka duniani kila mtu anategemea kwamba kuwe na watu nyuma watakaosema mwanga wa bwana uwashiwe kule akhera sijui kuyasema vizuri haya maneno lakini sisi tunaomba dua ziombwe hawa watakaotuombe dua ni nani ikiwa leo mwanafunzi anaambiwa somo lako hili la dini halitazingatiwa katika udahili wa vyuo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli hili somo la dini halitamsaidia kule anakokwenda kwamba atasoma *chemistry* lakini halitamwongezee halita mchupisha amepata A ya chemistry amepata A ya biology amepata A ya physics lakini ameshindwa kupata B nyingine amekuja kupata D ya *Bible knowledge* na *Islamic knowledge* si itamsaidia kuingia *advance*, atakwenda kusomea chemistry lakini hapa imemsaidia lakini *in-directly*kwamba huyu mtoto umemfanya asome dini kwa hiyo kesho atakuwa padri kesho kutwa atakuwa shekhe atakuwa mwalimu wa Madrasa kwasababu ya elimu ile ile. (*Makof*)

Mheshimiwa Niabu Spika, kwa hiyo sasa hivi mwanafunzi hasomi tena dini kwasababu anaona Serikali haizingatii hiyo *credit* yake. Kwa hiyo ninamuomba sana Waziri ninaiomba sana Serikali ifikirie jambo hili nijambo kubwa na kwasababu sisi Watanzania wote kila mtu ana dini yake ninamuomba sana aangalie sana juu ya kurudisha ile hadhi ya somo la dini katika udahili wa vyuo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamuomba pia Waziri afikirie namna ya kujenga uzalendo wa watanzania kwa kupitia Wizara hii ya Elimu leo watu wengi tumesoma lakini matatizo yameongezeka ukiangalia huku mara mtu anakwambia sijui nini kimeibiwa sijui hichi kimeibiwa tatizo nini, tatizo ni kwamba kila mtu hapendelei kwamba nchi ipate nini, anapendelea yeye mwenyewe apate nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mtu atakuwa na madaraka miaka mitano, sita, kumi yeye akiwa na madaraka ndani ya siku tano ni tajiri... (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa ahsante sana.

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, Naunga mkono hoja ninashukuru sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima, atafuatiwa na Mheshimiwa Eric James Shigongo Mheshimiwa Jeremiah Amsabi Mrimi, ajiandae.

**MHE. ASKOFU JASEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Kwanza nikupongeze jana kwenye futari ya *CRDB* ulipendeza sana na nikaona umeanza kuitwa Ukti, *keep it up* utafika mahali pazuri sana. Lakini watu wengi sana waliochangia nataka nipate nafasi ya kuchangia hii hoja ya Wizara ya Elimu watu wengi sana waliochangia wamezungumza kwa habari ya *curriculum* au mitaala. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mawazo ya watu wengi walikuwa wanachangia wakisema kwamba ni muhimu sana mitaala ya elimu hii kubadilishwa ili iwe *skill basic curriculum* na sikatai, lakini lipo jambo la muhimu sana ambalo ningependa ku-discuss it is a matter of national concern siyo jambo la tu Wizara ya Elimu peke yake lakini is a matter of national concern na hili jambo lina athiri Wizara ya Elimu directly as far less curriculum is concern.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba ninukuu mchangiaji wa jana aliyechangia anaitwa Mheshimiwa Nusrat Hanje alichangia jambo ambalo nanukuu alitoa kwenye Sera ya Elimu ya mwaka 2014 ambayo inasema kwamba lengo la elimu au *objective* ya elimu ni kumpa mtu maarifa, ustadi, umahiri, uwezo na mtazamo changa katika kuchangia maendeleo ya nchi. Hivyo ndivyo sera ya elimu ya mwaka 2014 inavyosema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaanza kuona kwamba *objective* ya elimu ni kumfanya mtu awe na maarifa awe na ustadi, awe mahiri, awe na uwezo na awe na mtazamo chanya katika kuchangia maendeleo ya nchi. Kwa hiyo, *objective* ya elimu ni maendeleo ya nchi sasa lipo jambo ambalo ni *serious* sana ambalo ningefikiri mtu ye yote msomi aliye kwenye Bunge hili anatakiwa aisaidie hii nchi na kizazi kijacho. Kama lengo la elimu ni kumsaldia anayepata elimu ni kuzalisha mtu ambaye ana uwezo wa kuchangia kwenye maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *then* maendeleo ya nchi ni nini, ni muhimu sana nchi hii iwe na maono ya miaka mingi kuhusiana na mambo yanayohusiana na Taifa hili. Niliwahi kuchangia nikasema *without vision people perish* pasipo maono watu kuangamia. Mataifa mengi sana yaliyoendelea yana *vision* ya nchi zao unakuta kwa mfano miaka kama 10 iliyopita Wamarekani walikuwa na *a hundred years of the new American* wa *Finland* walikuwa na *forty years of the Finland development* na nchi nydingine, lakini sisi nchi yetu inakuwa haina *vision* tulikuwa na Mpango wa Maendeleo wa Mkapa ambao unaisha mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa hivi tuna llani za Uchaguzi tu na mipango ya muda mfupi miaka mitano, mipango hiyo inaifanya nchi idumae sana kwanini nasema hivyo, nasema hivyo kwasababu panapokuwa na mpango wa muda mrefu kwa mfano Tanzania tukasema tuwe na mpango wa miaka 50 wa maendeleo na tuna kitu gani tunakiita maendeleo, tunaweza kusema kwa mfano maendeleo kwetu sisi kila mtu awe na maji safi na salama,

maendeleo kwetu sisi ndani ya miaka 50 kila nyumba ya mtu iwe na umeme, maendeleo sisi ndani ya miaka 50 asiwepo Mtanzania hata mmoja anayekaa kwenye nyumba ya majani.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo kwetu sisi asiwepo Mtanzania kijana mwenye uwezo wa kusoma shule akashindwa kwenda chuo kikuu ndani ya miaka 50, maendeleo kwetu sisi kila barabara iwe ya TARURA iwe barabara ya TANROADS iwe la lami, tukaya-*define* haya maendeleo kwamba kiongozi anayekuja kwenye power atutimizie hayo maendeleo ndani ya miaka 50 na tutaona ubora wa kiongozi ni kwa jinsi gani anayatimiza hayo maendeleo yetu kwa muda mfupi kuliko muda ambao tumejipangia sisi wenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye sera ya Elimu nitakuja kwasababu lengo langu ni kuongea sera ya elimu, lakini shinda inayotusumbua sasa hivi tunahitaji Rais mwenye maono ina maana sisi kama nchi hatuna maono. Kwa hiyo, Rais anapoingia madarakani anatimiza maono yake namna ambavyo yeye anatafsiri maendeleo tunajikuta tunaendelea lakini kwa namna ambavyo kiongozi ana-*passive* maendeleo, lakini kusema ukweli tusingehitaji Rais mwenye maono tungehitaji nchi yenyе maono ili Rais atakapoingia atimize maono ya nchi hayo ambayo sisi wenyewe tumejipangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa mfano kama tungkuwa na maono kwa mfano ndani ya miaka 50 tukasema Wizara ya Elimu tunasema ndani ya miaka 50 tutakuwa na *University* kila Wilaya, tukasema ndani ya miaka 50 tutakuwa na Hospitali ya Rufaa kila Wilaya kwa hiyo sasa elimu zote zingeanza kujipanga kuelekea hiyo miaka 50. Kwa hiyo, hata wanafunzi wanaosoma wangeiona *vision* ya nchi, *vision* ya nchi ni miaka 50 kwa hiyo ndani ya miaka 50 tutakuwa na *university* kila Wilaya kwa hiyo, kila mtu anayesoma shule angekuwa anajua maprofesa wanatakiwa ma-*tutor assistant* wanatakiwa, wasomi wanatakiwa kwa hiyo tungemsaidi mwanafunzi kuona mbali kwa sababu ameiona *vision* ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukisema kwa mfano kwenye miaka 50 kila Wilaya iwe na Hospitali ya Rufaa kwa hiyo anayekwenda shule angeona soko la madaktari lipo nisome madaktari soko la ma-nurse lipo nisome u-nurse anayetaka kuuza vifaa vya *medicine* angeona naye soko lipo, tungewasaidia hata wawekezaji wetu wakawekeza kwa uzuri zaidi kwasababu wanaiona *vision* ya nchi, lakini sasa hivi tunakuwa hatuna *vision* tunakuwa na vitu vya kukimbiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu kwenye Halmashauri yangu kulikuwa na maeneo hakuna madawati wanafunzi wanafaulu tunakimbia kusema tunataka madawati na mwaka kesho tutakimbia tunataka madawati na mwaka kesho kutwa tunataka madawati, kwani hatuna *statistics* za kujua kwamba mwaka huu *estimation* za ufaulu zitakuwa kiasi hiki tukaanda madawati, tunakosa *vision* nikwambie jambo moja Mheshimiwa Waziri kwenye shida yetu tusipoweza ku-handle kuwa na *vision* kubwa ya Taifa letu maeneo mengi sana tuta-stuck kuna uwekezaji ambao mtu akiwekeza *return* yake inakuja baadaye sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano ukisema mtu awekeze kwenye kujenga Hospitali ukimaanisha kwamba kutoka kwenye hospitali utapata madaktari kwa hiyo wale wanaosoma wanajua wanakwenda kusoma nitakapofika *form six* nitachakua *medicine* kwasababu soko la madaktari lipo anayesoma anasema mimi ninasoma *nursing* kwasababu madaktari wanatakiwa kila Wilaya soko la *nursing* lipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaofanya biashara ya vifaa vya hospitali wataingiza vifaa wanajua ndani ya miaka 50 soko la vifaa vya hospitali lipo. Kwa hiyo hata wale wawekezaji kwenye *industry* ya elimu wanawekeza wakijua soko lipo. Lakini sasa hivi unasikia wote tumekimbia kwenye gesi baada ya miaka mitatu minne anakuja mwengine gesi haipo, tayari watu wameshajenga hotel wameshajenga nyumba wameshajenga hivi wanakula hasara baadaye kwenye korosho tunapiga kona tena hatuko korosho baadaye kwenye kwenye dhahabu tunapiga kona hapo kwenye dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaza nchi hii kama inatakiwa iendelee lazima iwe na *vision* ya nchi ya muda mrefu ili kiongozi anayeingia ndani ya utawala atumikie *vision* ambayo wananchi wameiweka sio *vision* yake. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana ninaunga mkono hoja. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Eric James Shigongo atafuatiwa na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, nadhani tutamaliza na hao kama muda utabaki atamalizia Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninapenda niende moja kwa moja kwenye hoja kwasababu ya muda, lakini naomba tu kwanza kwa kusema kwamba ninatangaza mapema kabisa kabla ya wakati kwamba nitashika shilingi kwenye mshahara wa Waziri wakati utakapofika kwasababu ya suala zima la *RPL-Recognition of Prior Learning* ambayo Wizara ilifuta na hatimaye inawanyima watu ambao hawakupata nafasi ya kupata elimu ya Sekondari kuweza kupata elimu ya chuo kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaielezea baadaye vizuri zaidi wakati wa kushika shilingi utakapofika, naomba nizungumzie suala zima ambalo ninaliona kama changamoto kwenye Taifa langu, changamoto namba moja ninayoiona ni utekelezaji wa mambo tunayozungumza ndani ya Bunge, tangu nimefika hapa nikisikia michango inayotolewa hapa ndani najiuliza tatizo lipo wapi? Hapa ndani kuna michango very *constructive* watu wanaongea vitu vya maana tatizo kubwa kabisa ni utekelezaji na ninaomba namuomba Mheshimiwa Waziri haya yanayozungumzwa hata kama sio yote akayafanyie kazi ni kufanya kazi peke yake itatutoa tulipo kwenda mbele. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tusijekuwa Taifa la watu tunaozungumza watu tumeacha shughuli zetu kuja hapa tunaongea alafu hayafanyiki, haya yanayosemwa hapa yakifanyika nchi hii inabadilika. Tatizo kubwa kabisa ninaloliona katika nchi hii na ambalo ninaamini ni *solution* la mataatizo ya nchi zote za Afrika ikiwemo Tanzania ni mabadiliko ya *mind set* ni mabadiliko ya akili za watu namna wanavyotazama mambo, shinda kubwa kabisa tuliyonayo bado hatujabadiilita jinsi tunavyotazama mambo na namna tunavyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumrukku Dkt. Gwajima mara ya mwisho alipozungumza aliongea suala la *human resource is far better above natural resources*. Alisitisiza kwamba kinachohitajika katika nchi yoyote duniani ni watu kuwa na akili. Watu wakiwa na akili wataweza kutafsiri Liganga na Mchuchuma kuwa barabara, watu wakiwa na akili wanaweza kutafsiri utajiri walionao uweze kuwa elimu au huduma za afya, changamoto yetu ndiyo iko hapo tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya vyuo vikuu, shule za msingi inachangia kuweka akili kwenye vichwa vya watu. Kama siyo shule basi ni familia, kama siyo familia basi ni *society* tunazoishi ndani yake. Tunatia akili kwenye vichwa vya watu wetu ili waweze kutusaidia kutatua changamoto zetu. Ndiyo kazi ya shule, kazi ya vyuo vikuu ni kuweka akili na ufahamu kwenye vichwa vya watu ili waweze kuwa na uwezo wa kutatua changamoto zinazowazunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti na hapo hatutaweza kuhama mahali tulipo. Ndiyo maana leo nimesimama hapa kusema kwamba naona kuna tatizo kubwa sana kwenye mtaala wa elimu ya Tanzania. Hii ndiyo inasababisha nchi hii isiende mbele kwa kasi. Simaanishi kwamba hakuna kilichokwishafanyika, mambo mengi mazuri yamefanyika na yanaendelea kufanyika lakini mimi naomba mtaala huu ufumuliwe upya na kama ilivyoamuliwa uweze kupangwa upya ili uweze kupeleka Taifa letu mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano na mfano huu ni wangu mimi mwenyewe niliyesimama hapa. Mpaka mwaka 2017 nilikuwa darasa la saba, sikuwahi kusoma sekondari mahali popote kwenye nchi hii. Baadaye nikasema bora nirudi shule nikasome ili niweze kupata elimu ya kuniwezesha kufanya kazi zangu ofisini. Nikaenda *TCU* nikapeleka vitabu ambavyo nimeviandika nikawaonyesha walipoona vitabu vyangu wakasema unaweza kusoma chuo kikuu, nikapewa mtihani nikaufanya nikafaulu nikaingia *degree ya kwanza Tumaini University, one of the best University in the country* kutoka darasa la saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma pale miaka mitatu nimemaliza mwaka jana chuo kikuu, nina *degree* yangu safi, kutoka darasa la saba mpaka *university* na nimemaliza. Fuatilia pale utaambiwa nimemaliza na *GPA* 4.8 nikiwa *best student* katika chuo kile kutoka darasa la saba. Kilichonipeleka chuo kikuu mimi ni *RPL* lakini Mheshimiwa Waziri kaifuta. Kwa kuifuta anawanyima watu wengi sana fursa ya kupata elimu. Leo hii nimekaa hapa nasema kama *RPL* hairudishwi shilingi mimi sitaitoa, nataka kusema wazi hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme hapa mambo anayotakiwa kufanya Mheshimiwa Waziri kwa ajili ya elimu ya nchi yetu, naomba Waheshimiwa Wabunge hapo mlipo muandike neno UKUTA kwenye karatasi zenu, nataka kusema nini kifanyike kama *solution*.

Kwanza, lazima mtaala utakaokuja ufundishe ujasiriamali na uzalendo kwa taifa letu. Watoto wetu wafundishwe uzalendo kwa Taifa na ujasiriamali, itawasaidia sana baadaye hata wakikosa kazi waweze kuajiri wenzao. Mimi nimeajiri watu katika taifa hili na elimu yangu ndogo niliyokuwa nayo nimefanikiwa kuajiri watu ofisini na wanafanya kazi mpaka leo, jambo hilo lazima liwefundishwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, U tumeizungumzia K ni Komputa, lazima watoto wetu wafundishwe komputa

tangu wadogo. Haiwezekani Taifa hili hatufundishi watoto wetu elimu ya *computer*. Kuna shida gani tukifundisha *coding* kwa watoto wetu ili waweze kuwa na uwezo wa kutengeneza *software* na *application* mbalimbali? Taifa letu linaenda kwenye *digital economy*, dunia imebadilika sasa hivi *digital economy* ndiyo inayotawala dunia bila kuwapa watoto wetu elimu ya *computer* watawezaje kushindana? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, la tatu ni U, nimesema UKUTA, U inayofuata hapo ni uamuzi *either Kiswahili au Kiingereza basi*. Hatuwezi kuwafundisha watoto wetu Kiswahili mpaka darasa la saba halafu *form one* tunaanza Kiingereza, ni uongo. Wabunge wote walioko hapa ndani anyooshe mkono Mbunge yejote ambaye mtoto wake anasoma Kiswahili, tunawadanganya wananchi wetu. Sisi hapa wote watoto wetu wanasoma *international schools* na shule ambazo zinatumilia Kiingereza kufundisha; wakulima wetu tunawafundisha Kiswahili akifika *form one* wanafundishwa Kiingereza watoto wana-*fail* masomo, hatuwezi kuendelea namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, jambo la nne ni T ambayo ni tuamue, *practical* ni lazima iwe 70% na *theory* iwe 30% ili watoto wetu waweze kuwa-*competent*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda haunitoshi lakini naomba niseme kwamba nitawasilisha mchango wangu kwa maandishi, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wakati ukizungumza kuhusu Kiingereza au Kiswahili nikawa najiuliza wale amba walikuwa wanatoka ama tunatoka hapa unaenda kusoma lugha ya nchi unayokwenda halafu unapata *degree* ya pili, *degree* ya tatu yaani *degree* ya uzamivu, *degree* ya uzamili mbona iliwezekana? Najaribu kujuliza lugha ndiyo shida kweli ama tuna shida nyine? (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, wako watu wengi hapa wameenda Ujerumanii hajawahi kusoma hata neno moja

akafika kule kajifunza Kijerumani miezi sita ameweza kufanya *degree* ya uzamili na mwagine akafanya *degree* ya uzamivu. Wengine wameenda Urosi wamesoma udaktari Urosi kwa Kirusi wakiwa wametoka hapa wamesoma hii hii elimu yetu tunayoisema. Wengine wameenda China wanarudi hapa na Kichina na *degree* wamefundishwa kwa Kichina.

Waheshimiwa Wabunge, najiuliza kama shida ni kubadilisha lugha yaani kwamba tumetoka Kiswahili shule ya msingi tukaenda sekondari tukafundishwa lugha nyingine mbona tunaweza kusoma hizo lugha nyingine huko kwingine na tukafanya vizuri? Najaribu kusema kwamba ile hoja ya kutafuta hasa tatizo letu ni nini kama nchi ni ya msingi. Tukizungumzia lugha kwa namna ya kwamba yenye ndiyo inayotukwamisha, mimi nasikiliza michango yenu Waheshimiwa Wabunge humu mchanganyiko wa mambo Kiswahili hatukijui na Klingereza hatukijui wala lugha nyingine.

Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na mchangwa Mheshimiwa Tumaini Magessa atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Theonest.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa nafasi hii ambayo umenipatia kuchangia...

**NAIBU SPIKA:** Samahani kidogo Mheshimiwa Tumaini. Mheshimiwa Anatropia Theonest utachangia mchana kulikuwa na Mbunge ameomba kuchangia asubuhi hii ana dharura mchana, Mheshimiwa Taofiq ndiyo tutamalizia naye. Mheshimiwa Tumaini.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Elimu. Kwa sababu ya muda nitachukua maneno machache ya kuchangia hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee elimu bure. Hii elimu bure ambayo tulianza mwaka 2016 ilikuwepo siku nyuma inatupelekea mwaka 2022 kuwa na wanafunzi wengi

watakaoingia sekondari. Nashukuru kwamba Wizara ya Elimu ambayo ndiyo Wizara ya kisekta ikishirikiana na TAMISEMI imekuja na mpango ambapo kutakuwa na shule 1,000 zitakazoongezwa kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini ukweli ni kwamba ukigawanya kwenye halmashauri zetu utaona kila halmashauri itapata karibu shule tano, kama unafanya ugawaji sawia ule. Mahitaji halisi yaliyoko kwa wananchi wetu sasa ni karibu kila kata inahitaji sekondari nyingine kutokana na wingi wa hawa wanafunzi. Kwa mazingira hayo niishauri Wizara pamoja na mpango mzuri waliokuja nao Waziri na Naibu Waziri na hata TAMISEMI wa shule 1,000, zitakuwa hazitoshi kuhimili wingi wa wanafunzi ambao tutakuwa nao baada ya elimu bure kuingia sekondari, karibu kila kata lazima iongezewe sekondari nyingine moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini kingine ambacho nasimama kuishauri Wizara ya Elimu hapa kama nchi tatizo letu ambalo tumekuwa tunalisema hapa ni uadilifu. Uadilifu ni tatizo kubwa, je, ni mahali gani kwenye mitaala yetu tunaweza kuingiza watu wajifunze uadilifu. Kwa sababu kama nchi tatizo kubwa ni uadilifu na tumekuwa tunalisema hata hapa Bungeni, je, kwenye mitaala yetu ni mahali gani kwenye shule tulizonazo wanafunzi wetu wanaweza kuwa wanapata huu uadilifu. Nafikiri Wizara iangalie ni mahali gani tunaweza kutengeneza uadilifu wa watu wetu. Uzalendo tunaweza kuupata hata JKT na mahali pengine, je, uadilifu huu tuuingize wapi ili watu wetu wawe waadilifu na tufike safari yetu ya maendeleo tunayoenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini lingine ambalo nataka niliseme ni kutoka kwenye Jimbo langu Busanda na hata kwa jirani zangu Mbogwe, kuna majimbo makubwa kabisa ya kata 25 hayana high school hata moja. Kata 25 kubwa au kata 30 kubwa hazina high school hata moja na mpango wa Serikali ni kuanzisha shule moja, shule moja haiwezi kuwabeba hawa wanafunzi wote hata kama wanatoka sehemu za jirani na sehemu zingine ikawa ni high school ambayo itawachukua wanafunzi.

Niombe sana na niishauri Wizara kwamba kwenye maeneo tuliyonayo sasa wafikirie namna ya kuanzisha high school kwenye shule za zamani na hawa ndugu zetu wa Udhhibit Ubora waende wakaone vitu gani vinatakiwa kule badala ya kwenda tu na kuonesha mapungufu waoneshe vitu gani vinatakiwa vije Serikalini na hizo *high school* ziweze kuanzishwa.

Mwisho kabisa kwa sababu ya muda sasa tupo tunashughulikia maendeleo ya nchi yetu, tunapeleka umeme na maji vijijiini, tunaanzisha viwanda kule vijijiini, wataalamu wako wapi? Tunatakiwa kwenye majimbo yetu huu mpango uliokuwepo kwenye Wizara ya Elimu wa kuweka VETA kwenye maeneo mbalimbali hautoshi. Tunatakiwa sasa hivi kwa mahitaji tuliyonayo na ongezeko la wananchi kila jimbo liwe na VETA siyo kila wilaya. Kila Jimbo liwe na VETA kwa sababu watu wataendelea kuongezeka na mahitaji ya wataalamu yataendelea kuongezeka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, naomba niunge mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ajili ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake yote kwa kuandaa hotuba hii. Najua muda ni mfupi sana, mambo ni mengi lakini nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianzia kwenye ile hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna picha pale imeonyesha kwamba kuna mmoja wa wabunifu akiwa katika kiti cha walemaru ambacho alikibuni katika sherehe za kitaifa za sayansi na teknolojia mwaka 2020. Sasa napenda kufahamu hawa

watoto wetu wanaonyesha ubunifu na pengine na Watanzania wengine wengi, je, baada ya ubunifu huu nini kinaendelea, ni faida gani au tija gani inayopatikana baada ya ubunifu huu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijielekeze moja kwa moja katika mchango wangu. Napenda kuzungumzia kuhusu suala la uendelezaji elimu ya msingi pamoja na sekondari. Katika ukurasa wa 7 wa hotuba hii Mheshimiwa Waziri amezungumzia kwamba wamepeleka walimu 174 wa shule za sekondari ambao wamejengewa uwezo wa huduma za unasihi mashulenii. Mimi naishauri Serikali, tatizo la wanafunzi wetu ni kubwa yaani wana mazonge makubwa sana, kwa hiyo, wanahitaji sana kupata watu wa kwenda kuwaambia yale mambo yanayowasibu. Kwa hiyo, hii idadi ya walimu 174 kwa kweli ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba kama ikiwezekana ingewekwa programu maalum ya kuweza kuwafundisha walimu wengi zaidi hii elimu ya umahiri katika suala zima la unasihi ili kusudi walau kila shule ya msingi, sekondari na katika vyuo wawepo walimu hawa waweze kuwasikiliza hawa watoto na vijana wetu kwa sababu tatizo hilli ni kubwa sana. Ikiwezekana walimu hawa wa unasihi wawe wengi, wawe zaidi ya wawili au watatu ili mwanafunzi akiwa anahitaji huo unasihi aone ni mwalimu yupi ambaye anaona yeye mwenyewe anafaa kwenda kumpa ile shida yake aweze kumsaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naipongeza sana Wizara kwa sababu mimi *professionally* ni mwalimu najua tulikotoka, hali kwa kweli imebadilika. Haya yote tunayazungumza tunaishauri tu Serikali ili kusudi kuweza kuboresha zaidi. Jamani, mimi nilikuwa mwalimu mwaka 1984 sasa nikiangalia hii *trend* Wizara *you deserve all the best.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imesema kwamba imetoea mafunzo kwa walimu 1,076 ili waweze kuwafundisha wanafunzi wasioona, wenye ulemavu wa akili na ambao

wana matatizo mbalimbali ya ulemavu. Naomba nitoe ushauri kwa sababu watoto wenyewe mahitaji maalum wako wengi na sisi tunahamasisha sana hili suala la elimu jumuishi ni vizuri kama Serikali au Wizara ikaona kuna muhimu kuwe na *basic knowledge* yaani ianzie katika mitaala ya elimu ili kusudi kila mwalimu aweze kupata *basic knowledge* ya jinsi gani atakavyoweza *ku-deal* na hawa watoto wenyewe ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona kabisa sasa hivi kwa mfano hii elimu ya alama, kwa kweli elimu ya alama inahitajika sana. Kwa hiyo, kama watu wakipata zile *basic skills* ikawekwa kabisa kwenye mitaala ikawa *compulsory* ingawaje kuna wengine ambao watakuja kubobe basi ni budi Wizara ikaona kwamba *at least* katika mitaala kukawa kuna ulazima wa kusoma masomo hayo ili kusudi walimu wote ikiwezekana wawe wana zile *basic knowledge* za jinsi ya *ku-deal* na hawa watoto wenyewe ulemavu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuzungumzia kuhusu suala la mitaala, wenzangu wengi sana wamezungumzia, kwa kweli sisi tunaendelea kuishauri Wizara ijaribu kuona kwamba hii mitaala irekebishwe ili kusudi iweze kuendana na mahitaji ya sasa. Tumeona kabisa kwamba nchi yetu imeingia katika uchumi wa kati na hii mitaala lazima iangaliwe upya. Tunajua kabisa kwamba kuna stadi zimewekwa kule basi ni budi sasa kuangalia stadi nydingi zaidi ili kusudi hawa watoto wetu zile stadi wazitumie kujienda badala ya kusema kwamba wanategemea kazi za kuajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nilitamani na walimu pia ungewekwa utaratibu maalum wa *refresher course* za mara kwa mara. Hizi *courses* zitawasaidia kupata uwezo mzuri zaidi wa kuweza kuendana na hii hali halisi ya sayansi na teknolojia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna hili suala la kisomo chenye manufaa. Nakumbuka miaka ya nyuma kulikuwa kuna utaratibu wa kisomo chenye manufaa kwamba kuna wale watu ambao hawakupata fursa ya kusoma basi kuwe

kuna utaratibu kwamba ikifika wakati kuna masomo yale ya jioni, kulikuwa kuna walimu na Waratibu Elimu Kata wakifanikisha hilo. Nakumbuka kipindi cha Rais Marehemu Julius Kambarage Nyerere kuna baadhi ya wanafunzi walilokuwa bora walikuwa wanapelekwa kwenda kufundisha kwenye ile elimu ya Ngumbaro. Ili kupunguza watu wasiojua kusoma na kuandika ni budi basi Serikali ikaona kwamba inafufua vipi hiki kisomo chenye manufaa. Kwa hiyo, huo pia ulikuwa ni ushauri wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine nataka kushauri kwenye upimaji wa umahiri katika ngazi ya chekechea. Tunajua kabisa kwamba Serikali ina lengo zuri sana la kutaka kuona kwamba tunapata msingi mzuri hasa kwenye hii elimu ya chekechea. Najua kabisa katika elimu ya chekechea kuna umahiri ambao unapimwa kwa wale watoto kwa mfano, umahiri wa kutunza afya zao, kutunza mazingira, kuwasiliana, kuhusiana na kutumia zana za hisabati na kumudu stadi za kisanii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pale natamani hapa ndio tuweze kujua vipaji vya wale watoto wetu tunapoanzia nao kuanzia chekechea. *We build up from there* kwamba akipelekwa kwa yule mwalimu wake anayemfundisha darasa la kwanza akaambiwa kwamba huyu kipaji chake ni muimbaji mzuri tunaanza kumuanzishia pale. Huyu ameonesha kukaa sana na vifaa vya magari basi tumpeleke katika *trend* ile. Kwa hiyo, natamani Wizara au Serikali ione umuhimu sasa wa kuwaangalia hawa watoto tunawaendelezaje kutokea pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, natamani nitoe ushauri kuhusiana na suala la hawa wanafunzi ambao pamoja na upimaji utakuta kuna wengine hawajui kusoma, kuandika na kuhesabu. Nafahamu kwamba Wizara imeweka utaratibu kama ikitokea hivyo mtoto wa darasa la kwanza au la pili anaweza kukaririshwa lakini kama maendeleo yake bado duni tunafanyajae? Ni vizuri sasa tuweke utaratibu au kuweka madarasa maalum ili kuweza kuwasaidia hawa watoto ambao wana uwezo duni. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua muda ni mfupi sana naomba niunge mkono hoja, ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, huyo ndiyo alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa kipindi chetu cha kwanza. Mchana ama alasiri tutakuwa na wachangiaji wachache, niwataje ili waweze kuwahi maana muda wetu utakuwa umevana. Watakuwa ni Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, Mheshimiwa Anatropia Rwehikila Theonest, Mheshimiwa Boniface Mwita Getere, Mheshimiwa Taska Mbogo, Mheshimiwa Haji Amour Haji, Mheshimiwa Ighondo Ramadhan Abeid tutamalizia na Mheshimiwa Jeremiah Amsabi Mrimi.

Ninalo tangazo hapa kutoka kwa Waziri wa Maji, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wanaotoka kwenye miji 28 ambayo inafaidika na mradi wa maji huo wa hiyo miji 28 waonane naye leo mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge hapa, wataonana *DUWASA* kwa maana ya Ofisi za Mamlaka ya Maji Dodoma.

Kwa hiyo, muende huko ili mpeane uelewa wa pamoja kuhusu mradi huu. Naona wahusika wanapiga makofi wengine na sisi tutapata fursa siku nyininge tutapiga makofi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 kamili alasiri leo.

(*Saa 07.54 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni*)

(*Saa 10.00 Jioni Bunge lilirejea*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 - WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na majadiliano. Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, atafuatiwa na Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe na Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, ajiandae.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia kwenye bajeti ya Wizara ya Elimu. Kwanza, naomba radhi kidogo, uliniita hapo mapema, nilikuwa na mataizo kidogo ya kifamilia, nikatoka nje kuyashughulikia mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla naungana na wote waliotaa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara ya Elimu. Ni ukweli usiopingika kwamba unapotafuta wanawake wa mfano wanaofanya kazi nzuri ya Taifa letu, huwezi kuacha kumtaja Mheshimiwa Prof. Joyce Ndalichako. Niseme kwa kweli anatujengea heshima hata nasi tunaotoka katika Mkoa wa Kigoma kwa kazi nzuri anayoifanya kwa Taifa letu na sisi wengine tunajitahidi kuiga mfano wake ili tukipewa kazi kama hizi tuzifanyi kwa uhaminifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupitia mapitio ya utekelezaji wa bajeti wa 2020/2021, nimeona yapo maeneo ambayo Wizara imeonyesha kabisa kwamba yanahitaji msukumo, maana huko nyuma katika mapitio yalikuwa hayafanyi vizuri sana. Moja ya eneo ambalo nataka nilizungumze tena kwa mfano mzuri hata katika jimbo langu, ni hivi vituo vya *Teachers Resources Centre (TRC)*. Hivi vituo kwa ujumla vimekuwa kama havipo. Kwa mfano, mimi katika Jimbo langu la Kigoma Mjini, kulikuwa na vituo hivi katika Shule ya msingi Bungu, eneo la Mnarani, Shule ya Msingi Muungano

na eneo la Rusimbi, Shule ya Msingi Rusimbi; lakini vituo vyote hivi vimefungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, alitokea Afisa Elimu mmoja tu akaamua akasema ninyi walimu mliopo hapa nendeni mkafundishe, ondokeni nendeni madarasani, basi vile vituo vimekuwa kama vimefungwa. Hata hivyo, ukipitia mapitio ya Wizara na Taarifa yake ya 2020/2021 inaonyesha kwamba asilimia kama 54 wamevitembela, vinafanya kazi kwa takribani kipindi cha miaka mitatu sasa, lakini moja ya tatizo kubwa ambalo linakutana na vituo hivi ni kukosa mfumo wa TEHAMA. Unapozungumza katika dunia ya sasa ya Sayansi na Teknolojia, unakuwa na vituo vyta maarifa ya walimu ambavyo havina mfumo wa TEHAMA, maana yake unaendelea kuwarudisha nyuma hawa walimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme katika utekelezaji wa bajeti ya 2021/2022 Waziri ajaribu kuangalia uwezekano, kwanza kuwepo na hao walimu, lakini zaidi ya yote kuwepo na vifaa hivi vya TEHAMA. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anatazama bajeti yake hii angalie VETA. Tumetoa msukumo mkubwa sana wa kuanzishwa VETA kule ambako hakuna, lakini pale kwangu ipo VETA, lakini inakabiliwa na changamoto nyngi. Moja, ni tatizo kubwa la bweni. Mabweni yaliyoko hayatoshi na kwa maana hiyo wanachukua wanafunzi wachache kutokana na kukosa mabweni na vijana wengi wanaomba nafasi. Kwa hiyo, hili ultazame.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba, sasa hivi eneo moja kubwa linalofundisha vijana taaluma ya udereva ni VETA, lakini ukienda VETA ya Kigoma hiyo gari wanayofundishiwa wanafunzi ni kama wanafundishiwa matatizo badala ya kufundishiwa udereva. Maana mara isimame njiani, mara imekwama na iko gari moja. Sasa madhali eneo hili limetoa ajira ya kutosha; kuna boda boda, madereva wa magari na kadhalika, lazima VETA viwepo vifaa

vya kutosha vya kufundishia ikiwa ni pamoja na pikipiki na magari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo nataka niliseme katika mchango wangu wa leo ni huu uhusiano wa Wizara moja na nyngine katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Hili nalisema kwa maana Wizara ya Elimu bado yapo mahitaji makubwa ya vijana wa Kitanzania ya kupata Elimu za Taaluma na Elimu za Juu. Vipo vyuo vya kitaaluma ambavyo, kwa mfano, pale Kigoma kipo Chuo cha Hali ya Hewa. Chuo hiki kina eneo kubwa, kina miundombini mingi, lakini kinatoa taaluma moja tu ya hali ya hewa. Taaluma ambayo hata ajira yake ni ndogo sana katika nchi, muone uwezekano wa kuchukua kile chuo mwongeze taaluma nyngine ili kiwe hata Chuo Kikuu kishiriki cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam vijana waweze kupata nafasi za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo hivi mbali na kusaidia elimu, vile vile vinasaidia eneo ambapo kunakuwa na vyuo vingi, kama vile mfano Mkoa wa Iringa, mzunguko wa fedha unakua mzuri.

Mimi nimekaa Iringa pale nimeona, kuna vyuo vitatu pale; kuna Tumaini, kuna Mkwawa na *Ruaha University*. Hivi vyuo vina wanafunzi pale zaidi ya 3,000. Kwa hiyo, mzunguko wa fedha katika mji ule wa Iringa unaona hata unachangamka kutokana na vyuo vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika miji hii ya kwetu kama Kigoma ambayo kidogo mzunguko wa fedha ni mdogo, mnapoleta vyuo hivi, basi mnatusaidia na sisi mzunguko wa fedha unaongezeka. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, atafuatiwa na Boniphace Mwita Getere na Mheshimiwa Taska Mbogo, ajiandae.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata hii fursa ya kuchangia katika

Wizara ya Elimu. Niungane na maoni ya wasemaji wengi na mmoja wao ameongea mchana akieleza umuhimu wa Wizara ya Elimu kuondosha fedha ya mikopo ambayo ni zaidi ya shilingi bilioni 500 ambazo zinakuwa zinahesabika kama fedha ya maendeleo. Hiyo fedha inaonyesha kwamba bajeti ya Wizara inakua; bajeti ya Wizara ni kubwa, lakini katika uhalisia wake bajeti inakuwa ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano katika mwaka uliokwisha, kati ya miradi 33 ambayo mliahidi kuitekeleza, ni miradi sita tu imetekeliezwa ambayo ni sawa na asilimia 18. Sasa hiyo inatosha kuona kwamba bajeti inaonekana iko kubwa, bajeti inajitosheleza lakini fedha inaenda kwenye kukopesha wanafunzi. Hiyo kwa nini haipo kwenye Wizara nyingine? Mbona tunaona hiyo fedha ya mafunzo, fedha ya kufanya *activities* nyingine inakuja kama OC, lakini ikija kwenye Wizara ya Elimu, inaonyesha kwamba ni fedha ya maendeleo. Nadhani tusifanye hivyo ili tupate picha halisi, tujue kama fedha haitoshi tupambane ili tuweke fedha za kutosha. Mimi ndiyo wito ninaoutoa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala tumekuwa tukiliongelea humu siyo mara ya kwanza. Kwa hiyo, nitapenda Wizara itueleze, hicho kigugumizi kinatoka wapi? Kwa sababu, hii siyo mara ya kwanza, wala ya pili na aliyeisema hapa alikuwa Mbunge ambaye ni mgeni. Kwa hiyo, ina maana na yeche kipimo ni *concern* na kwetu ni *concern*. Ina maana Wizara haipati fedha ya kutosha. Tukija hapa tunaona kwamba fedha ya maendeleo ni shilingi bilioni 900, lakini *in reality* ni kama shilingi bilioni 405 ambayo ni tofauti sasa na fedha ya mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo niungane na waliongea kwamba lazima vyuo vya kati vipewe mikopo, kwa sababu *actually* wale watu ndio tunaowahitaji kwa sasa. Leo nimesoma taarifa ya CAG kwamba, sokoni kwa maana ya *ma-graduate*, wanakuja kama 100,000 au 150,000 *plus*. Katika miaka hii mitano ina maana udahili umeongezeka, tunazidi kutengeneza *ma-administrator* badala ya kutengeneza watu wanaoenda kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tuwape wale vijana fedha na tunao wengi kwa sababu ya mfumo wetu wa elimu ambao sijui kama muda wangu utanitosha, lakini ningependa kuongelea mfumo wa elimu tulionao sasa. Hiyo ni ya kwanza, kuondoa kutengeneza fungu *specia/kwa ajili ya hiyo mikopo* badala ya kuiacha kwenye kifungu cha maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaenda mbali sana, niongelee changamoto ya Wilaya ya Kyerwa. Mimi ni Diwani katika Halmshauri ya Kyerwa na ninajua Wizara ya Elimu ndiyo *ina-deal/na* kudhibitisha sasa kwamba shule *ive-accredited* sasa iweze *kuwa-admit* wanafunzi na ipate usajili. Kyerwa tuna changamoto ya shule nydingi ambazo hajizawa *accredited*. Mfano, kuna shule inaitwa Isihoro, ipo Kata ya Mrongo. Hiyo shule wazazi wamechangishana wenyewe. Ina vyumba takribani viwili mpaka tatu na ina vyoo. Ila hiyo shule hajjaweza kuanza. Watoto wa maeneo hayo wanatembea zaidi ya kilomita nane kwenda kutafuta elimu, siyo sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kurudia aliyoyasema Mheshimiwa Spika; wakati wazazi sasa wanaona shule imeanza, wanapata morali ya kuendelea kujenga zaidi, lakini na Serikali itaanza kuweka jicho lake pale, lakini tukiendelea kuyaacha yale yakiwa magofu, tutakuwa tunasaidia nini? Hatupeleki walimu, hatupeleki *capitation fee* na majengo hayaendelei na juhudzi za wananchi zinakuwa hazina maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo ya Isihoro tu, hiyo ipo pia Kashanda. Nimefanya ziara, nimefika kwenye Kata ya Kakanja. Pia kuna shule inaitwa Nyakagera, nimefika. Hiyo shule sasa wamemaliza hadi Darasa la Saba, badala ya kufanyia mtihani pale kwa sababu hajijasajiliwa, wanaenda kufanyia mtihani kwenye Kata ya Kakanja, nadhani siyo sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tutengeneze utaratibu, ambao *at least* ameeleza vizuri Mheshimiwa Mwalimu Tunza, kwamba hata tunavyokuwa tunasajili, basi tutengeneze *standard* kwamba, hii imesajiliwa lakini bado inachangamoto *ABC* lakini naweza kuruhusiwa kuendelea na kazi nyingine. Hiyo ipo pia huko Kata ya Kichenkura, iko

Chakalisa Kata ya Kimuli, iko Kashasha, Kata ya Kibale; Muhulile, Kata ya Nkhwenda; na Chaju Kata ya Mabira. Kwa hiyo, natoa picha mwone sisi Kyerwa kama Halmashauri kama Wilaya tuna changomoto kubwa kiasi gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichomekee hapo hapo, Mheshimiwa Waziri wewe ni mwanamama; unapoenda kugawa hizo sekondari za bweni 26 kwenye mikao mbalimbali, tunaomba Kagera hiyo sekondari ijengwe kule Kyerwa. Ninaomba hayo kwa sababu ukija kuangalia jio grafia ya mkoa wetu Kyerwa ni kama imeachwa pembeni. Ni wakati huu tu zile shule za sekondari zimepandishwa hadhi na kuwa *high school*. Miaka yote hatuna Kidato cha Tano wala cha sita. Kwa hiyo, watoto wa kike wa maeneo yale ni watu ambao kama hawakupewa kipaumbele. Tuna ardhii ya kutosha, tuna eneo la kutosha, hebu tupeni hicho kipaumbele, tutawalipa matokeo ninakuomba sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi pia kwenye ambayo wamesema wenzangu. Tuangalie dira ya elimu *vis a vis output*, nimepitia kama alivyoongea Mheshimiwa Askofu Gwajima na Mheshimiwa Nusrat. Wamesema Dira ya Elimu inasema ni kuwa na Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi, umahiri, uwezo na mtazamo chanya ili kuweza kuchangia katika kuleta maendeleo ya Taifa. Twende kwenye dhima, kuinua ubora wa elimu na mafunzo na kuweka mfumo na taratibu zitakazowezesha kupata idadi kubwa ya wanafunzi walioelimika. Sitaki kuendelea, lakini Wabunge wengi wameongelea hapa, wanasesma Sera yetu ya Elimu ya 2014 ina matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kila Mbunge anayesimama anaongea, Serikali inapata kigungumizi gani kurudisha mchakato na wananchi wakashiriki ili tuone aina ya elimu tunayoitaka? Mimi sioni kama sera inaongea vibaya, dhima sioni kama inaongea vibaya, lakini ukiangalia *output*, kwa nini *hai-respond* sera inasema nini? Ina maana kuna tatizo somewhere. Aidha ushiriki wa wadau au wameshindwa kuwa *compatible*, ina maana lazima tutafute *solution* ya kudumu pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine ambao nitataka kuusemea kwa mfano mfupi tu leo, elimu yetu ya Tanzania tullyonayo leo ni ya *ku-pass* mitihani. Ukiangalia humu ndani utaona watu *wana ma-degree*, watu wana vyeti, watu wana *Ph.D.*, lakini anaolewa nini? Hilo ni swali kubwa ambalo huwezi kulijua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mama ni mwalimu; mimi ni mwalimu pia, *degree* yangu ya kwanza nimesoma Ualimu. Tulifundishwa kwamba elimu ni kile ambacho kinabaki kichwani baada ya vile vyote ulivyofundisha kusahaulika. Sasa sisi tunaoenda kukusanya vyeti, unachokifanya ni kukariri tu; *examination, examination and passing the exam*. Unapewa cheti, biashara imeishia hapo. Ni lazima tuangalie sera yetu ya 2014, ni lazima tuangalie dira yetu tuweze kuvioainisha hivi vitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaongea kitu kingine. Leo tuna waandishi kadha kadha wa vitabu, lakini mmewahi kuona *standard za vitabu vinavyoandikwa?* Mmeshaona vitabu wanavyovisoma wanafunzi? Vitabu vingine ni matangopori, yaani matangopori *pa pa pa!* Nakumbuka tukiwa *Advance na O' Level* tulisoma vitabu vya Nyambali Nyangwine, mwalimu anakuja anasema vyote vile mlivyo soma ilikuwa ni *OP (out of point)*. Sasa leo tumeweza *censorship* ipi ya kuona vitabu wanavyovitumia wanafunzi wetu ni sahihi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Japokuwa dah! Vyeti yetu tena vinaletwa kwenye maswali hapa! Nadhani pengine itabidi tumwombe Mheshimiwa Spika aweke utaratibu mzuri wa mambo haya. Maana jamani vyeti vikiwekwa vyote kapu moja, kweli namna ambavyo huwa tunavisotea hivyo vyeti siyo masihhara jamani. Ni kazi ngumu mtu kupata *Ph.D.* Hao watu wengine huko mimi sielewi habari zao, lakini ninachojua ni kazi ngumu. Ukipikia mtu anaitwa Profesa, labda kama kanunua au ni kama Professa Maji Marefu, lakini kwamba amefanya kazi, ukiacha hao wa kuijita;

hilo la kujiita ni suala lingine, lakini kisomo ni muhimu kiheshimiwe. Ndiyo hivyo, nasi wasomi tujitahidi basi kuishi kwa kile cheti chako. Maana na sisi tupo ambao tunasababisha maswali, tunaitana huku Madaktari halafu ndiyo mtihani tena. (*Makofi*)

Haya, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Taska Restuta Mbogo dakika tano na Mheshimiwa Haji Amor Haji ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hii Wizara. Kwanza tu nimpongeze dada yetu, ndugu yetu Mheshimiwa Prof. Ndalichako, anafanya kazi kubwa sana kwa kweli. Hii ni pongezi bila unafiki, anafanya kazi kubwa sana. Wizara hii toka ameishika tumekuwa na mabadiliko makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo shule zilikuwa zinaitwa za vipaji au shule maalum; ukienda pale Mara kuna *Alliance*, kuna Tabora, kuna Msalato, kuna Nganza na maeneo mengi. Amefanya kazi kubwa *ku-renovate* zile shule zimekuwa nzuri sana. Shule zile zinavyojengwa, hata kama imejengwa Bukoba, Tabora na kadhalika, watoto wetu wote wa Kitanzania wanaenda kusoma pale. Kwa hiyo, amefanya kazi nzuri sana, mama tunatakiwa kukupongeza kwa kazi nzuri, kuwapongeza na watumishi wako wote waliofanya kazi hiyo nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nazungumza jambo la *corruption of mind*; na katika hili namshukuru sana Marehemu Dkt. John Pombe Magufuli aliyekuwa Rais wetu. Alikataa jambo la *corruption of mind*. Hivi kweli asingekuwa yeeye, hili suala la *corona* huku kwetu leo ingekuwaje? Tungevaa mabarakoa mpaka yakavunja kila kitu. Kwa hiyo, akakataa *corruption of mind* kwa maana ya kwamba siyo kila kitu unachokiona ukifanye wewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wamezungumza Wabunge wengi hapa leo, hivi kuna haja gani watoto wanaokaa kwenye ardhi ya udongo mwekundu ukaambiwa wavae

*uniform* nyeupe kila siku? Kuna haja gani? Kuna vitu vingine Mheshimiwa Prof. Ndalichako unatakiwa uvitazame, kwamba jamani hivi kweli hili tunaenda nalo mpaka lini? Nasema hiyo ni *corruption of mind*. Juzi tu kuna mtoto ameniuliza swalii, ni mwanangu mdogo tu, kwamba hivi baba, Waziri Mkuu wa Kwanza wa Tanzania ni nani? Nami nimekaririshwa huko *primary* nikasema Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Akanicheka, nikasema huyu mtoto amekuwaje? Akaniambia hapana baba, Mwalimu Nyerere alikuwa Waziri Mkuu wa Tanganyika, kwa sababu Tanganyika iliishia 1962 na Waziri Mkuu wa Kwanza wa Tanzania alianza 1964. Ni nani sasa? Rashid Kawawa, si nikakaa kimya. *Corruption of mind!* Yaani tunakaa, tunakariri vitu, hatuna uwezo wa kubadilisha kwamba hili liendeje na lifanye kazi gani? Mama nakushukuru umefanya kazi nzuri. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kuhusu kile kituo changu cha VETA. Chuo cha VETA mama nimekutembelea sana na nimekuja kwako sana. Kuna shule inaitwa *Mgeta Primary* Chuo cha Ufundii, inafundisha ufundi pale, imesajiliwa kwenye ufundi, inafanya mitihani miwili; ya kawaida na ufundi.

Mama naomba ukumbuke kwenye hicho Chuo cha VETA, kipindi hiki kwa kweli, utakuja nayo tu, kwa sababu uliniahidi kwamba mwaka huu utaondoka nayo, nami nakubali kwamba ukija uje vizuri kwenye hiyo VETA. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shule nane katika Jimbo langu la Bunda; kuna Shule ya Hunyali, haina Walimu wa Sayansi; Shule ya Chamuriho, haina Walimu wa Sayansi; Shule ya Salama, haina Walimu wa Sayansi; Shule ya Milingo, haina walimu wa sayansi; Shule ya Mtomalilo haina walimu wa sayansi, Shule ya Nyamanguta, haina walimu wa sayansi; Shule ya Makongoro, haina Walimu Sayansi; na Makongoro *High School*, haina Walimu wa Sayansi. Kama katika shule wanahitajika Walimu 24 wako watano au sita. Naomba tafadhalii kwenye huo mgao wa Walimu uweze kupata nafasi ya kunisaidia kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere, mimi huwa nasema na huwa tunaimba hivi bila Mwalimu mambo yangekuwaje? Hivi inakuwaje yule Mwalimu ametutumikia miaka 24 na ye ye hakujenga chuo wala hakujenga barabara, leo mkienda kujenga chuo nyumbani kwake, chuo kinakaa pale kama maganda fulani, hivi hivi anajisikiaje pale kwenye kaburi lake, hivi kama hakukuwa na haja ya kwenda kujenga pale kwa nini waende kujenga? Wametoa Walimu, wametoa kila kitu na kila jambo liko pale, lakini chuo hakipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi Mwalimu pale kwenye kaburi lake anajisikiaje? Kama Wizara hajawa na mpango maalum jamani wa kwenda Butiama, isiende, ili yule mzee akae vizuri kule, hivi anaonaje wameenda kumjengea chuo wanaliita jina lake na chuo hakipo miaka 14; majengo tumewapa bure, kila kitu tumewapa bure, hivi inakuwje? Hii nayo inaleta tatizo sana kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, nilitaka tu nimkumbushe mama VETA ni muhimu sana. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Mheshimiwa Haji Amour Haji na Mheshimiwa Ighondo Ramadhani Abeid ajiandae.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa napenda nimpongeza Mheshimiwa Profesa Ndalichako kwa kazi nzuri sana aliyoifanya kwenye Wizara hii ya Elimu. Mchango wangu unaenda moja kwa moja kwenye lugha ya kufundishia, siamini kwamba watoto wakifundishwa Kiswahili wataelewa Zaidi, kwa sababu hata mimi nilijifundishwa kwa lugha ya Kiswahili, nimesoma masomo kutoka darasa la kwanza mpaka darasa la saba kwa Kiswahili. Nikaenda Sekondari ya Loleza nikapambana na Kiingereza. Nikasoma *geography* kwa Kiingereza, *history* kwa Kiingereza, hesabu kwa Kiingereza, *chemistry* kwa Kiingereza, *biology* kwa Kiingereza na masomo mengine yote kwa Kiingereza na

tuliweza kufanya hivyo tukaweza kufaulu mitihani. Hoja yangu ni kwamba tuangalie tatizo ni nini, lugha sio tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba tusije tukawandanganya Watanzania tukasema kwamba wakifundishwa kwa Kiswahili ndio wataelewa wakati watoto wetu tunawasomesha kwenye *english medium*, hiyo itakuwa ni dhambi kubwa sana tumeifanya. Naamini Wabunge humu ndani watoto wao wanasoma kwenye zile shule zilizoanzishwa sasa hivi za *English medium*, sasa tukianza kujenga hoja hapa kwamba watoto wafundishwe kwa Kiswahili tutakuwa tunawakosea sana Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri hoja muhimu ni kuangalia tatizo nini, kwa nini wanafunzi hawelewi darasani, lakini tatizo sio lugha. Je, utakuwa unajenga Taifa gani ambalo litakuwa linafundisha lugha moja ya Kiswahili, naamini kwamba lugha ni biashara, lugha ni mtaji na lugha ni elimu. Nasema lugha ni mtaji kwa nini, lugha ni mtaji kwa sababu unapojuia lugha nydingi unajua Kifaransa, Kispaniola na Kiingereza, ina maana una-command/lugha, hata unapoitwa kwenye *interview* utakuwa unaenda kujieleza vizuri. Kwa maana kwamba unaweza ukaenda kwenye zile nchi, ukafanya kazi, lakini kama wewe umekaa na lugha moja ina maana huna *exposure*, huwezi kwenda kufanya kazi hizo nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mawazo yangu, ningependa kwanza Mheshimiwa Ndlichako aongeze lugha; lugha nydingi zifundishwe mashulen kama Kifaransa, Kispaniora na Kiingereza kiwekewe mkazo ili watoto wawe na *confidence* wanapoitwa kwenye *International Organizations*, wasiingiwe na ile *inferiority complex*, wanaanza *can you explain yourself*, anaanza ho ho ho badala ya kueleza *my name is so and so*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lugha pia ni biashara, mfano unakwenda china unajua Kichina, ina maana wewe *uta-bargain* biashara za kule China. Kwa hiyo hoja yangu ni kwamba shule ziongezewe lugha za kufundishia, lugha ziwe nydingi, sio lugha moja tu ya Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo ningependa kulizungumza leo ni vitendea kazi kwenye shule zetu za msingi pamoja na sekondari, lakini hasa za msingi. Ningeomba Mheshimiwa Profesa Ndalichako, Waziri wa Elimu awasiliane na Wizara ya Maliasili na Utalii. Kuna misitu mingi sana hasa kule kwenye Bwawa la Nyerere ambako kunajengwa umeme kule *Stigler's Gorge*, ile miti inayokata wanatengeneza mbao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri awasiliane nao, apate zile mbao ili ziweze kutengeneza madawati kwa sababu wanasafisha pale kwenye lile bwawa, kwa hiyo ile miti wanatengeneza mbao lakini zile mbao wanazuwa. Namwomba awasiliane na Wizara ya Maliasili ili mbao ziweze kupatikana madawati yaweze kutengeneza kwa wingi na watoto wetu wasiweze kukaa chini na hapo tutakuwa tumelenzi falsafa ya Hayati Dkt. John Pombe Magufuli ya elimu bure kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nafasi bado ipo nilipenda kuzungumzia pia mfumo wa elimu. Mheshimiwa Ndalichako itakuwa ni vizuri sana kwa sababu amesema anakwenda kurekebisha mfumo, tunaomba kwa sababu kulikuwa na kujichanganya hapa katikakati 2015 to 2020, alikuwa amesema watoto watasoma kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la 12 ndio watakuwa wamehitimu, lakini baadaye akaja akarudisha kwenye ile sera zamanii tuliyosoma sisi la kwanza mpaka la saba, halafu kwenda sekondari, itakuwa ni vizuri sana aki-review hii sera ya elimu ili tujue Tanzania sera yake elimu ni ipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine la mwisho ambalo ningependa kuzungumzia kama muda upo...

Mheshimiwa Naibu Spika, basi nimeona umewasha kipaza sauti, hivyo naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Haji Amour Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Ighondo Ramadhani Abeid.

Tutamalizia kwa upande wa wachangiaji Wabunge na Mheshimiwa Jeremiah Amsabi Mrimi

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako nami nichangie Katika Wizara ya Elimu. Kwanza namshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweza kuondosha ile tozo ya asilimia sita katika mkopo wa elimu ya juu.

La pili nije katika mchanganuo wa hoja zetu ambazo kila mmoja katika kusimama kwetu hapa kwa mujibu wa Wabunge wengi wanacholilia ni vitu viwili. Kwanza, wanalilia mfumo wa elimu ambaeo tulokuwa nao na la pili wengi wao wanazungumzia suala la *curriculum*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani nije kwa upande wa kuangalia mfumo wa elimu. Mfumo wa elimu kwa upande wa Tanzania, mie nimetokea upande wa Tanzania Zanzibar.

Kule Zanzibar zamani tulikuwa tumeanzia ile *base*, tulikuwa tuna kitu ambacho tunakiita uzalishaji mali, ambapo kwa zamani uzalishaji mali maana yake ilikuwa imeanzia kuanzia *standard one* hadi *standard seven*, maana yake tunajifunza masuala ya elimu ya vitendo kama kulima pamoja kufuma na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kukua kwa leo, kwa sababu tuna uleo, maana yake tunasema kwamba tuna elimu ya ujasiriamali. Sasa katika vitu viwili hivyo maana yake nilikuwa najuliza huu uzalishaji mali na ujasiriamali sjui tofauti yake ipo wapi. Kikubwa zaidi nijaribu kuzungumza kwamba, ningekuwa naulizwa, ningesema kwamba, tungekuwa tunaanza na ile elimu ya uzalishaji mali kuanzia ile *standard one* au kuanzia darasa la chini huku maana yake kwenda juu ili kumkuza mtoto katika misingi ya kujua ujuzi. Bila ya hivyo, kwa kusema kwamba tusubiri tu wanafunzi watakaomiliza katika elimu za juu au kuanzia kumaliza darasa la saba wajunge katika mafunzo ya ufundi maana yake pale tutakuwa kuna kitu tunakipoteza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ushauri wangu kwa Wizara ya Elimu ni kwamba haya mafunzo ya ufundi hasa ambayo kwa huku tunaita ni mafunzo ya ufundi, tungeanzia huku kwenye *standard one* tukaanza na huo uzalishaji mali. Tukizungumzia suala la uzalishaji mali maana yake yule mwanafunzi unaanza kumjenga namna ya kuanza kujua kama ni kulima anajua nini maana ya kulima; kama ni kufuma, anaanza kujua nini maana ya kufuma. Sasa tunapokuja katika hatua ya juu, hapo ndio tunakuja katika suala la *entrepreneurship*, suala la ujasiriamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba kwa upande wa Wizara ya Elimu, suala hilo lazima wajaribu kuliangalia, mbali na mitaala yetu ambayo tunayo hapa Tanzania, kwa sababu kila mmoja maana yake analaumu mtaala, lakini suala la mitaala hili linakuja kutokana na mfumo wetu na namna ambavyo watendaji wetu wanavyohisi, kwa sababu Tanzania tuna mfumo ule wa kwamba kila mmoja anapokwenda katika nchi fulani kwenda kusoma anarudi na mfumo wake. Anayekwenda China akirudi akija Wizara ya Elimu atakuja na mfumo wa Kichina; anayekwenda Japani atakuja na mfumo wa Kijapani; na anayekwenda Marekani atakuja na mfumo wa Kimarekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa bado sisi wenyewe hatujajjua hasa tunachokitaka ni kipi katika mfumo, kama Watanzania ukilinganisha na tamaduni zetu pamoja na silka zetu. Bila kujua hilo maana yake itakuwa ni vigumu sana na kila siku tutasema mtaala sio au tunakokwenda siko, lakini kitu muhimu zaidi, tunapotengeneza hii mitaala yetu, kitu cha msingi tujaribu kuangalia tamaduni zetu zinatuelekeza wapi na mazingira yetu yanatuelekeza wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikizungumzia suala la mazingira, Tanzania ina mikoa mingi, kila eneo lina vitu vyake katika masuala ya uzalishaji. Kuna mikoa ambayo inazalisha sana katika kilimo, kuna mikoa ni madini, kuna mikoa ni mambo mengine, maana yake kila mkoaa una sifa ya aina yake. Nadhani kwamba tungejaribu kuangalia kuangalia

elimu kwa kutazama hasa mifumo ya mikoa pamoja na uzalishaji wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pale zamani wakati ule ambapo sisi tupo kwa sababu kwa upande wa kule Zanzibar unapoanza *primary school*, unapokwenda sekondari kulikuwa kuna ile kwamba mtu anapokuja kufauli kutoka darasa la sita au darasa la nane, kwa sababu kulikuwa kuna darasa la nane kwenda la tisa kulikuwa kuna fani maalum ambayo mwanafunzi yule anatoka pale kuelekea katika ile fani. Kwa mfano tuwe na wanafunzi ambao watakwenda kusomea kilimo tangu sekondari, tuwe na wanafunzi...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ighondo Ramadhani Abeid, atafuatiwa na Mheshimiwa Jeremiah Amsabi Mrimi na Mheshimiwa Juma Kipanga, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ajiandae.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi angalau na mimi niseme machache kwenye mjadala wa Wizara yetu ya Elimu ambayo ni Wizara muhimu kwelikweli kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuipongeza na kuishukuru Serikali; nampongeza sana Rais wetu Samia Suluhu Hassan kwa hatua yake muhimu sana ya kuondoa ile asilimia sita kwenye mikopo ya elimu ya juu. Kitendo hiki ni cha kiungwana na kwa kweli nampongeza sana. Vilevile nimpongeze Waziri wa Elimu kwa kuondoa ile asilimia kumi iliyokuwa inatokana na penati kwa maana ya wanufaika kuchelewesha mkopo ule kwa hiyo naishukuru sana Serikali kwa hatua hii hapa imeonyesha ni kwa kiwango gani inamjali Mtanzania wa chini, yule maskini, kwa sababu

mikopo hii lengo lake ni kuwakomboa watoto wa kimaskini wa Kitanzania ambao hawawezi kukopeshwa na mtu ye yote yule isipokuwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe mikopo hii sasa tapanue wigo tuipeleke kwenye ngazi za chini, kwenye ile elimu ya kati, vyuo vya kati, *VETA* vyuo vingine vya ufundi tumesha-*train graduates* sasa naona kwa kiwango fulani, mpaka tumeshindwa kuwaajiri na wenyewe wako mataani kila mahali. Naomba sasa tuelekee na huku kwenye hii elimu ya kati ambao ndio wanaofanya kazi moja kwa moja, tena hawa ukiwapa mkopo leo hii, ndani ya miezi mitatu anakwenda kufanya kazi moja kwa moja, kama ni fundi atapaua, atajenga ukuta, atapata fedha atakuja kurudisha huu mkopo.

Kwa hiyo, naomba sana Serikali iangalle sasa kwenye elimu ya kati nao wanufaike na hii mikopo na ikumbukwe hivi sasa tuna shule hizi za sekondari karibu kila kata. Kwa hiyo sio wote wanaoweza kwenda vyuo vikuu, turudi huku chini huku nao wanufaike na mikopo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapohapo niombe sasa huu mpango wa Vyuo vya *VETA*, nilishaongea sana na Waziri wa Elimu mara kadhaa, aipe kipaumbele Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Jimbo la Singida Kaskazini katika kupata Chuo Cha *VETA*. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, vijana wana wito mkubwa sana wa kwenda kusoma mafunzo ya ufundi, lakini hakuna chou, viliyyopo ni mbali, havifikiki, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri akija hapa niombe *commitment* yake, aniambie ujenzi wa Chuo cha *VETA* Singida Kaskazini ni lini utaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja hapa naomba nichukue nafasi hii kulisema, kwa sababu tukiendelea kunyamaza tutakuwa hatuitendei haki nchi yetu. Nchi yetu imeweka rasilimali nyingi sana kwenye elimu, vyuo vikuu vya kutosha, vyuo vya kati na shule za sekondari na hata za msingi. Nataka nitoe masikitiko yangu makubwa sana, sisi hapa Bungeni mara kadhaa tumekuwa sasa vinara

wa kubeza juhudhi hizi na kuonyesha elimu haina umuhimu. Hili jambo kwa kweli, naomba tulichukulie umakini na twende kwa tahadhari.

Mheshimiwa Naibu Spika, *statement* tunazozitoa sisi Wabunge humu Bungeni hata wakati mwingine utanisamehe, hata kitu, kwamba elimu ya darasa la saba ni ya muhimu kweli kuliko wasomi maprofesa. Hii *statements* sio nzuri, sio kwamba napuuza darasa la saba, hapana, nahestimu sana mchango wao na nahestimu sana umuhimu wao kwenye nchi yetu, lakini naomba twende kwa tahadhari, tusije tukafika mahali tukapuuza elimu, tukapuuza taaluma, tukapuuza wataalam, tutalidhalilisha Taifa hili. Tutafika mahali tutaangamiza Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuanzia leo baada ya hotuba hili, tuache kabisa kejeli kwenye taaluma, kwenye elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naomba pia nizungumzie upungufu wa Walimu kwenye shule zetu za misingi na sekondari...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa nafasi. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jeremiah Amsabi Mrimi, atafuatiwa na Mheshimiwa David Ernest Silinde, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Mheshimiwa Juma Kapinga Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia ajiandae.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ya kuchangia Wizara ya Elimu. Nazidi kushauri na kupendekeza Wizara hii kupewa fedha zilizoombwa na kuona uwezekano wa kuiongezea fedha nydingi Zaidi. Hii ni kwa sababu Wizara ya Elimu ni moja ya

Wizara pekee zinazoweza kuzifikisha nchi yetu mahali tunapopata. Nasema haya kwa sababu ukiangalia hata katika Dira ya Maendeleo ya Taifa letu ya 2020 – 2025, katika yale malengo makubwa matano tuliyokuwa nayo, malengo yote matatu yanategemea sana elimu ili tuweze kufikia huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika llani yetu ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi imeonyesha tunahitaji kutoa zaidi ya ajira milioni nane na hizi ajira kwa hakika zitakana na uboreshaji mkubwa wa elimu.

Pia ni dhahiri kuwa, tafiti nyingi zimefanywa, kwa mfano utafiti mmoja wa *ending poverty in India* uliofanywa na Profesa Ramanuja umeonesha hakuna nchi yoyote inaweza ikaendelea zaidi ya maendeleo yake katika elimu. Kwa hilo niombe tutenge fedha nyingi ili kuona tunaweka vizuri katika elimu

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri kwa kazi kubwa ambayo wameifanya kwa miaka mitano iliyopita pamoja na Wizara yote kwa ujumla, lakini niombe kuchangia mambo machache kwa ajili ya kuboresha zaidi na kufikia matarajio ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Wizara ikawekeze zaidi katika bajeti hii kuona tunapata Walimu wa kutosha. Shule zetu nyingi hazina Walimu wa kutosha, katika jimbo langu la Serengeti ukienda shule nyingi Nagusi, Serengeti, Machochwe na zingine nyingi hazina Walimu wa kutosha. Walimu wengi imeonekana wanaoletwa katika Jimbo la Serengeti, wanahama, wanaobaki ni wachache.

Sasa wakati tunajipanga kujenga nyumba za kuishi pamoja na mazingira kuboreshwa Zaidi, niombe Wizara ishirikiane na Wizara nyingine kuhakikisha kuwa Walimu wanaojitolea ambao wanatoka mazingira yale, tuweze kuwapatia kipaumbele katika ajira na mie niko tayari kutoa ushirikiano mkubwa kwa Waziri ili kuona kuwa tunawaajiri vijana wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri pia tuwekeze zaidi katika maabara, vitabu na mabweni. Shule yoyote ya sekondari isiyokuwa na vitabu nya kutosha na maabara ni sawa na kujenga bwawa la kuogelea lisilokuwa na maji. Na shule zetu bila kuwa na maabara, bila kuwa na vitabu watoto hawa tusitarajie kuwa na elimu tunayoitaka. Kwa hiyo, niombe fedha nydingi iende kuwekezwa huku.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tuangalie kwasababu ya changamoto ya fedha kutotosheleza, katika jimbo langu na majimbo mengine ambayo wamejenga maboma ya maabara, maktaba pamoja na mabweni ziende kupewa fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunakamilisha mabweni, maabara pamoja na maktaba. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jimbo langu shule za Sekondari za Serengeti na Dagusi, Shule ya Msingi Mugumu, Kitunguruma, Machochwe, Kisaka, Ngoremi wameshajenga maboma pamoja na shule nydingine nydingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende pia kushauri kwamba ili tufikie ajira milioni nane, sasa Wizara iende kuweka kipaumbele kikubwa katika ujenzi wa vyuo nya VETA, VETA zinahitajika sana ili tufikie lengo hili la ajira milioni nane. Kwa hiyo, niwaombe Wizara twende kufanya kazi kubwa. Katika jimbo langu tayari tumetenga maeneo yapo ya kutosha na tupo tayari kutoa ushirikiano unaohitajika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri kuhusu mitaala, tumelalamika sana, tumezungumza kuhusu elimu na Watanzania wengi wanaona kuna shida. Sasa wakati mwingine sit u kwamba kutoa *degrees* nydingi ni shida, lakini shida kubwa naiona katika suala la mitaala, mitaala yetu mingi ambayo tunaitumia, hasa ile ya *knowledge-based education and training* haiwezi kutusaidia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mitaala ya *competence-based education (CBET)* pamoja na *outcome-based* inaweza ikatusaidia. Mitaala hasa inayosimamiwa na *NACTE* inaweza kufanya vizuri sana. Kwa hiyo niombe sana Wizara iangalie

namna ya kuipa nguvu *NACTE* kuweza kusimamia mitaala hii. Na *process* ya utengenezaji wa mitaala, hasa katika *situation analysis* tuweze kwenda kuwekeza vizuri sana katika eneo hili. (*Makof*)

Niishauri pia Serikali kuangalia vizuri suala la uongozi au *management* ya elimu. Leo ukiona katika shule nyingi walimu wakuu ndio hao sasa wamekuwa manesi, wahasibu, wamekuwa pia kama *matron*. Sasa kazi hii inawafanya ile *core business* yao iweze kuwa *shifted*. Tuombe sasa katika hizi shule tupeleke wahasibu, manesi na watu wa kusaidia shughuli nyingine, wakuu wa shule washughulike na kazi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia shule zetu nyingi sasa na Wizara yetu tunaangalia sana suala la matokeo ya mitihani zaidi ya *process* ya ufundishaji. Naomba *management* ya elimu sasa i-focus kwenye *process* ya ufundishaji.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niombe sana Wizara iweze kuhakikisha wanazipatia *TCU* na *NACTE* nguvu zaidi zitusaidie katika ubora wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa David Ernest Silinde, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Kipanga, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia; mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kunipatia fursa hii kuchangia hotuba ya bajeti ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tumeona tutolee ufanuzi baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wakati wanachangia hotuba ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wamejaribu kuzitoa hapa ambazo sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI tunazigusia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja namba moja ambayo Wabunge wengi walichangia walikuwa wanaiomba Serikali ama kuitaka Serikali kukamilisha maboma ambayo ni nguvu ya wananchi, ambayo yalitokana na nguvu za wananchi huko katika maeneo husika. Na sisi kama ambavyo bajeti yetu ilivyopita, tumetenga fedha kwa ajili ya kukamilisha hayo maboma nchi nzima lakini kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano katika mwaka wa fedha 2021/2022, kwenye maboma ya maabara peke yake kwa shule za sekondari tumetenga bilioni 26.07 kwa ajili ya maboma 1,043. Lakini vilevile kwa ajili ya kukarabati na kukamilisha majengo ya shule za msingi tumetenga bilioni 23.154 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya shule za msingi 1,852. Na kwa ajili ya sekondari tumetenga bilioni 23 kwa ajili ya maboma 1,840. Kwa hiyo, hiyo ni hatua ya awali kuhakikisha kwamba tunaunga mkono nguvu za wananchi ambazo wamekuwa wakijitolea katika maeneo husika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Waheshimiwa Wabunge walijenga hoja hapa wakitaka mkakati wa Serikali wa kukabiliana na ongezeko la wanafunzi wa sekondari wanaotokana na elimu bila ada au elimu bila malipo ambao sasa tunaamini katika mwaka wa keshokutwa, kwa sababu sasa hiivi ukiangalia watoto wa darasa la sita tulionao ambao wanatokana na Sera ya elimu bila ada wako milioni moja na laki nane. Kwa hiyo, watakavyofika mwaka 2022 tutakuwa na watoto ambao wanatakiwa kwenda kidato cha kwanza mwaka 2023, ukifuatilia ili *pass rate* ya kila mwaka ya zaidi ya asilimia 80, zaidi ya watoto milioni moja na laki mbili wanatakiwa wajunge na kidato cha kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ndio maana kwenye bajeti yetu tumetenga fedha, kwa mwaka huu tutaanza na ujenzi wa shule mpya 300, lakini ndani ya miaka mitatu tutajenga shule 1,000 ambazo zitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 400,000 kwa hiyo, maana yake ukichanganya na idadi ya sasa tutakuwa walau tumeshapunguza hiyo kero ya wanafunzi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezielekeza halmashauri zote nchini kulingana na mapato yao ya ndani kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa. Na tumeweka *categories*, kwa mfano halmashauri zenyе kipato chini ya bilioni 1.5 kujenga madarasa 20 kila mwaka kwa kutumia fedha za ndani, kwenye halmashauri ambazo mapato yake ni katи ya bilioni 1.5 na bilioni 5 watajenga madarasa 40 kwa kutumia mapato ya ndani, na katika halmashauri zenyе mapato zaidi ya billioni 5 watajenga madarasa 80. Kwa hiyo, yote hii ni mikakati ya kuhakikisha kwamba tunaondoa hiyo kero ya madarasa katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la taulo za kike tuliona Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia, na sisi TAMISEMI tukaona ni vizuri tuka-*respond*. Tumeziagiza shule zote na tumeandika mwongozo kuhakikisha kwamba kwenye ile fedha ya *capitation grant*, asilimia kumi itatumika kwa ajili ya kununulia taulo za kike shulenii. Kwa hiyo, hilo nimeona tuliseme kwasababu ndio dhamira ya Serikali, na litakwenda kutekelezeka na sisi kama wasimamizi tutahakikisha hilo linafanya kazi yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna miradi mbalimbali ambayo ipo sasa hivi; tunakamilisha majengo, tunakarabati, tunaboresha, zikiwemo shule kongwe na zingine ambazo tumeziainisha kupitia Miradi kama ya *EQUIP*, *SEQUIP*, *Boost* na Shule Bora; tuna Miradi vilevile ya *EP4R*pamoja na *LINES II*. Kwa hiyo hii yote ni sisi Wizara ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI tukishirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, tunataka kuhakikisha mtoto wa Kitanzania anapata elimu bora na anakuwa na mazingira bora na sahihi.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rwamlaza.

## T A A R I F A

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa Naibu Waziri, Mheshimiwa Silinde, kwamba hiyo *capitation* inayopelekwa shulenii, shilingi 4,000 inabaki Wizarani, inabaki shilingi 6,000 kwenye shule. Nina mashaka kama shilingi 6,000 hiyo ambayo haitoshelezi hata kununua chaki katika shule kama inaweza kusaidia watoto katika kupata taulo za kike.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Silinde, unaipokea taarifa hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nafikiri Mheshimiwa Mbunge anafikiri labda ni shilingi 6,000 peke yake ndiyo inayokwenda shulenii kwa mwanafunzi mmoja; fedha tulizotenga kwenye bajeti kwa ajili ya *capitation* ya kwenda kule ni zaidi ya bilioni 298. Kwa hiyo fedha hiyo wewe *calculate* asilimia 10 ya hiyo fedha kwa ajili ya kwenda kununulia hizo taulo za kike kwa ajili ya kusaidia wananchi, kwa hiyo hilo ndilo lengo la Serikali na tumejipanga kulitekeleza kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, niwaombe mtakapokuwa mnapita kwenye ziara zenu katika shule waombeni taarifa, kila mkuu wa shule na mwalimu mkuu wamenunua taulo za kike kiasi gani kwa kutumia fedha ya *capitation*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwasababu katika shule siyo kwamba inakwenda 6,000 peke yake, hiyo 6,000 ni kwa mwanafunzi mmoja. Kwa hiyo, kama shule ina wanafunzi zaidi ya 1,000 na kuendelea maana yake unachukua ile 6,000 unazidisha mara 1,000. Kwa hiyo, kuna shule zinapata zaidi

ya milioni 30, kuna shule zinapata milioni 12, kwa hiyo inategemeana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa hivi kwenye hiyo *formula ya capitation grant* tunakuja na *formula* mpya kuhakikisha kunakuwepo na *minimum amount*. Kwasababu shule nyingine zina idadi ndogo ya wanafunzi lakini mahitaji ya kishule yanalingana. Kwa hiyo, tumeliangalia vizuri na tuko makini katika kulikamilisha hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimeona niyatolee hayo ufanuzi, na niunge mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Juma Kipanga, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, tutamallizia na mtoa hoja.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa fursa ya kuchangia hoja hii. Wachangiaji wengi wakati wakisimama hapa walikuwa wana-*declare interest* na wengi wao walikuwa ni walimu, na nimepata bahati ya kufanya kazi sasa na walimu, naomba ni-*declare interest* ya *professionalism* yangu, by profession ni *Quantity Surveyor*, kwa maana ya kwamba ni *QS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba nichangie hoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutumia fursa hii adhimu na adimu kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyenijalia afya njema na leo nimepata fursa ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini na kunituea katika nafasi hii. Ninampongeza kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuwaletaa maendeleo Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, sina budi kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushauri na maelekezo yao muhimu katika utekelezaji wangu wa majukumu ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru wewe na Mheshimiwa Spika kwa kuliongoza Bunge hili kwa hekima, busara na weledi mkubwa. Naishukuru pia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano mkubwa wanaotupatia; hii ni moja ya Kamati bora sana ambayo Wajumbe wake wana uelewa mpana katika sekta ya elimu na hivyo kuendelea kutoa ushauri muhimu katika kuboresha Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Prof. Joyce Lazaro Ndalichako, Mbunge, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa uongozi wake thabiti ndani ya Wizara. Pia namshukuru Katibu Mkuu, Dkt. Akwilapo; Naibu Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara kila mmoja kwa nafasi yake, kwa ushirikiano wanaonipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, naishukuru familia yangu kwa upendo na ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu. Pia nawashukuru sana wapigakura wangu wa Jimbo la Mafia kwa imani yao kubwa kwangu na ushirikiano ambao umesaidia jimbo letu kupiga hatua kubwa katika kipindi cha Awamu ya Tano na ya Sita ya Serikali yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo sasa naomba kutoa ufanuzi kwa baadhi ya hoja ambazo zimechangiwa na Waheshimiwa Wabunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja kuhusu umuhimu wa sayansi teknolojia na ubunifu; Waheshimiwa Wabunge wengi

walionesha umuhimu wa kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu kwa ajili ya maendeleo ya nchi. Serikali inatambua umuhimu wa mchango wa ubunifu na teknolojia katika kurahisisha na kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii na ni nyenzo ya kichocheo cha maendeleo ya haraka katika sekta ya huduma za jamii na uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanzisha Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) kwa lengo la kuibua, kutambua na kuendeleza ubunifu na ugunduzi wa teknolojia mbalimbali unaofanywa na Watanzania, hususan wale wa ngazi za chini. Mashindano haya yanawapa nafasi wabunifu na wagunduzi wa teknolojia kujitangaza na hivyo kujulikana na wadau wa ubunifu unaozalishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuanza kwa mashindano haya mwaka 2019, Serikali imefanikiwa kuibua na kutambua wabunifu wachanga 1,780 kati ya hao, wabunifu mahiri 1,030 wameendelezwa na Serikali ili ubunifu na teknolojia walizoanzisha zifiki hatua ya kubiasharishwa na hivyo kuongeza fursa za ajira kwa vijana na kuchangia kwenye Pato la Taifa. Aidha, Serikali kuititia *COSTECH* imeanzisha vituo atamizi 17 kwa ajili ya kukuza na kuendeleza ubunifu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja kuhusu Serikali kuongeza vyuo vya *VETA* kwa kila mkoa na wilaya; Serikali ina mpango wa kuhakikisha kunakuwepo na Chuo cha Ufundisti katika kila mkoa na wilaya nchini. Kwa sasa vyuo 42 vinaendelea na mafunzo, pamoja na hivyo, Serikali inaendelea na ujenzi wa vyuo 29 vya wilaya na vyuo vine vyua ufundisti vya mikoa ambavyo viro katika hatua mbalimbali za ujenzi. Hata hivyo, Serikali itaendelea na utekelezaji wa ujenzi wa vyuo vya *VETA* vya wilaya kwa kadri fedha zitakavyopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja kuhusu Wizara kuboresha vyuo vya ufundisti ili viweze kuendana na

maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu. Serikali inaendelea na kuboresha na kuimarisha vyuo vya ufundi kwa kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia pamoja na kununua vifaa na mitambo ya kisasa. Kwa sasa Serikali kupitia mradi wa *A STRIP* naendelea na ujenzi wa vituo mahiri (*Centers of Excellence*) katika Chuo cha Ufundi Arusha, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam katika Kampasi za Dar es Salaam na Mwanza na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (*NIT*) katika Nyanja za nishati, usindikaji wa ngozi, usafiri wa anga na TEHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilika, vyuo hivi vitakuwa na hadhi ya kimataifa vinavyowezza kutoa ujuzi unaoendana na soko la ajira na hivyo kuvutia wanafunzi wa ndani na nje ya nchi. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha vyuo vingine vya ufundi nchini katika bajeti yake ya maendeleo ili kuhakikisha vyuo hivyo vinatoa elimu stahiki inayoendana na mahitaji ya soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja kuhusu Serikali kuwa na utaratibu wakufanya ufuatiliaji wa wahitimu baada ya kumaliza masomo (*tracer study*); Serikali impokea maoni na itaendelea kuhakikisha kuwa ufuatiliaji wa wahitimu unafanyika na unakuwa endelevu ili utumike katika kuboresha mitaala ya mafunzo na hivyo kukidhi mahitaji ya soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, vyuo vikuu mbalimbali, Baraza la Elimu ya Ufundi (*NACTE*), Mamlaka ya Ufundi (*VETA*) na Taasisi ya Sekta Binafsi (*Tanzania Private Sector Foundation*) na mamlaka nyingine nchini hufanya *tracer studies* mara kwa mara kwa baadhi ya fani ili kupata taarifa za wahitimu hao, waajiriwa na waliojiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja kuhusu Serikali kuwa na utaratibu wa kufanya utafiti wa soko la ajira ili kubaini mahitaji...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kengele imeshagonga.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kipengele cha mwisho cha udhibiti ubora; Serikali kupitia miradi yake ya kuendeleza elimu *Lens* na imekuwa ikituwezesha idara ya udhibiti ubora wa shule kutekeleza majukumu yake kwa kufanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeongeza bajeti ya wadhibiti ubora kutoka bilioni 5.2 mpaka bilioni 5.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, nawashukuru sana kwa kunisikiliza, ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, mtoa hoja uje uhitimishe hoja yako.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuhitimisha hoja yangu.

Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama tena hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kuhitimisha hoja hii ambayo tuliiwasilisha jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kumshukuru Mheshimiwa Spika, Job Yustino Ndugai, kwa kuongoza mjadala wa hoja yangu jana, lakini pia nakushukuru sana wewe ambaye umekaa katika Kiti hiki tangu asubuhi na mpaka sasa ninapohitimisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, nawashukuru sana kwa michango mizuri sana ambayo mmeitoa, hakika mmekuwa na michango mizuri ambayo inaonesha dhamira yenu ya kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto zilizopo katika sekta ya elimu na kuhakikisha kwamba elimu ambayo

inatolewa katika nchi yetu inakidhi mahitaji katika Taifa letu na kimataifa. Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishukuru Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Ukiangalia taarifa ya Kamati imesheheni uchambuzi wa kitaalam, imesheheni maoni na mapendekezo ambayo wote kwa pamoja, niwaambie tu Wajumbe wa Kamati, Serikali tumepokea mapendekezo yenu na tutakwenda kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda sitaweza kujibu hoja moja baada ya nyininge, lakini niwahakikishie kwamba maoni yote ya Kamati tumeyachukua kwa uzito kama ambavyo nao wameyafanya kazi kwa uzito mkubwa. Kwa hiyo, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na si vibaya nikisema tu kwamba Kamati ile ukienda pale lazima uwe umejipanga, wanachambua kwelikweli. Kwa hiyo, Kamati ya Huduma za Jamii iko vizuri, tunawashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 63 wamechangia hoja yangu ambapo Wabunge 58 wamechangia kwa kuzungumza na Wabunge watano wamechangia kwa maandishi. Michango yote ililenga kuhakikisha kuwa elimu yetu inaendelea kuboreshwa kwa kiwango stahiki na kuhakikisha kwamba tunatoa wahitimu ambao wameiva vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote sitaweza kuzijibu hoja zote, wengine walikuwa na dakika na tano na wengine saba lakini anachangia mambo mengi. Kwa kweli naona walikuwa wamejipanga vizuri kwenye Wizara yangu ya Elimu naendelea kuwashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa pongezi ambazo wamezitoa katika Wizara yetu ya Elimu. Hakika tumefarijika sana kuona kwamba mnatambua kazi ambayo tunafanya kama Wizara ya Elimu. Kwa hiyo, niwahakikishie kwamba pongezi ambazo mmezitoa kwa Wizara zitakuwa chachu kwetu ya kwenda kufanya Zaidi. Pongezi ambazo mmezitoa zitakuwa chachu kwetu ya kwenda kufanya kazi maoni na mapendekezo ambayo mmetupatia. Kwa hiyo, tunawashukuru sana na tunaahidi kwamba tutajituma zaidi ili kuhakikisha kwamba tunatekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyenyekevu mkubwa, naomba pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa pongezi ambazo wamezitoa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mpewda Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Hakika tunashukuru sana kwa namna ambavyo mmepokea uamuzi wake wa kuondoa tozo ya asilimia 6 katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwahakikishie kwamba Mheshimiwa Rais ameonyesha njia, yupo tayari kusikiliza na kufanya maamuzi. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge tumuunge mkono ili adhma yake ya kuweza kuwatumikia Watanzania na kutuletea yaliyo mema zaidi iweze kutekelezwa. Kwa hiyo, nimepokea kwa unyenyekevu mkubwa salamu na pongezi kutoka kwa Waheshimiwa kwa niaba ya Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa, naomba niende kwenye hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezisema na nitakuwa sitaji majina kwa sababu muda hautoshi kuwataja wote isije ikaonekana kwamba nyingine nimeziacha, lakini nimejaribu kuchukua hoja ambazo zilichangiwa na watu wengi na ndiyo nimeona nianze kuzitolea ufanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, ni kuhusiana na mfumo wa elimu. Waheshimiwa Wabunge wengi ambao

wamezungumza, wamezungumzia mfumo wa elimu na wamezungumzia haha ya mfumo wa elimu kujikita katika falsafa ya elimu ya kujitegemea. Waheshimiwa Wabunge wameonyesha kwamba wangependa elimu yetu iweze kumjengea mwanafunzi uwezo wa kujiamini, imjengee uwezo wa kujifunza zaidi kwa wengine lakini pia, iwajengee uwezo wa kufanya kazi za uzalishaji mali mara baada wanapohitimu masomo yao. Pia suala la mitaala limezungumzwa na Wabunge wameomba kuwe na Mjadala wa Taifa wa kujadili mitaala na kuangalia ni namna gani tunakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na mfumo wa elimu yetu, Wizara imepokea maoni ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge na hatuoni tatizo lolote la kuwa na mjadala kuhusiana na suala la elimu. Kwa hiyo, tutafanya utaratibu, tutafanya mjadala na tutaomba Waheshimiwa Wabunge nao wawe ni sehemu ya kuchangia kwamba tunataka kwenda wapi. Mtaona changamoto ambayo inajitokeza kwa sababu hata katika michango huyu anasema tufanye hiki, huyu anasema tufanye kile, kwa hiyo, tutasikiliza na mwisho wa siku tutaona kile ambacho kweli kikitekelezwa kinakwenda kufanya vijana wetu watoke wakiwa wameiva vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kukubaliana na hoja ya kufanya mjadala kwa sababu ukiangalia ile Sera ya Elimu ni ya tangu mwaka 2014, muda haujapita mrefu sana lakini tangu imeanza kulikuwa na changamoto za hapa na pale. Ndiyo maana kuna baadhi ya matamko ambayo yapo kwenye sera lakini hayajaanza kutekelezwa. Kwa hiyo, Serikali imekubaliana tutafanya mapitio.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia na mimi niungane na baadhi ya wachangiaji waliosema pamoja na kufanya mapitio isionekane kwamba sasa elimu ya Tanzania si mali kitu, si kweli ndugu zangu, elimu yetu ni nzuri, ina changamoto za hapa na pale na hayo ndiyo tunaenda kuyarekebisha. Tusije tukajenga dhana kwamba yaani elimu ya Tanzania

haifai na inafika mahali labda mtu anaona kwamba hakuna sababu ya kumpeleka mtoto shule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi huwa nasikiliza michango humu, bahati nzuri wanaosema kwamba hakuna haja ya kuendelea na masomo zaidi ya darasa saba, wengine hata nimewasaidia kuwatafutia watoto wao vyuo vikuu. Kwa hiyo, najua ni maneno tu ambayo wanayasema kwa sababu nawafahamu wengine ni darasa la saba na wanafanya vizuri lakini wanawasomesha watoto wao tena kwa wivu wote na wanasomesha katika shule nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, isije ikatafsiriwa kwamba wanachokisema ndicho wanachokiamini. Naomba mimi nisimame kuwaambia Watanzania elimu ni ufunguo wa maisha, ni mwanga na ni tochi inakuonyesha uende wapi. Tusifike mahali kama taifa tukaanza kubeza kwamba elimu haina maana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niwapongeze sana wale ambaopengine hawakwenda shule kwa sababu moja au nyiningine lakini wakafanikiwa lakini tuijulize wapo wangapi? Tunapochukulia kama hicho ni kigezo tuijulize wapo wangapi? Kwa hiyo, kweli kuna watu ambaowamefanikiwa sana lakini pia si wengi kama ambavyo tunataka kuwaaminisha Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi kama Waziri nimepewa dhamana ya elimu naomba watoto wote waende shule, elimu ni haki ya kila mtoto wa Kitanzania. Tuhakikishe watoto wanasona shule na Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ya watoto kusoma shule lakini yule ambaye anakipaji, ndiyo maana tunayo pia *section* ya ubunifu ambapo tunawaendeleza vijana wetu ili yule ambaye Mwenyezi Mungu amemjalia kipaji na kipawa kama kuna njia nyiningine ambayo anaweza akafanikiwa kwa haraka zaidi mifumo yote hiyo katika elimu yetu ipo; tuna elimu rasmi na elimu nje ya mfumo rasmi. Kwa hiyo, niliona ni muhimu hilo suala nilizungumzie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la kupitia mfumo wa elimu litaenda sambamba na kupitia Sera yetu ya Elimu, mitaala na Sheria ya Elimu. Ombi langu, naomba Wizara tupewe nasafi ya kufanya kazi, mambo mazuri hayataki haraka. Suala la kupitia Mfumo wa Elimu inabidi ufanye utafiti, tuangalie na washindani wetu, mazingira yetu na *resource* zetu, kwa hiyo, tusitegemee kwamba tukirudi mwakani tuna mfumo mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niwahahakishie Waheshimiwa Wabunge kazi hii inakwenda kuanza kabla hata ya Julai. Tumeshakaa na Katibu Mkuu, fedha kidogo ambazo zipo wazitumie ili huu mjadala uanze kabla hata ya Julai. Kwa hiyo, nachotaka kusema ni kwamba kazi ya kufanya mapitio tutaianza. Hata hivyo, naomba niwaandae kisaikolojia, tunataka tuifanye kisawasawa, kwa sababu kama tumebadilisha sera mwaka 2014 leo hili tunasema tubadilishe tena, tutakuwa ni nchi ambayo kila siku tunabadilisha mambo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ya Marekani mwaka 1983 ilifanya mapitio makubwa ya sekta ya elimu kama ambayo sasa tunataka kuyafanya katika nchi yetu. Utafiti wenyewe ulichukua mwaka mmoja na nusu lakini sisi mtu anategemea mwakani tumekuja na mitaala mipy. Jambo hili tutalifanya lakini tutalifanya kwa weledi, kwa umakini na kuna mengine ambayo tutaanza kuyatekeleza wakati tunafanya mapitio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa niwahahakikishe kwamba tuna dhamira ya dhati kwa sababu hata sisi tunaosimamia elimu hatupendi kila siku kusikia elimu yetu ikilalamikiwa, tunafanya vizuri lakini kuna mambo ambayo tunatakiwa kuyarekebisha. Tuko tayari kusikiliza maoni ya wadau, tupo tayari kuyafanya kazi na naamini tutatoka vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakati tunaendelea na huu mchakato ambao nimeuzungumzia kidogo mtupe muda tufanye kitu cha uhakika. Kuna mambo

mengine ambayo tutaanza kuyafanya, kwa mfano, kuimarisha mafunzo ya ufundi, tayari tuna shule zetu za ufundi, kwa hiyo, niwahahakishie kwamba suala la kuimarisha mafunzo kwa vitendo hilo tayari tumelianza. Shule zetu zote za ufundi zile tisa nilizozitaja, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge aliyesema kwamba ni chache ni kweli, lakini nasema ukweli ndiyo zilizopo. Kwa hiyo, tutaanza na hizo tisa zilizopo, tayari tumezinunulia vifaa, tumezipelekea walimu wa kutosha na sasa hivi tuna fedha nyingine milioni mia moja katika kila shule ya kuendelea kuziimarisha. Kwa hiyo, hilo ni suala ambalo tumelianza na tutaendelea kulifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika vyuo vyetu vya VETA tutahakikisha tunaimarisha mafunzo kwa vitendo. Wanafunzi waende viwandani na kwenye makampuni kujifunza. Niwapongeze VETA wameanza ushirikiano huo, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam nao wameanza, wana kitu ambacho wanaita dhana ya mafunzo viwandani. Kuna mabasi yao mnaweza kuyaona yameandikwa *Teaching Factory*, hayo ni mabasi ambayo yanakuwa yanawachukua wanafunzi kuwapeleka kwenye viwanda na tutaendelea kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tutaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo imekasimiwa jukumu la kuendeleza ujuzi na tunashirikiana vizuri na dada yangu *Chief Whip*, Mheshimiwa Jenista Mhagama.

Kwa hiyo, niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu akina mama tukisamama, tunasimama kweli kweli, kwa hiyo, suala la ujuzi dada yangu Jenista Mhagama nadhani umesikia vizuri michango ya Wabunge, bajeti yangu ikipita hapa naomba kama tulivyokubaliana tukae kikao wataalam wa Ofisi ya Waziri Mkuu na wataalam wa Ofisi ya Wizara ya Elimu kuangalia masuala ya kujenga ujuzi yanayoteklezwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na yale ambayo tunayatekeleza Wizara ya Elimu ili kama nchi tuwe na mfumo ambao utakuwa umeunganishwa kwa pamoja. Kwa hiyo, hilo tunakwenda kulifanyia kazi mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kutoa wito kwa taasisi za elimu kuhakikisha zinazingatia mafunzo kwa vitendo. Nchi yetu inajenga uchumi wa viwanda, naomba *Vice Chancellors* (Makamu Wakuu wa Vyuo) wajitafakari hivi ni wangapi ambaao wanatembelea viwanda vilivyopo Tanzania ili kuhakikisha kwamba ujuzi unaotakiwa kwenye viwanda ndiyo ule ambaao wanautoa katika taasisi zao. Kwa hiyo, niwasih i sana Makamu Wakuu wote wa Vyuo na taasisi zote zinazotoa elimu kuhakikisha kwamba suala hili la kufanya mafunzo kwa vitendo linaanza kutekelezwa mara moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa ni eneo la kilimo na ujasiriamali. Naomba tu niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba masomo haya ya kilimo na ujasirimali kwa sasa yanafundishwa katika somo la Stadi za Kazi. Hata hivyo, tumepokea michango yenu, tutaaangalia namna ya kuyaboresha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi kwamba Waheshimiwa Wabunge wanazungumzia suala la elimu ya kujitegemea (suala la kilimo) kwa sababu wapo baadhi ya wazazi ambaao mtoto wake akiambiwa kwenda shamba anapiga simu kwa Waziri analalamika kwamba sasa hivi watoto wetu wanalinishwa. Kwa hiyo, nimefurahi kwamba ni mtazamo wa nchi kwamba elimu ya kujitegemea ni muhimu, elimu ni kazi na watoto shulen i wawe tayari kufanya kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ambalo linahusiana na hili suala la kazi ni utoaji wa chakula shulen. Waheshimiwa Wabunge wamezungumza na mimi kwa kweli niwashukuru sana kwa kuwajali watoto kwa sababu wakiwa na njaa ni ukweli kwamba hawawezi wakasoma. Kwa hiyo, suala hilo ni la muhimu sana na Wizara tayari imetoea mwongozo (kitabu hiki hapa) cha namna ya kutoa chakula na lishe shulen.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Waraka wetu Na. 1 wa mwaka 2016 wa Utoaji Elimu Bila Malipo tulisisitiza pia suala

la utoaji wa chakula shuleni. Kwa sababu Bunge hili ni jipya niahidi kwamba nitagawa kwa Waheshimiwa Wabunge ili watusaidie kuwa mabalozi kwa sababu imeainishwa vizuri na kwa sababu ya muda siwezi kwenda ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala la uwepo wa chombo kimoja kinachosimamia elimu ya juu. Ni kweli kwamba sheria iliyoanzishwa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu imeipa mamlaka ya kusimamia elimu kuanzia ngazi ya cheti, *degree* mpaka na ngazi ya udhamivu lakini pia Tume ya Vyuo Vikuu imepewa mamlaka hayo, kwa hiyo, kuna mwingiliano wa kimajukumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mapendekezo pia kwamba hii vyuo vya kati ambavyo vinatoa *degree* vijikite katika kutoa utaalamu katika fani ambazo wallanzishwa. Kwa sababu mmetupa kazi ya kufanya mapitio na kuwa na mjadala, naomba niwahakikishie katika kufanya mapitio suala hilo tutalizingatia kuhakikisha kwamba tunapunguza vyuo ambavyo vinatoa *degree*. Kwa sababu sasa hivi kila chuo cha kati na chenyewe kinatoa *degree*. Kwa hiyo, tumepokea michango yenu na tutalifanyia kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusiana na vyuo vikuu kuchelewa kuwasimamia wanafunzi na kusababisha wanafunzi kuchelewa kumaliza na kulazimka kulipa tena ada, jambo hili halipendezi hata kidogo. Nichukue nafasi hii kuviagiza vyuo vikuu hasa Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuu vyote vya umma na vya binafsi kuweka mfumo mzuri wa kufuatilia wanafunzi wanaoenda kusoma hasa katika ngazi za uzamili na uzamivu na kuweka utaratibu wa kuwafualia walimu ili kujua kulikoni na waanze na kufanya tathmini, je, ni katika *faculty* zote au kuna baadhi ya shule ambazo zinachelewa na wachukue hatua mahsus. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo vikuu naviheshimu sana kwa sababu na mimi nimetoka huko, ni vyuo ambavyo wanafanya kazi kwa misingi na taratibu na ndiyo maana hamuwezi mkaniona naenda kukagua ufundishaji katika vyuo

vikuu. Hata hivyo, kwa malalamiko yaliyopo sasa hivi, naomba niwahahakishe kwamba sasa mimi mwenyewe nitafanya kazi ya kufuatilia katika kila chuo kuangalia tatizo nini ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa lakini jambo hili halikubaliki hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limezungumzwa tena kwa uchungu sana ni suala la kuanzisha Chuo Kikuu cha Kilimo cha Teknolojia cha Mwalimu Nyerere Butiama. Mwalimu Nyerere Baba wa Taifa kwa kweli alituwekea misingi mizuri, tunamheshimu sana na tunamuenzi. Kwa hiyo, Wizara ya Elimu haiwezi kufanya utapeli katika eneo ambalo anatoka Muasisi wa Taifa hili, Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kutumia muda kueleza lakini najua tu ni kwa sababu wanataka kutoa *pressure* kwa Serikali lakini hata Waheshimiwa Wabunge wanaouliza wanafahamu changamoto zilizokuwepo ambazo zimechelewesha kuanzishwa kwa chuo hiki na nyingine zinatokana na mahali wanakotoka. Waswahili wanasesma yaliyopita si ndwele, bahati nzuri leo hii wameuliza swali hili Bungeni tukiwa tumeshakamilisha changamoto zote zilizokuwepo, kwa hiyo, sasa tupo tayari kusonga mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kitabu changu cha hotuba katika miradi ya Wizara ya Elimu, tuna Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Juu ambapo tumetenga Dola za Kimarekani milioni 42 kwa ajili ya kuanzisha Chuo cha Mwalimu Nyerere. Niseme tu kwamba majengo ya sekondari hayawezi kuwa majengo ya chuo kikuu maana walikuwa wanasesma majengo yapo lakini wenyewe wamesema ile ilikuwa ni sekondari. Hadhi ya chuo kikuu na hadhi ya sekondari ni vitu viwili tofauti. Kwa hiyo, niwatoe hofu, jambo hilo Serikali tunalifuatilia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine dada yangu Mheshimiwa Jacqueline Msongozi alizungumzia suala la Chuo cha JUCO na akawa amesema kwamba leo shilingi yangu

ataishika, dakika moja tu asinishikie shilingi. Suala la Chuo cha *JUCO* ni kweli kilianzishwa mwezi Julai 2013, lakini kutokana na changamoto za uendeshaji katika kikao cha 37 cha Bodi ya Wadhamini ya Vyuo Vikuu cha Kikatoliki Tanzania maana kinamilikiwa na Wakatoliki, walikaa tarehe 12 na tarehe 13 Februari, 2019 wakaazimia kwamba wasitishe kuendesha chuo kwa sababu walikuwa na vyuo karibu kila mkoa, kwa hiyo, gharama za uendeshaji zikawa kubwa. Kwa hiyo, tumekisitisha kutokana na ombi kutoka kwenye Bodi ya Wadhamini ya Chuo Kikuu hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hoja yake kwamba kwa nini Serikali haiviungi mkono vyuo binafsi, Serikali inaviunga mkono vyuo binafsi. Tunapotoa mafunzo namna ya kuendesha hivi vyuo tunawakaribisha kwa gharama ya Serikali Wahadhiri kutoka vyuo vikuu binafsi. Nimhakikishie tu dada yangu Mheshimiwa Jacqueline Msongozi kwamba Serikali inathamini elimu ya juu na tunathamini pia viongozi wa dini hatuwezi kuwafanya uharamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niwaambie Waheshimiwa Wabunge wamesikia kengele lakini mambo ya kuwajibu yalikuwa mengi, michango ilikuwa ni mizuri lakini sasa siwezi kuomba muda wa ziada nitakuwa nimevunja Kanuni. Naomba tu mridhike kwamba hoja zenu zote tutazijibu kwa maandishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, kwa heshima kubwa naomba sana mtuidhinishie mafungu yetu ili tukatendee kazi maoni na mapendekezo ambayo mmeyatoa. Naomba sana Waheshimiwa Wabunge wote muunge mkono bajeti ya Wizara ya Elimu ili kazi iendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsanteni sana, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, tutaendelea na utaratibu wetu.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 46 – WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Kifungu 1001 – *Administration & Human Resources Management*.....Sh. 7,782,796,064

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki ndicho chenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri na nimeletewa hapa majina ya Waheshimiwa Wabunge wanaohitaji ufanuzi. Mheshimiwa Issa Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ninayo nia ya kushika mshahara wa Mheshimiwa Waziri kama sitopata ufanuzi mzuri juu ya haya. Katika mchango wangu wa msingi siku ya jana, nilieleza juu ya changamoto ya ukuaji wa ubora wa elimu unaosababishwa na upungufu wa wataalam wabobezi; maprofesa na hawa wenye shahada ya uzamivu na hasa kwenye hadhi za wataalam hawa. Imekuwa ni changamoto sana kwa hawa wataalam kupandishwa vyeo na msingi ili wapande vyeo, miongozo yao inasema kutoa machapisho mbalimbali, lakini sasa hivi ni muda mrefu, hata wakitoa machapisho hawapandi vyeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo likiwa ni moja, sasa swalilangu kwa Mheshimiwa Waziri, kama misingi hiyo haizingatiwi na sasa kujenga majengo ya shule au vyuo tunaona ni bora kuliko kuwapa hadhi hawa maprofesa, na ndiyo

inasababisha wakati wa uchaguzi wengi wanakuja kwenye haya mambo yetu huku:-

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha stahili za wahadhiri zinaboreshw na hadhi zao zinalindwa? (*Makof*)
- (b) Mheshimiwa Waziri atuambie...

**MWENYEKITI:** Huwa hoja ni moja tu Mheshimiwa.

**MHE. ISSA JUMMANNE MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ufanuzi kwa hoja hiyo.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru kaka yangu Mheshimiwa Mtemvu kwa kuona umuhimu wa wahadhiri na wataalam wetu kupata stahiki zao kwa wakati kulingana na vigezo vilivyowekwa. Ni kweli kwamba kumekuwa na changamoto katika kipindi hiki kidogo ambacho baadhi ya watumishi wamekuwa hawapandi madaraja kwa wakati. Hii siyo kwa wahadhiri peke yao, hata hivyo nashukuru kwamba Mheshimiwa Rais ameliona hilo na wakati wa Mei Mosi amezungumzia suala la kupandisha madaraja na wale ambao walikuwa wameshaahidiwa watapandishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naahidi kwamba nitasimamia ili kuhakikisha kwamba wale ambao tayari walikuwa na barua, lakini hazikutekelezwa, wanapata stahiki zao kama ambavyo Mheshimiwa Rais ameshatoa maelekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Issa Mtemvu ametingisha kichwa kuashiria ameafiki. Mheshimiwa Eric Shigongo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo nia ya kushikilia shilingi ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana na suala zima la *recognition of prior learning*. Huu ni mfumo ambao unampa fursa mtu mwenye kipaji au mtu yejote yule mwenye elimu ambayo haiko *formal* lakini amefanya mambo makubwa, aweze kupata elimu ya chuo kikuu. Mfumo huu uko sehemu mbalimbali za dunia. Huko Uingereza wanauita *Recognition of Prior Learning*, Australia wanauita *Recognition of Prior Learning* vile vile na ukienda nchi nyingine kama Marekani vile vile wanao mfumo wa namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Tanzania ulikuwepo. Kama nilivyozungumza kwenye mchango wangu wa msingi, nilisema kwamba mimi ni tunda la mfumo huo ambao umeniwezesha kupata *degree* ya Chuo Kikuu kutoka Darasa la Saba. Sasa, Mheshimiwa Waziri aliuondoa mfumo huu mwaka 2017, nami ni *batch* ya mwisho ya watu waliopata elimu kwa mfumo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatakuwa tayari kutoa fursa kwa vijana masikini wa nchi hii ambao kwa sababu ya dhiki au historia za maisha yao hawakupata elimu ya chuo kikuu, lakini wana ujuzi, wamegundua vitu mbalimbali, sitakuwa tayari kuruhusu shilingi ya Mheshimiwa Waziri katika suala la *Recognition of Prior Learning*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka watoto masikini wa nchi hii, watu ambao hawakupata fursa ya kusoma kama Mheshimiwa Musukuma, ndugu yangu Mheshimiwa Kibajaji nao wapate elimu ya chuo kikuu. Ahsante sana kwa kunisikiliza. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Sasa hiyo elimu kwani mtu anarukia tu chuo kikuu bila vigezo! Maana umeanza kutoa mifano hapa tena inayoleta utatanishi; yaani kwamba mtu atatoka darasa la saba, mwingine aende na sekondari, halafu mwingine apitilize bila vigezo! Wewe uliwekeza vigezo na ukavipita hivyo. Si ndiyo!

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Sasa ukianza kutaja mifano ambayo haina vigezo vyako, unatupa wakati mgumu kidogo. Mheshimiwa Waziri, ufanuzi.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza naomba tu niweke kumbukumbu sawa kwa sababu, Mheshimiwa Eric Shigongo anasema kwamba Waziri ndio aliondoa kigezo.

Naomba tu niseme kwamba, sheria haijanipa mamlaka ya kufanya hivyo. Mamlaka ya kuweka vigezo vya kujunga na vyuo vikuu iko kwenye Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania. Kwa hiyo, kwa kutumia mamlaka yake Tume ya Vyuo Vikuu ndio iliondoa.

Mwenyekiti Mweyekiti, ni kweli kwamba Tume ya Vyuo Vikuu ilichukua kigezo hiki kama majoribio na walikifanyia kazi, lakini kikawa na changamoto. Walikifanyia kazi na baada ya miaka mitano walivyofanya tathmini kwanza waliona kuna udanganyifu mkubwa, *control* yake ni ngumu kwa hiyo, wakaamua kukiondoa kwa mujibu wa mamlaka waliyopewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa tu pia kuonyesha kwamba tusiwe tunajichanganya. Maana yake huku tunasema kwamba tunathamini sana makaratsi. Sasa kama mtu ana ujuzi na kila kitu anacho, hicho cheti cha chuo kikuu ambacho tunasema vyuo vyetu vikuu ni bure, mwanafunzi akienda kule hamna kitu ni makaratsi, si huyu aendelee na ujuzi wake!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani katika mapitio, haya mambo tuyaangalie vizuri. Ameshabobea bila hata kwenda shuleni, sasa anataka makaratsasi ambayo wanasesma hayana faida, ya kazi gani? Kwa hiyo, nadhani wakati mwingine mnatushauri lakini kama Serikali unasikiliza, sasa unasema kwamba tufanyeje! Huku tunasema tunaabudu sana makaratsasi, sasa mtu ameshafanikiwa,

ameshabobeaa tuweke mifumo ya kuwatambua hata kama ni ajira, tuwatambue. Mimi nadhani hilo ndio jambo la msingi, kuliko sasa kila mtu mpaka awe na makaratasii. Tunarudi kule kule ambako siku zote mbili hizi mlikuwa mnaondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Shigongo naomba kwa sababu tumesema tunafanya mapitio, tutakapokuwa tunafanya mapitio na hili tutaliangalia. Naomba nirudishie shilingi yangu ili tufanye mapitio, tuwe na mfumo ambao kila mtu atajivunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Shigongo, naona umesimama.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza kusema sijardhishwa sana na majibu ya Mheshimiwa Waziri. Nitakueleza kabisa mfano halisi wa kinachoendelea. *TCU* ndiyo walionipa mimi barua kwamba nafaa kwenda kusoma chuo kikuu. Nikasoma miaka mitatu nikamaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha, kwa mfano nimetaka kufanya *Masters University* of Dar es Salaam, ingawa nimefaulu vizuri chuo kikuu, UDSM wamenikataa, wanataka cheti cha *Form Four* ambacho mimi sina. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siko tayari kwa sababu hii fursa iko dunia nzima. Tuwape watu fursa ya kupata elimu, kwa sababu, watu wanalipa fedha zao, wala hawahitaji mkopo wa Serikali. (*Makofii/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Nadhani, Waheshimiwa Wabunge...

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Ulikuwa umeshakaa.

Waheshimiwa Wabunge, wakati Mheshimiwa Waziri anatoa maelezo, nadhani hii sentensi yake ya mwisho

amesema, wakati wanafanya mapitio ya mfumo mzima wataangalia na hilo nalo ambalo baada ya kulifanyia kazi kwa miaka mitano, wamegundua kuna changamoto.

Unajua wakati mwingine jambo linaweza kuwa limeenda vizuri kwa mtu mmoja, lakini lisiende vizuri kwa mtu mwingine. Mtu anaweza akaleta uzoefu kwa mfano, ye ye ni mkulima na analima miaka yote na ana shamba lake mahali. Akienda chuo chetu cha kilimo pale Morogoro, naye ana shamba lake na wanalikagua kila mwaka, naye akipewa ile karatasi ndiyo yale tunarudi tena hapo hapo kwa Mheshimiwa.

Nafikiri tuwape fursa Wizara wakafanye hayo mapitio na Mheshimiwa Shigongo utakuwa ni mmoja wa wadau wa kutoa mawazo yako. Ila sasa hii hoja ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, pengine kukataa, nadhani huwa wanakatalia watu wengi tu kulingana na nafasi na vigezo walivyonyavyo wao. Kwa hiyo, hilo nisingependa tuliweke kana kwamba...

Mheshimiwa Waziri naona anataka kutoa ufanuzi tena.

#### **WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nitazungumzia tu hili suala la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuwakataa wanafunzi. Labda niseme tu, Tume ya Vyuo Vikuu inaweka kiwango cha chini, lakini chuo kama chou, mamlaka ya kuangalia taaluma yako kwenye *senate* za chuo. Kwa hiyo, seneti zina mamlaka ya kupanga vigezo kulingana na mazingira ya chuo chenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, kwanza, wamekuwa wanaagiza Serikali iweke madaraja ya vyuo vikuu kwamba, labda hii anaenda mtu wa *class fulani*. Kwa hiyo, ni utaratibu ambao unawekwa na *senate* za vyuo vikuu na kama ambavyo kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja anasema elimu imetulia. Ni kwa sababu Waziri anaafuata sheria. Siingilia mimi

senate. Kama senate zimepangwa mtu akija, nawaambia ndiyo utaratibu uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo ya vigezo kama unavyosema, ni vyuo vyenyewe kupitia senate zao zinaweka. Nami naomba kwa kweli tusifike mahali tukaanza kuingilia mpaka masuala ya taaluma. Tuviheshimu vyombo ambavyo tumevitungia sisi sheria. Kwa hiyo, kama vyombo vyetu vitakuwa na shida, turekebishe sheria, lakini tungewaacha wafanye kwa manufaa ya nchi yetu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Hapa ninayo majina mengine. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, mimi ni mmoja wa watu wanaotolewa mfano. Professor kanitolea mfano, ni kweli alinitafutia nafasi ya mtoto wangu; na mjumbe mwininge alisema pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi *tunao-challenge degree* na elimu kubwa siyo kwamba hatupendi elimu. Mfano mzuri, mimi najenga shule niikabidhi Serikali. Sasa ukini-judge kwa namna hiyo, mimi siko kwenye maana hiyo. Maana yetu ni hivi, watu wengi mliopata *u-professor ma-degree* makubwa matokeo yenu kwenye jamii ambayo hatukusoma hatuyaoni. Nanyi wenyewe ni mashahidi, mpaka mmetengenezewa na *PCCB*. Kwani *PCCB* ilishawahili kushika darasa la saba! Inakamata wasomi hao hao. Sasa ni vizuri tuelewane, tusionekane Wabunge wa Darasa la Saba tunachukia elimu. (*Makofii*)

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiruswa, kwa kawaida, kwa sababu sasa hivi hachangii, anataka ufanuzi, kwa hiyo, kama ni hoja yake, tutaenda mpaka tuanze kuchangia, pale ndiyo tunaanza kupeana taarifa. Mheshimiwa Musukuma

kengele imegonga. Nakupa sekunde 30 weka hoja yako mezani, sijaelewa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni hii. Ziko shule hizi za *private* nyingi ambazo zinasajili watoto wetu katika shule yao kwa mfano kwa jina la Musukuma; wana *division One* vizuri tu, wanapofika pale wakianza kufanya mtihani wanachuja watoto 30. Kwa mfano 30 mpaka 35, hawana shule mbadala, wanakuwa na shule ya *briefcase* ambayo haina hata majengo. Hiyo ni kwa ajili ya kufanyia mtihani na kuchukulia namba moja Kitaifa. Sasa na aliyetao hivyo vibali vya kufungua shule ni *professor* na anaenda kukagua shule...

**MWENYEKITI:** Haya. Muda wako ulikuwa umeisha. Ngoja atoe ufanuzi. Mheshimiwa Waziri, ufanuzi.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Musukuma kwa sababu ni kweli amekuwa anafuatilia mahali ambapo watu wanafanya ujanja ujanja kwenye sekta ya elimu. Nakiri kwamba wapo baadhi ya wamiliki wa shule binafsi ambao siyo waaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana huu udanganyifu unaanza hata kuingia katika shule za Serikali. Kwa mfano, katika usajili wanafunzi wanaofanya mtihani wa darasa la saba mwaka huu tulipata taarifa kwamba kuna baadhi ya wanafunzi hawaandikishwi eti kwa sababu hawana uwezo, wanakaririshwa darasa la sita. Baada ya kufanya ufuutiliaji, tumegundua hizi ni shule za Serikali takribani 32,000 ambao tuliagiza warudishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kwamba Serikali inapopata taarifa kama hizo, tunafanya kazi kwa sababu, wakati mwingine shule inakuwa inasajiliwa na inakuwa na wanafunzi, lakini ni vigumu sana kujua kwamba labda huyu ni mwanafunzi ambaye ameonekana amefeli kwenye shule fulani ndiyo akapelekwa.

Kwa hiyo, natoa wito kama ambavyo Mheshimiwa Musukuma ametoa taarifa, nitafuatilia na hatua tutachukua. Kama kuna shule nyingine ambazo mnazifahamu Waheshimiwa Wabunge au raia ye yote mwema, hata hizo tulizogundua za darasa la saba ni kutokana na raia mwema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niwashukuru sana Watanzania ambao wanapoona ukiukwaji wa elimu wanatoa taarifa na tutaendelea kuchukua hatua kadri ambavyo inatakiwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nicodemas Maganga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi naomba ufanuzi. Mwaka 2020 tulinadi majukwaa mengi kwenye llani ya Chama chetu cha Mapinduzi kwamba kila wilaya itapata Chuo cha VETA. Naomba ufanuzi kwenye Wizara ya Elimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ufanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya VETA nimeyaelezea na katika baadhi ya hoja ambazo nilikuwa nimejaribu kuitia hapa, ni pamoja na ujenzi wa vyuo vya VETA nchini na nilielezea kwamba tuna vyuo 42 ambavyo tayari vimekamilika na vinaendelea na mafunzo na vyuo vingine 33 viko katika hatua mbalimbali za ujenzi. Nikasema mwishoni kabisa kwamba, tuna mpango mkakati wa kujenga vyuo katika kila wilaya na katika kila mkoa nchini kwa kadri upatikanaji wa fedha utakavyokuwa unaruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi, aondoe hofu, Serikali iko makini, itakwenda kutekeleza ahadi yake kwa kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana. Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia Theonest.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wote tunatambua umuhimu wa Idara ya Udhibiti Ubora. Pia, wachangiaji wengi na ukisoma ripoti ya CAG inaonyesha upungufu, uwezo mdogo na kutotiliwa mkazo kwa Wizara katika kuwekeza katika Idara hii ya Udhibiti Ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitaji *commitment* ya Serikali katika kuhakikisha *at least* kila Kata inakuwa na wadhibiti ubora na fedha iwe inaenda. Ili elimu yetu iweze kuboreka ni lazima tuwe na wadhibiti ubora. Kuna wengine wameenda mbali zaidi wakasema wadhibiti ubora ndio *ma-CAG* wa elimu. Tunategemea kupata elimu gani bora bila kuwa na *ma-CAG* wa kada hiyo? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitaji *commitment* ya Serikali na kama sitaridhika, nitashika shillingi. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ufanuzi. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda kwanza kushukuru kwa watu kuendelea kuisemea udhibiti ubora, kwa sababu katika michango wengi wanazungumzia udhibiti ubora. Nami nikiri kwamba hilo ndiyo jicho letu, kwamba wanatuangularizia elimu inakwendaje, wanatupa taarifa na ndiyo maana ukiangalia katika miaka mitatu iliopita, Serikali imewekeza sana kwenye udhibiti ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga ofisi za wadhibiti ubora 155, tulikamilisha 100 na katika mwaka huu wa fedha tumejenga tena 55, lakini mwaka 2020 tulinunua magari 45, mwaka huu tumenunua 37 na kuna mengine 12 yanakuja mwezi ujao, Juni. Pia, tumeongeza fedha ambazo tunatoa. Ni kweli kwamba hii Idara ilikuwa na changamoto hata fedha za mafuta hawapelekewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba pamoja na jitihada hizi, bado jitihada zaidi zinahitajika kuwekeza. Kwa

hiyo, tutaendelea kuwaongezea bajeti kadri ambavyo fedha zinapatikana. Nashukuru sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamis Tabasam.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika ufanuzi wa Mheshimiwa, Waziri aje anieleze katika Jimbo langu la Sengerema tuna vyuo vitatu; *FDC* Karumo, *FDC* Sengerema na tuna Chuo cha *VETA* kwa Mchima pale eneo la Nyatukala. Vyuo hivi havina vifaa vyovoyote kwa ajili ya ufundi na amesema katika bajeti yake kwamba kuna milioni 500 ambazo alikuwa ametoa kwa ajili ya kununua vifaa. Sasa, hatujui Sengerema hivi vifaa vimepelekwa wapi?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Tabasam. Nadhani Mheshimiwa Waziri ameshasikia hiyo hoja, lakini kwenye mshahara wa Waziri, huwa unauliza jambo lile la jumla la kisera, siyo la eneo lako mahususi. Hata hivyo, Serikali mko hapa, Naibu Waziri upo, Waziri upo mtazitafuta hizo fedha zilizokwenda maana inaonekana zimepotea.

Sijajua Halmashauri ya Mheshimiwa Tabasam ni kwa nini kila fedha inavyoonekana zikienda zinapotelea mahali. Kwa hiyo, mfanye utaratibu nadhani maalum, fedha zikienda huko zinapotelea wapi? Sijui zinaishia ziwani kabla hazijavuka? Kifungu kinaafikiwa?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh.952,267,501
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning Department</i> .....	Sh.2,074,924,212
Kifungu 1004 - <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh.1,105,411,000
Kifungu 1005 - <i>Procurement Management Unit</i> ..	Sh.679,727,164
Kifungu 1006 - <i>Government Communication Unit</i> .....	Sh.498,972,700
Kifungu 1007 - <i>Legal Unit</i> .....	Sh.341,640,000

Kifungu 1008 – <i>Information Communication</i>	
<i>Technology and E-Learning.....</i>	Sh.468,619,000
Kifungu 2001 - <i>Basic Education Development</i>	
<i>Office.....</i>	Sh.32,989,205,632
Kifungu 2002 - <i>School Quality Assurance.....</i>	Sh.36,599,275,659
Kifungu 5001 - <i>Teacher Education.....</i>	Sh.26,106,822,000
Kifungu 7001 - <i>Higher Education.....</i>	Sh.278,893,017,480
Kifungu 7002 – <i>Technology and Vocational Training</i>	
<i>Division.....</i>	Sh. 50,229,664,189
Kifungu 8001 - <i>Science, Technology and</i>	
<i>Innovation.....</i>	Sh. 41,752,535,399

*(Vifungu viliyyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **FUNGU 18 – TUME YA TAIFA YA UNESCO**

Kifungu 1001 - <i>Administration and Human Resource</i>	
<i>Management.....</i>	Sh.2,254,777,000
Kifungu 1001 - <i>Administration and Human Resource</i>	
<i>Management.....</i>	Sh.11,500,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **MIPANGO YA MAENDELEO**

### **FUNGU 46 – WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Kifungu 1001 - <i>Administration and Human Resource</i>	
<i>Management.....</i>	Sh.11,500,000,000
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning</i>	
<i>Department.....</i>	Sh.44,272,494,800
Kifungu 2001 - <i>Basic Education Development</i>	
<i>Office.....</i>	Sh.124,408,761,763
Kifungu 2002 - <i>School Quality Assurance.....</i>	Sh.9,600,000,000
Kifungu 5001 - <i>Teacher Education.....</i>	Sh.21,202,120,120
Kifungu 7001 - <i>Higher Education.....</i>	Sh.591,037,509,693
Kifungu 7002 – <i>Technology and Vocational</i>	
<i>Training Division.....</i>	Sh.82,322,982,804
Kifungu 8001 - <i>Science, Technology and</i>	
<i>Innovation.....</i>	Sh.19,594,053,820

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imemaliza Kazi yake.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Bunge linarejea.

*(Bunge Lilitrudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Mtoa hoja taarifa.

## **T A A R I F A**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
*(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa kwa utaratibu wetu nitawahoji kuhusu hoja hiyo ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ya kupokea na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu,  
sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022  
Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kujadili hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na mimi kwa niaba yenu nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuleta hoja ambayo ni nzuri na sasa imeweza kupitishwa na Bunge. Kwa hiyo kwa nafasi hii niwapongeze sana Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wenu wote ambao wapo hapa na wengine hawapo, lakini tunawapongeza kwa kazi nzuri. Waheshimiwa Wabunge wamekubaliana nanyi na wamewapitishia Mafungu kama mlivyo kuwa mmeomba. Kwa hiyo tunawatakiwa kila kheri katika utekelezaji na yale ambayo mmewaa hidi Waheshimiwa Wabunge kwamba mnakwenda kuyafanya katika mwaka wa fedha ujao, tunaamini mtayafanya hayo kama mlivyo ahidi na tunawatakia kila la kheri.

Pia niwashukuru Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ambayo inashughulika na Wizara hii, kwa kazi nzuri waliyoitoa na mawazo yao mazuri ambayo yameifanya Wizara kuleta bajeti ambayo inaanishi yale ambayo tunayataka yafanyike kwenye jamii zetu kwenye upande wa elimu, sayansi na teknolojia. Tunawashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, vile vile mmtoa michango mizuri ambayo itawasaidia katika utekelezaji wa Wizara. Yapo mambo mbalimbali ambayo Waheshimiwa Wabunge wametamani waone mabadiliko na naamini mtayafanya kazi kwa kadri walivyotoa mawazo yao. Mengine pengine siyo ya kuyafanya kazi, lakini ni kwenda kuyafanya utafiti zaidi ili muone hoja zao zina uzito kiasi gani na zinaweza kutekelezwaa kiasi gani. Nafahamu muda ulikuwa mfupi kidogo, kwa hiyo, hamkupata muda wa kufafanua hoja nyingi, lakini hoja nyingi mzichukue mkazifanyie kazi. Kwa mfano, hoja ya Watoto wa shule kulazimika kuvalaa shati nyeupe, pengine kulikuwa na sababu za msingi wakati huo, je wakati huu bado hiyo sababu ipo? Kama haipo hayo ni mambo ambayo mnawenza kwenda kuyatazama.

Naamini mngepata nafasi mngetaka kuyatolea ufanuzi hayo yote, lakini ni muhimu kwenda kuangalia hasa Mheshimiwa Waziri wa Elimu unatoka kule Kigoma na ukipita maeneo mengi Kigoma kwa sababu ya ardhi yake ambavyo ina rutuba, ina wekundu wa ziada, kwa hiyo mazingira kama yale mnawenza kuangalia umuhimu wa jambo hili.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka pia Mheshimiwa Spika alikuwa amesisitiza sana juu ya jambo linalohusu usajili wa shule. Hilo nalo mkalitazame kwa uzito unaostahili kwa sababu wananchi wanapojoitoa kujenga shule ili watoto wao wasiende mbali ni muhimu sana Serikali ikaziona juhudii hizo za wananchi na ninyi mkaingia kuanzia hapo. Sasa hoja ya usajili ni moja, lakini kumalizia hizo shule ni hoja ya pili. Kwa hiyo kulingana na hao Wadhibiti Ubora hicho watakachokuwa wamekiona, maadam wananchi wameshakwenda hatua kadhaa, mnawenza mkatengeneza utaratibu mzuri kwamba ikifiki hapa tutaweza kusajili, lakini madarasa angalau ukisema ya awali yakiwepo mangapi waanze. Ukitisema unasubiri mpaka yote yakamilike unaleta changamogo. Wakianza ni rahisi na wewe kuanza kufuatilia ubora wakati huo, kuliko kufuatilia ubora watoto wameshafika darasa la sita na wewe haukuwa na taarifa na hiyo shule. (*Makofii*)

Kwa hiyo namna alivyokuwa amesisitiza Mheshimiwa Spika, ni muhimu mkalichukua kwa uzito hasa kwa kuzingatia kwamba wananchi wanataka wapate hizo huduma karibu na maeneo yao. Kwa hiyo hilo ni eneo mojawapo mnawenza mkaamua kuwa mnatoa usajili wa muda, halafu mtazame maendeleo yanaendaje, halafu baadaye mnaingia nyie kumalizia kama mnavyokamilisha maboma hata hizo shule mnao uwezo wa kuzikamilisha pengine kwa awamu. Hayo nayo mtayatazama. (*Makofii*)

Jambo lingine ambalo limezungumzwa hapa kwa uzito na ni muhimu ninyi kama wizara nadhani wananchi kidogo wakati mwingine kama Waziri alivyosema hata sisi Waheshimiwa Wabunge tunawachanganya kidogo na kauli zetu. Kwa sababu wakati mwingine, kuna muda kwa sababu

hili jengo jamani tuna kanuni zetu sawa, lakini kuna muda wa masihara, halafu mtu akifanya yale masihara hasemi kama wakati huo anafanya masihara. Kwa hiyo likichukuliwa kule nje linachukuliwa Bunge limesema hawajui hata Bunge utaratibu wake wa kufanya maamuzi ni lazima mhojiwe, lakini akishachangia Mbunge kwa sababu ya hadhi ile uliyonayo Mheshimiwa Mbunge, inachukuliwa kwa uzito sana. Kwa hiyo, tuchunge hata sisi namna tunavyozungumza haya mambo yetu hasa yanayohusu elimu.

Kama tuna changamoto hapa na pale tutazame namna nzuri ya kufikisha ujumbe kuliko kuwapelekea vijana wetu ujumbe ambao tunakuwa hatuuweki vizuri. Tunatamani watoto wetu, vijana wetu wasome, tena wasome sana, kwa sababu ipo siku na sisi tunataka watoto waende huko mwezini. Sasa huko mwezini watoto wetu watafika vipi kama tunataka kuendesha mfumo wetu wa elimu kwa namna hili ambayo tunarahisisha rahisisha hivi, hapana. Tusichukulie kwamba elimu hii ya darasani labda irahisishwe ama ifanywe kwa namna ile ambayo haipaswi, hapana, isipokuwa mawazo yote yaliyotolewa ni ya muhimu na yote yafanyiwe kazi.

Maeneo ya wafugaji, muangalie namna mnavoyeza kuboresha mitaala ili mtoto wa mfugaji akienda pale basi aweze kuhudumia na mifugo ya wazazi wake au kitalu cha uvuvi, namna hiyo, lakini tusifike mahali tukaifanya elimu yetu kama haina thamani kwa sababu hata sisi tutataka kwenda mwezini siku moja na ili twende huko lazima twende kwa utaratibu mzuri ambao dunia nzima inakwenda namna hiyo, kwa hiyo elimu lazima tuiheshimu.

Waheshimiwa Wabunge, kuna jambo moja ambalo huwa tunalifanya sana hapa ndani; hasa lile la kusema nataka; kuna sentensi imezoeleka sana sasa ni kama inakuwa ya Kiswahili mtu anasema sasa nataka *nidiklee interest*. Kwanza sio Kiswahili, *nidiklee* ndio nini? Kwa sababu ukilitafuta kwenye kamusi halipo, kwa hiyo niwakumbushe tu Kanuni ya 68 mtu ukisimama, ukisema jambo hili nina maslahi nalo, lazima utueleza una maslahi ya kifedha kiasi gani? Sio maslahi

ya mimi ni Mjumbe wa Kamati, hapana, sio maslahi ambayo yanakatazwa kwenye kanuni zetu. Wala sio maslahi ya kwamba mimi nilishawahi kufanya kazi kwenye kampuni hii, hapana. Labda kama unayo maslahi ya kifedha kwa lile unalotaka kulizungumza, kwamba Kampuni fulani hajjalipwa fedha na nini mimi mwenyewe kule kuna bilioni mbili zangu, hilo lazima uliseme. Kwa sababu ukishasimama ukasema nina maslahi, lazima utueleze kiwango cha maslahi yako. Usiseme mimi Mjumbe wa Kamati, mimi ni mwali muwenzao, mimi sijui na nini, hapanal! Hayo siyo maslahi ambayo kanuni zetu zinakusudia kusema. (*Makofi*)

Tutofautishe, ni tofauti na maslahi ya kule mahakamani kwa sababu kule mahakamani, yule hakimu anafanya maamuzi; kwa hiyo yeye ni maslahi ya namna yoyote ya undugu, ya nini, yote hayo yanatazamwa. Humu ndani maamuzi yetu yanatokana na Bunge zima kuhojiwa. Kwa hivyo, Mbunge anakatazwa maslahi haya ya kifedha kwa sababu anawashawishi Wabunge kuamua.

Kwa hiyo kuna tofauti, tusiwe tunajipotezea sisi wenyewe muda wetu wa kuchangia. Unasema nina maslahi halafu tutakapokuuliza kikakuni; natakiwa nikuulize, maslahi yako ni kiasi gani? Halafu huwezi kuyasema. Kwa hiyo tuipitie Kanuni yetu ya 68 ili tuwe tunayatumia hayo maneno mahali yanapostahili.

Sasa Waheshimiwa muda wetu umekwenda lakini Mheshimiwa Shigongo alikuwa amesimama kuomba mwongozo kwa maana ya kwamba kuna jambo hapa ndani limefanyika ambalo liko kinyume na Kanuni. Mheshimiwa Shigongo.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilisimama kwa Kanuni ya 76 na nilitaka tu kueleza wazi sikuwa nimeridhishwa sana na majibu yaliyotolewa kuhusiana na suala zima la ubunifu. Nilitaka nipewe mwongozo wa Spika naweza kufanyaje baada ya hapo? Maana yake kuna

watoto wengi sana nilikuwa nazungumza hapa sio kwa faida yangu, kwa *interest* ya watu wengine ambao wanahitaji kupata elimu. Kwa hiyo nilikuwa nahitaji tu, maana pale kwa,sababu ya,kutokufahamu nafikiri; sikuomba kutoa hoja kwa hivyo sikupata *support*ya Wabunge wengine. Kwa hiyo, nilikuwa naomba tu nielekezwe namna ninavyowenza kufanya kwa sababu, nilitembelea *TRIDO* juzi kuna mtoto ametengeneza *bulb* anaizima kwa kusema maneno na yule kijana amekomea *form four* peke yake. Kijana huyu anahitaji elimu ya Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Sawa, Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 76 inazungumza kuhusu mwongozo wa Spika na kanuni hii unaweza kuomba mwongozo ili Kiti Kitoe ufanuzi Ikiwa jambo lilofanyika hapa Bungeni linalohusia au haliruhusiwi. Kutokuridhishwa na ufanuzi au majibu huwezi kuomba Mwongozo.

Sasa ameuliza nini kifanyike, nadhani tunarudi palepale kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri ya kuruhusu mapitio. Kwa sababu nikianza kuongea nitazungumza mawazo yangu mimi kuhusu huyu kijana, jambo ambao halitakuwa zuri kwa sababu itaonekana Bunge linawatazama namna fulani hivi vijana wetu wabunifu ambao hawakusoma sana, hapana. Taratibu zao zimebekwa na ziko wazi, kijana mbunifu anaweza kusaidiwa kwa namna gani!

Nadhani wote mnafahamu kwamba Bill Gates hakumaliza Chuo Kikuu cha Harvard, wote tunamfahamu *Bill Gates* si ndiyo jamani!

**WABUNGE FULANI:** Ndiyoo.

**NAIBU SPIKA:** Tufuatilie hata historia za hawa watu wengine ule ubunifu wao, ule ubunifu wao, naambowi alizaliwa Mwanza, sawa. Ule ubunifu wao una njia nytingine, kile kitu chake kitakapotambuliwa, basi ule utambuzi wa lile

jambo alilolifanya sina hakika sana sisi kama Bunge tunafikiri kumtambua kwa kumpa cheti kwamba huyu pengine ana *Ph.D* kwa sababu ya huu ugunduzi ndicho tunachokitafuta. Kwa hiyo, tuliepuke hilo tuwape fursa Wizara wakafanye hao mapitio, waweke utaratibu mzuri wa kumtambua huyu kijana hata kama kupewa *degree* labda apewe ya heshima, kama ambavyo Waheshimiwa wengi tu humu ndani wanapewa *degree* za heshima, lakini sio lazima awe anaitwa daktari. Kwa hiyo mambo kama hayo, sasa sitaki kuyasemea sana kwa sababu sijafanya huo utafiti na sina taarifa ya kutosheleza. (*Makofii*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Shigongo, nadhani yale mawazo yako katika hiki kipindi cha mapitio, ni vizuri uwapelekee Wizara waone namna ya kuboresha zile changamoto zilizokuwepo huko nyuma ambazo ziliwapelekea kufuta huu utaratibu, basi nadhani watazifanya kazi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

(*Saa 12.04 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 6 Mei, 2021 Saa 3.00 Asubuhi*)